Msururu wa
FATAKI

Chozi la Heri

Assumpta K. Matei



OnePLANET

3701-

Fasihi Tambuzi ya Kiafrika: Riwaya

Chozi la Heri

Fasihi Tambuzi ya Kiafrika (FATAKI)

1. Sahani ya Hoho – Zake Yaona
2. Chozi la Heri – Assumpta K. Matei
3. Usiku wa Mashaka – Ngulamu Mwaviro
4. Nargisi Michongomani – Johnson Nzaro
5. Nisamehe Mama – Ben Mkota

Chozi la Heri

Assumpta K. Matei

OnePLANET

Published by
One Planet Publishing & Media Services Limited
PO Box 7070 – 00200, Nairobi, Kenya
Email: info@oneplanetpublishing.com
Website: www.oneplanetpublishing.com

© Assumpta K. Matei 2014

The moral rights of the author have been asserted.

First published 2014
Reprinted 2015 (thrice)

All rights reserved. No part of this publication may be reproduced or transmitted in any form or by any means, electronic or mechanical, including photocopy, recording or any information storage and retrieval system, without the prior written permission of One Planet Publishing & Media Services Limited.

Enquiries concerning reproduction may be sent to the Publishing Department, One Planet Publishing & Media Services Limited, at the address above.

ISBN 978 9966 068 18 7

Design and layout by Paul Murunga
Cover illustration by Robert Kambo

Printed by
Printing Services Ltd
PO Box 32197 – 00600, Nairobi, Kenya

PL
8704
M3487
C46
2015

Sura ya Kwanza

Ridhaa alisimama kwa maumivu makali, mikono kairudisha nyuma ya mgongo wake uliopinda kwa uchungu. Macho yake yaliyotanda ukungu alikuwa kayatunga juu angani, akitazama wingu la moshi lililojikokota kwa kedi na mbwembwe; wingu lililomnywesha na kumkumbusha ukiwa aliozaliwa nao na ambao alihofia kuwa angeishi na kuzikwa kwao. Mara aligeuka, akawa anatazamana ana kwa ana na tanuri la moto ambalo lilikuwa linaliteketeza jumba lake la kifahari huku likimfanyia taadi kana kwamba linamhakikishia kuangamia tena kwa nguvu zake.

Sasa anakumbuka vyema. Anakumbuka kupepesa kwa jicho lake la kulia kwa muda wa wiki mbili mtawalia. Anakumbuka anguko ambalo alianguka sebuleni mwake, akatafuta kilichomfanya kujikwaa asikione. Anakumbuka mavune yaliyouandama mwili wake na kuunyong'onyeza kwa muda hata pasi na kuudhili kwa kazi yoyote ya haja. Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba yake ya nyumbani adhuhuri ya juzi ile. Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama. Milio hii ndiyo iliyomtia kiwewe zaidi kwani bundi hawakuwa wageni wa kikaida katika janibu hizi. Anakumbuka akimwambia Terry, mke wake, "Milio hii ni kama mbiu ya

mgambo, huenda kukawa na jambo." Terry, kwa ucheshi wake wa kawaida, hakunyamaza.

"We nawe huishi kufanya tumbo moto! Kila jambo kwako lazima liwe na kiini? Utakuja kujitia fadhaa bure. Ninashangaa vipi daktari mzima hapo ulipo unajishughulisha na mambo ya ushirikina. Si wewe unayeniambia kila siku kuwa ni muhimu kuikwangura sagamba hiyo ya mielekeo ya kijadi ambayo inayafifilisha maendeleo? Na hata kukawa na jambo, *what can you do?* Mlaani shetani," alisema Terry huku akiendelea na shughuli zake kana kwamba hajasema lolote, kisha akamgeukia mumewe tena na kusema, "Si wewe unayeniambia kila mara kwamba hata mtu akijitia wasiwasi vipi hawezi kuongezea hata pima moja katika maisha yake," akaendelea Terry, "kwamba liandikwalo ndilo liwalo? *Since when has man ever changed his destiny?*"Alimalizia Terry ambaye alipenda kuchanganya ndimi anapozungumza.

Ridhaa akamwambia, "Wewe endelea kupiga hulu tu, lakini utakuja kuniambia!"

Laiti Ridhaa angalijua kwamba hii ndiyo iliyokuwa mara yake ya mwisho kuzungumza na mpenzi mkewe! Angalikamia kutumia kila sekunde ya dakika za uhai zilizokuwa zimesalia kumuuliza mkewe maswali haya ambayo sasa yameivamia akili yake!

Machozi yalifurika machoni, yakayaziba, na kuulemaza uwezo wake wa kuona. Moyo wa Ridhaa ulipiga kidoko, ukataka kumwonya dhidi ya tabia hii ya kike ya kulia pindi mtu akabiliwapo na vizingiti ambavyo ni kawaida ya maisha, ukamkumbusha maneno ya marehemu mama yake siku za urijali wake.

"Ridhaa mwanangu, mwanamume hufumbika hisia. Machozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha. Huku ni kujiumbua hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi; ulitunukiwa makoo," angesema bibi huyu ambaye alikuwa kabugia chumvi ya maisha ikamrishai.

Leo hii Ridhaa hakujali la mama wala la baba. Alisukuma kekevu moja kuu ambayo ilichimbua milizamu ya machozi iliyoshindana kufanya njia nnenne kwenye mashavu yake yaliyozimiliki sharafa za ndevu. Alijihisi kama mpigana masumbwi aliyebwagwa na kufululiziwa makonde bila mwombezi. Hata hivyo, Ridhaa hakuhitaji mwombezi wala mwamuzi katika kitali hiki. Alisalimu amri, akayaacha machozi yamvamie yatakavyo, yautakase undani wake ambao ulikuwa unatuta na kutoa usaha kwa kuvunjikiwa. Katikati ya mito hii ya machozi, Ridhaa aliileta picha ya maisha yake mbele ya kipaji chake. Alijiona akiamka asubuhi ambayo ilizaa usiku wa jana, usiku ambao ulitandaza kiza katika maisha yake. Kwa mbali alianza kuisikia sauti ya mkewe ikilia kwa kite.

"Uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni! Uuuui! Uuuui! Mzee Kedi, usituue, sisi tu majirani! Maskini wanangu! Maskini mume wangu!"

Anakumbuka akisikia mlipuko mkubwa, kisha kushikwa na uziwi wa muda uliofuatwa na sauti nyingine ya mkewe,

"Yamekwisha!"

Kumbukumbu hii ilimpa kuzimia. Alipozinduka alijipata kalala kando ya gofu la jumba lake lililokuwa linafuka moshi. Alijaribu kuinuka na kujikongoja kwa maumivu. Alitembea tata hadi kwenye shamba lililokuwa karibu na jumba lake—

la kiunzi hasa cha jumba. Aliyainua macho yake, akatazama visiki vya mihindi vilivyoutwaa weusi wa mashizi kutokana na dhuluma ya moto, akapaza sauti na kusema, "Familia yangu na mali yote hii kuteketea siku moja? Bila shaka hili ni zao lingine la husuda."

Ridhaa alirudi nyumbani na kusimama katikati mwa chumba ambacho yeye na aila yake walikuwa wamekitumia kama sebule kwa miaka na mikaka. Chumbani humu ndimo kilio cha kwanza cha kilaika kifungua mimba wao kilipohanikiza miaka thelathini iliyopita. Ridhaa anaikumbuka siku hiyo vyema. Alikuwa amesafiri kwa shughuli za ujenzi wa taifa, kama alivyoziita safari zake za kikazi. Uchungu wa mwanagenzi ukawa haujui simile, ukabisha hodi, naye Mwangeka akazaliwa. Hakuna aliyejua kuwa miaka thelathini baadaye, mwana huyu ndiye angebakia kumkumbusha Ridhaa kuwa alikuwa na familia.

"Mwangeka," alisema Ridhaa kupitia kwenye sauti ya mawazoni mwake, "kumbe wewe ni sawa na yule Mwangeka wa kihistoria ambaye kivuli chake kikitembea siku zote mbele yake, ambaye mwili wake ulikuwa kaka tu, roho yenyewe iliishi nje ya kaka hili kwa kutotaka kudhibitiwa? Umewezaje kunusurika? Kumbe wadhifa waliokupa wa kwenda kudumisha amani katika Mashariki ya Kati umetokea kuwa wongovu wako? Maskini Lily mkaza mwanangu! Umekuwa kama jani linalopukutika msimu wa machipuko! Umetoweka katika ulimwengu huu ukiwa teketeke, hata ubwabwa wa shingo haujakutoka!"

Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na

mjukuu wake, Becky. Anawaona wote mbele ya macho yake yaliyojaa mavune. Anamsikia mjukuu wake, Becky, akimwita, "Babuuuu!" Anakumbuka mjadala mkali aliokuwa nao na bintiye, Tila, kuhusu mafanikio ya baada ya uhuru, mjadala ambao hakuna mmoja katika aila yake aliyethubutu kuuchangia kwani kwenye masuala ya sheria na siasa, hakuna aliyempiku Tila.

"Baba, umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusimama dede?" Tila alimuuliza babake siku moja katikati mwa jadhba.

"Naona umeanza kuitia akili yangu kwenye mtihani mgumu. Unanichanganya hasa! Kwanza sijui wapi kapata mtoto wa miaka hamsini. Pili kusota na kusimama dede huhusishwa na vitoto vikembe, si mibaba ya miaka mingapi vile?"

"Lakini baba, wewe siwe uliyeniambia kuwa mashamba ya Theluji Nyeusi yalikuwa milki ya wakoloni? Na sasa yanamilikiwa na nani? Si mwana wa yule mlowezi maarufu ambaye wewe hunitajia kila mara? Maekari kwa maekari ya mashamba katika eneo la Kisiwa Bora yanamilikiwa na nani? Si yule Myunani ambaye amewageuza wenyeji kuwa maskwota katika vitovu vya usuli wao? Basi niambie, baba, unatumia mantiki gani kusema kuwa sisi si watoto wa miaka hamsini? Je, miaka hamsini ya uhuru imetukuza kiuchumi au tumebaki kuwa wategemezi wa hao hao ambao walitupa uhuru? Hatuna tunalolimiliki. Wageni ndio wanaoamua wakuze nini katika ardhi yetu! Tunabaki kuwategemea, si kwa lishe tu, bali pia kwa ajira. Na kazi zenyewe si kazi, ni vibarua vya kijungu jiko tu. Imekuwa tunaubadili ule msemo

wa mtegemea nundu haachi kunona. Sisi ndio tunaotumiwa kuikoleza hiyo nundu mafuta! Na si hayo tu baba, hata kidogo tunachokikuza chaenda kumfaidi huyo huyo aliyetupa uhuru. Sijui kwa nini hatujaweza kujisagia kahawa au chai yetu. Itakuwaje mbegu ziwe zetu, tuchanike kulikuza zao lenyewe, kisha tumpelekee mwingine kwenye viwanda vyake, alisage na kutuuzia hiyo hiyo kahawa na chai kwa bei ya kukatisha tamaa?"

"Ni kweli binti yangu, kwa kutumia falsafa hii, una haki ya kusema sisi tu watoto wa miaka hamsini," Ridhaa sasa analiambia lima la jivu ambalo anaamini ndilo mabaki ya mwili wa bintiye. Na binadamu yeyote angekubaliana naye. Fikiria wewe, mtu aje kutoka huko, anyakue ardhi, alime, afuge, kisha miaka hamsini baada ya kifo chake, bado anakuuzia maziwa yaliyoganda kutoka huko ahera aliko! Hili usilione kama mzaha! Mara ngapi umesimama kwenye *Shopping Mall* yake ukiwa safarini, ati unapumua kutokana na uchovu wa safari, kumbe waenda kumwongezea ngawira yake!

"Ni kweli asemavyo Tila," Ridhaa anayarudia maneno haya akilini, "mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikaji wa ardhi na Waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa ... yote yakapata wenyeji wageni ... dau la Mwafrika likagonga jabali. Waafrika, akiwemo Baba Msubili, walilazimika kuwa, ama vibarua katika mashamba yaliyokuwa yao, au maskwota ambao maisha yao

yalitegemea utashi wa Mzungu. Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadogowadogo, maskini, wasio na ardhi. Nadhani unaweza kukisia hali ilivyokuwa kwa familia nyingi za Kiafrika. Kama vile Baba Msubili alivyokuwa akisema, jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambamo Wazungu wangeamua kuchukua vibarua kupalilia mazao yao. Vijulanga vilinyakuliwa kwa lazima kutoka kwenye susu zao, hata vifua havijapanuka, vinapelekwa katika maeneo mbalimbali nchini kufanya kazi."

"Hadi sasa hali hii haijabadilika, nakubaliana na Tila," Ridhaa anajiambia. "Ama hii ndiyo ile wanayoiita, *Historical Injustice*?" Ridhaa alimuuliza Tila mawazoni.

"Lakini itakuwaje *historical injustice*, nawe Ridhaa, hapo ulipo sicho kitovu chako?" Ridhaa aliendelea kujisaili na kukaribia kujisuta.

Ridhaa hakuwa mkazi asilia wa Msitu wa Heri. Alikuwa 'Mfuata Mvua', kama walivyoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki. Hakupachagua mahali hapa, majaliwa yalitaka, na majaliwa yana nguvu! Baba yake yasemekana alikuwa na wake kumi na wawili. Unajua zama hizo hali ilivyokuwa! Mzee mwenye wake na wana wengi alihesabiwa kuwa mkwasi kwelikweli. Basi wake hawa hawakuchelea kutimiza amri ya maumbile, wakapania kuujaza ulimwengu! Ardhi ya Mzee Mwimo Msubili ikawa haitoshi kuyalelea madume yake ishirini. Iligawanywa hadi ikawa vikataa, ikalimwa na kupaliliwa mpaka ikachoka. Hatimaye Mzee Mwimo Msubili

alijiona amekabiliwa na kibarua kigumu cha kuvilisha vinywa hivi kutokana na zao dogo alilolipata.

Wana wa Mzee Mwimo Msubili walianza kubanana katika vipande vidogo vya ardhi, na bila shaka unajua kawaida moja ya maumbile ni kwamba chochote kinachobinywa na kukandamizwa hujaribu kufurukuta ili kupata nafasi ya kupumua. Hata kipungu anapoona wanawe wamelimatia sana kutoka kiotani kwenda kujitegemea, yeye hukifanya kiota kukosa faraja ya kawaida kwa kukijaza miiba, nao vifaranga wake huona kuwa wakati wao wa kupambana na dunia umefika. Bila kuambiwa hujua kuwa wamefukuzwa! Ndivyo ilivyokuwa katika familia ya Mzee Mwimo Msubili. Wingi wa vinywa vya kulishwa ulizua uhasama, migogoro na uhitaji mkubwa. Mzee Mwimo akaona ku moto, akaamua kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa Heri au Ughaishu, kama walivyouita watu wa huko. Siku hizo ilikuwa rahisi kwa mtu kuwa na mashamba kokote katika eneo lililomilikiwa na kabila lake kwani umiliki wa mashamba ulitegemea bidii ya mtu. Ridhaa aliangukiwa na bahati kwani mama yake ndiye aliyekuwa mke wa mwisho.

Ridhaa alikuwa na umri wa miaka kumi walipohamia humu. Hakuwa ameanza shule. Sasa anapiga darubini na kuona maisha yake mwezi mmoja baada ya kuwasili Msitu wa Heri. Hamkuwa na wakazi wengi, kwa hivyo alikosa ushirika wa ndugu zake. Ilimchukua muda kuzoeana na watoto wa majirani ambao waliwaona Ridhaa na ndugu zake kama waliokuja kuvuruga utulivu wao. Hata anapowazia haya, Ridhaa anafahamu fika kuwa hali hii ilizuliwa na wakoloni na kuwarithisha Waafrika. Anakumbuka baba yake, Mwimo Msubili, akimwambia,

"Kabla ya miaka ya hamsini, umiliki wa kibinafsi wa ardhi haukusisitizwa katika jamii yetu. Ilipotokea kwamba kulikuwa na upungufu wa ardhi katika eneo fulani, watu wangehama na kuishi na watu wa ukoo mwingine. Lilikuwa jambo la kawaida kuwapata watu wakiishi na kulima katika mashamba ya majirani, marafiki na jamaa. Baada ya kuyalima mashamba haya kwa muda, yaliishia kuwa yao. Hawakuhitajika kuyanunua kama mnavyofanya sasa. Hii ndiyo sababu uliyoiona familia ya Mzee Shamu ikiishi miongoni mwetu mle Ukungu, na hali inatoka kwenye jamii ya Kambirani. Hatua ya mkoloni ya kupuuza sera za Mwafrika za umiliki wa ardhi, na kuamua kujumuisha pamoja ardhi iliyomilikiwa na mtu binafsi, na kuuidhinisha umiliki huu kwa hatimiliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii. Katika sera ya kijadi ya umiliki na matumizi ya ardhi, raia wote, hata wageni, walikaribishwa na kugawiwa mashamba, hivyo kupata mbinu za kuyaendeshea maisha. Sera mpya ya umilikaji nafsi wa ardhi ilimaanisha kwamba wale waliokosa pesa za kununulia mashamba wangekosa mahali pa kuishi. Na hata wale waliobahatika kuwa na pesa za kununulia mashamba daima walichukuliwa kama wageni wasiopasa kuaminiwa."

Ridhaa alikuwa mmoja kati ya waathiriwa wa hali hii. Anakumbuka jinsi siku ya kwanza shuleni alivyotengwa na wenzake katika mchezo wao wa *Kavuta*, mchezo wa kusukuma vifuniko vya chupa za soda kwa ncha za vidole vyao. Anakumbuka mwanafunzi mmoja ambaye kwa kawaida alipenda kuwachokoza wenzake akimwambia,

"Wewe ni Mfuata Mvua. Hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda katika mitihani yote. Wewe ndiwe unayetuibia kalamu zetu ..."

Ridhaa hakungoja mwenzake amalize dukuduku lake. Alichukua mkoba wake na kufululiza moja kwa moja hadi nyumbani na kujitupa chini mchangani (siku hizo hakukuwa na haya makochi ya kujimwaya wanakojitupa watoto wanaolilia pipi!). Alilia kwa kite na shake. Alimwambia mama yake kuwa hangerudi shuleni tena, kwamba hangewapa wenzake cheko la kumchekea.

Mama Ridhaa alisikiliza malalamishi ya mwanawe, akamwambia, "Mwanangu, ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba. Elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo wala si fujo na chuki. Mwenzako labda ana hofu kwa vile anaona uhuru wake umeingiliwa. Pengine hata ni mzaha tu. Kesho nitakurudisha shuleni. Nitazungumza na mwalimu ili awaelekeze zaidi."

Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha ya heri kwa Ridhaa. Baada ya mwalimu kuzungumza na wanafunzi na kuwasisitizia umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano, dhihaka na masimango yaliisha. Ridhaa alipea kwenye anga ya elimu, akabisha milango ya vyuo, akafikia kilelecha cha ufanisi alipohitimu kama daktari. Utendakazi wa Ridhaa ulimletea mbivu, akawa mkurugenzi wa mashirika mbalimbali yanayohusiana na huduma za kiafya. Baadaye aliamua kuuasi ukapera, akapata mke; Terry. Alijaliwa wana ambao wote sasa, isipokuwa Mwangeka, wamegeuka majivu.

"Lakini ni kipi kilichosababisha hali hii?" anajiuliza Ridhaa kwa moyo wenye uzito wa nanga, "Mzee Kedi ndiye aliyenisaidia kupata shamba hili. Mwanawe, Mhandisi Kombo, ndiye aliyeusimamia ujenzi wa jumba hili. Mkewe na mke wangu wamekuwa kama ndugu wa toka nitoke. Mimi

mwenyewe nimeyadhamini masomo ya wapwaze wawili. Sehemu hii, hasa shamba hili, kaniuzia dadake Kedi, likiwa jangwa. Mimi binafsi nimefanya juu chini kuhakikisha kijiji kizima kimepata maji ya mabomba. Eneo ambalo awali likiitwa Kalahari sasa limetwaa rangi ya chanikiwiti. Miambakofi, mivule na miti mingine mingi imepandwa. Mvua inanyesha majira baada ya mengine. Je, huu si mchango tosha wa mtu kuitwa ndugu hata angawa mgeni? Kweli jaza ya hisani ni madhila? Vipi watu wawa hawa walioniita 'Ndugu' na 'Mzee', tukala na kunywa pamoja, tukazungumza ya kupwa na kujaa wananilipulia aila na kuyasambaratisha maisha yangu?"

Ridhaa hakujua majibu ya maswali haya. Alilojua ni kwamba haya siyo aliyotumainia baada ya miongo mitano ya maisha katika maskani haya. Alitamani kupiga ukemi kumwamsha mkewe lakini akili ilimkumbusha kuwa huyo hayupo tena katika ulimwengu huu. Sasa ameanza kuelewa kwa nini wiki iliyopita vikaratasi vilienezwa kila mahali vikiwatahadharisha kuwa mna gharika baada ya kutawazwa kwa *Musumbi* (kiongozi) mpya. Anaelewa kwa nini jirani yake alikata guu kwake mara moja. Anaelewa kwa nini mke wa jirani amekuwa akilalamikia kuuzwa kwa mashamba ya wenyeji kwa wageni. Kumbe yeye Ridhaa tangu hapo alikuwa mgeni, si mwenyeji? Kumbe baada ya kuwaponya wenyeji ametupwa kama ganda la muwa?

Ridhaa hakujua alikuwa amesimama pale kwa muda gani. Miguu yake sasa ilianza kulalamika. Polepole parafujo za mwili wake zililegea, akaketi juu ya majivu—la, juu ya miili ya wapenzi wake. Baada ya muda wa mvutano wa hisia na mawazo, usingizi ulimwiba. Katika fikira zake ambazo tangu

hapo zilikuwa macho, alikumbuka taarifa ya habari kupitia kwenye runinga, taarifa ambayo japo ilitangazwa miaka minne iliyopita, ilikuwa kana kwamba anaisikiliza sasa.

Matrekta ya Baraza la jiji yamefanya kazi ya Waheshimiwa alasiri ya leo. Kwa mujibu wa habari zilizotufikia leo, matrekta hayo yalizibomoa nyumba ishirini katika mtaa wa kifahari wa Tononokeni. Ilidaiwa kwamba majumba haya yalikuwa yamejengwa mahali ambapo pametengwa kwa ujenzi wa barabara. Mengine yalikuwa yamejengwa chini ya vigingi vya nyaya za stima. Wizara ya Ardhi na Makao ikishirikiana na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano, kupitia kwa Halmashauri ya Kitaifa ya Barabara, ilikuwa imewapa notisi mabwanyenye wanaoyamiliki majumba haya.

Hata hivyo, wengi wa mabwanyenye hao walipuuza notisi hii. Wengine walionekana wakitoa milungula hadharani, wengine wakatishia kuishtaki wizara husika kwa kile walichokiita ukiukaji wa haki za umiliki mali. Hali ikawa kimya hadi leo ambapo amri ya Waziri Tendakazi ilitimizwa. Eneo hili sasa ni vifusi vitupu. Tulipozihoji baadhi ya familia zilizoachwa bila makao, zilisema kuwa wenye nyumba hizi hawajaahidiwa fidia yoyote.

Siku hiyo ambayo matrekta yakitekeleza amri ya Bwana Mkubwa, Ridhaa alitazama picha za majumba yake matatu kwenye mulishi wa runinga. Anayatazama hata sasa katika ruya yake. Majumba haya sasa yamegeuka dongo. Anasonya usingizini na kutoa kidoko ambacho karibu kimwamshe. Hili la sasa ni pigo la pili ambalo ni kali zaidi. Je, upi mustakabali wake, wa mwanawe Mwangeka na Subira, dada yake Ridhaa, ambaye aliishi maili kumi kutoka hapa?

Sura ya Pili

Ni asubuhi. Tumo katika kambi fulani—la, si kambi, mabanda hasa yaliyosongamana na kutazamana kwa jitimai na dhiki, vibanda vya mtomeo hasa. Ni siku ya kumi tangu kuondoka kwetu na kujipata katika mazingira haya mageni. Na usidhani ni mazingira mageni, kweli si mageni, si mageni kwani tu mumu humu mwetu, hatumo ughaibuni wala nchi jirani. Tu katika jimbo lile lile tulilolizoea, kilichobadilika ni kijiji tu, ni kama kutoka chumba cha malazi kwenda sebuleni!

Ugeni uliopo ni ule wa hali, mazoea na silika. Hapa tulipo tupamwe na wamwe na waliokuwa nacho na wachochole. Unaweza kusema kuna kiasi fulani cha usawa. Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni! Kile ambacho hawajui ni kwamba hata katika kifo hamna usawa! Pana tofauti kati ya mandhari wanamofia. Kuna wanaokufa wakipepewa na wauguzi katika zahanati za kijijini. Wapo wanaolala maumivu yao yakiwa yamefishwa ganzi kwenye hospitali za kifahari, wakiliwazwa na mashine, kila moja ikihimiza nyenzake kuushikilia kukutu uhai wa mheshimiwa huyu. Hawa wafapo sura zao huwa tulivu; wameziachilia huru roho zao kwa faraja. Huwezi kuzilinganisha nyuso zao na za wanaokufa kwa hamaniko wakizingirwa na jamaa ambao hawana hata hela za kununulia sindano ya kuingizia

dawa mwilini! Kuna wale ambao hufia kwenye vitanda vya mwakisu vitongojini baada ya kupiga maji haramu. Hawa husemekana kuwa wamekuwa nzi ambao kufia dondani si hasara. Hulaumiwa kwa kujitosa katika msiba wa kujitakia. Tofauti hizi zote unazijua. Unajua pia kuwa kuna tofauti hata katika mitindo ya mazishi, viviga vinavyohusishwa na sherehe za mazishi na hata mavazi ya "mwenda zake" na wafiwa. Hata majeneza yenyewe huhitilafiana! Hayo si ya kuambiwa, umeyaona. Usawa ulio kati ya maiti ni kwamba wote huhojiwa na munkari. Hata hivyo hapa katika maskani yetu tuna nafuu. Mipaka ya kitabaka imebanwa. Kwa kweli haipo kwani hata sasa nisemapo nang'ang'ania chakula—uji haswa—na aliyekuwa Waziri wa Fedha miaka mitano iliyopita. Hilo usilione dogo kwani unajua kuwa wenzetu hawa katika hali ya kawaida ni watu wenye shughuli na hali zao. Ila sasa inabidi waniite ndugu; hasa Ndugu Kaizari.

Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshukuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siyeee. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama

tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa—mwamu hasa—akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizi-mwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini! Wanasema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la mama, hili la mbwa ataliamwa!

"Kumbe hata wewe shemeji Kaizari upo?" Ridhaa ananiuliza kwa unyonge. Hili linanizindua kutoka lepe langu la muda, linanitonesha kidonda si haba.

"Ndio, tu hapa na wengine wengi," ninamjibu, kisha ninaanza kumsimulia yaliyojiri kana kwamba ni mgeni wa hali hii, "siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu hakustahili kuiongoza jamii ya Wahafidhina, kisa na maana, alikuwa mwanamke, mbingu zilishuka. Watu walishika silaha kupigania uhuru wao; uhuru ambao walidai hawakupewa, waliupigania.

"Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike—yule anayesimuliwa katika visakale vya majirani zetu. Kumbuka jinsi katika enzi hiyo ya kiistiimari wanaume walivyotumikishwa! Si sisi tuliokuwa tukitifua udongo mashambani huku wanawake kama majeta wanakaa na kututumikisha? Sasa wanataka kuturudisha pale pale. Kwa miongo mitatu sasa, hawa watu wamekuwa wakitusumbua na *Affirmative Action,* na *A third should be women.* Hakuna tuliloweza kulipitisha hata katika vikao vya kitawala bila kusikia kidudu mtu akisema, 'Fikiria

suala la jinsia.' Na usidhani ni jinsia nyingine, ni dada zetu tu. Vyombo vya habari na vikao vya wapigania haki vinapigania elimu ya mtoto wa kike, haja ya kuwainua akina mama kiuchumi, hukumu ya kifo kupitishwa dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake ... Inashangaza mno, hata haki ya mtu kuhusiana kimapenzi na mkewe imebatilishwa na siasa hii ya usawa wa kijinsia! Almuradi anga nzima imehanikiza vilio vya kumkinga mwanamke. Lakini ni wangapi wanaokumbuka kuwa hata maghulamu wanalawitiwa? Ni wangapi wanaowatetea mamia ya wanaume ambao wanateseka katika ndoa kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia kutoka kwa wake zao? Je, ni nani asiyeshuhudia majeraha ya kudhalilisha wanayopagazwa wanaume mashavuni, na hasa mioyoni; kisa na maana, wamekula jasho lao na kudaiwa kutelekeza majukumu yao ya unyumba? Tumeendelea kuwakweza akina dada huku tukididimiza nguzo ya jamii yetu. Na kuwe huko kumtoa mekoni, lakini hili la kumpa jukumu la kuiongoza jamii nzima! Itakuwa kukivika kichwa cha kuku kilemba," alisikika Teitei, mwanaharakati mmoja, akisema.

"Lakini ndugu, si mambo ya *affirmative action* tu. Mwekevu alijitosa kwenye ugwe kama wanaume walivyojitosa, na akaomba kura kama walivyofanya hao wapinzani wake. Alistahimili vitisho na matusi kutoka kwa wanaume, akahiari kutengwa hata na jamii ya wanawake kwa kupanda kwenye ulingo wa wanaume. Ushindi wake ni zao la bidii na kujisabilia kwake kuwainua raia alipokuwa mkurugenzi wa Shirika la Chemchemi. Nashangazwa sana na jinsi binadamu walivyo wepesi wa kusahau! Je, ule mradi wake wa kuchimba visima haujawafaidi raia kwenye maeneo kame?" alikuli Bi. Shali.

Basi mwamu wangu Ridhaa, muda kabla ya kusikia mlio wa bunduki, mitutu yake ilitema risasi jinsi bafe atemavyo mate. Vilio vya kite vilihanikiza hewani, vita vikaanza kati ya kundi lililounga mkono uongozi wa Mwekevu na lile lililomuunga mkono mpinzani wake mwanamume. Mafahali wakaendelea kupigana, mafahali ambao awali waliishi katika zizi moja, wakishiriki kazi pamoja, wakishiriki pamoja vunoni, sasa wakawa hawapikiki katika chungu kimoja! Mara, "Tangu lini mwanamke akashinda katika uchaguzi? Kama Mamataifa hakuyashinda majabali miaka kumi na mitano iliyopita itakuwa huyu mwanagenzi ambaye hata kushika mgwisho sisi ndio tulimfunza? Lazima ameiba kura! Lazima wafuasi wake waliwanunua akina mama ambao ndio wapiga kura wengi."

Wengine walisikika wakisema, "Wakati wa mabadiliko umefika. Wimbi la mabadiliko limeivamia jamii yetu. Hatuna budi kukubali. Wakati si mwamba, ikiwa hata miamba hugeuka kuwa mchanga baada ya muda, sembuse wakati ambao u mikononi mwa mwanadamu? Binadamu lazima ayakumbatie mabadiliko katika maisha. Tunahitaji kumpa nafasi Mwekevu. Huenda hata akatukwamulia uchumi ambao unachechemea. Wana nguvu hawa wake na mabinti zetu. Wana ari kubwa! Washikapo jambo huwa kama duduvule, hawaachi hadi wanapoona hatima. Ni muhimu tuwape nafasi pia."

Mijadala hii ilizua na kukuza migogoro isiyomithilika. Hali ya taharuki ilitamalaki, vyombo vya dola vikatumwa kudumisha usalama katika vijiji, mitaa ikajaa sisimizi walioshika bunduki. Hali hii ilileta chachawizo zaidi katika vijiji na mitaa. Binadamu ana hulka ya kushangaza!

Hapendi kudhibitiwa. Kule kuwapo kwa walinda usalama kulimshinikiza binadamu kuhalifu sheria, makundi yote mawili yakashuku kuwa walinda usalama wametumwa kuja kuwamaliza na kuwang'oa uongozini viongozi wao. Viongozi wenyewe baada ya kupiga kura, walijikalia makwao, na kuendelea kuwatazama masahaba wao kwenye runinga wakiendelea kuzozana! Mchezo wa polisi kukimbizana na raia ulianza. Katika mchezo huo mamia ya roho zisizo na hatia zilisalimu amri chini ya pambaja za risasi na mapigo ya rungu, vitoa machozi navyo vikafanya kazi barabara. Kuna wale ambao waliona ku moto, wakaamua kuacha makazi yao na kukimbia. Nyuma walikoacha kuliwaka moto, wakapoteza kila kitu, si maisha, si mifugo, si aila ... Wengine waliokuwa jasiri walidiriki kuingia kwenye maduka ya wafanyabiashara wa Kihindi, Kiarabu na hata Waafrika wenzao, wakapora walichoweza kubeba kabla ya kukutana na mkono mrefu wa utawala.

Nchi ya Wahafidhina ilitwaa sura mpya. Misafara kwa misafara ya watu waliohama kwao bila kujua waendako ilizipamba barabara na vichochoro vya Wahafidhina. Mizoga ya watu na wanyama, magofu ya majumba yaliyoteketezwa kwa moto, na viunzi vya mimea iliyonyong'onyezwa na moto ilijikita kila mahali; uharibifu wa mali na mazingira ukashamiri.

Nakumbuka asubuhi ya pili baada ya mtafaruku kuanza. Nilikuwa sebuleni na wanangu tukitazama runinga. Mara nikasikia,

"Hakuna amani bila kuheshimu mwanamume. Hatuwezi kukubali haya. Hata mizimu itatucheka!"

Kilichofuata maneno haya kilisikitisha. Niliwaona mabarobaro wamebeba mabango yaliyochorwa picha za mpinzani wa kiume ambaye alishindwa na Mwekevu. Wote walikuwa wakighani, mkarara huu: *Tawala Wahafidhina tawala, Mwanzi wetu tawala Wahafidhina tawala.*

Mara hali ilibadilika, nikaona wote wameyazingira magari barabarani na kuanza kuyawasha moto kana kwamba wanayachoma mabiwi ya taka! Baadaye kulisikika vilio vya imani, binadamu akiomba kuhurumiwa na binadamu kaini, vilio ambavyo viliangukia masikio yaliyotiwa nta. Magari yaliwaka moto bila kujali kilichomo ndani. Moshi ulipaa mbinguni katika mstari mmoja kama kwamba unakwenda kumshtakia Mungu.

Katika vurumai hii mlisikika kelele kutoka kwa mmoja kati ya wale waliokuwa wakitekeleza tendo hilo:

"Nyamaza wewe! Nyinyi ndio mlioturudisha nyuma miaka yote hii. Mnatuhadaa kwa vishahada mnavyotupa vyuoni, vishahada ambavyo ni laana kwetu, tanuri hasa linalouchoma uwepo wetu. Mnatufunza kukariri nadharia bila kuwazia umuhimu wa kutupa umilisi na stadi za kutuwezesha kujitegemea na kuyadhibiti maisha yetu ya baadaye. Mtu anahitimu hata digrii tatu, kisha anapiga lami kwa miaka kumi bila kuwaza kuwa anaweza hata kujiajiri. Hebu niambie, mtu ataweza vipi kujiajiri na hata njuga zenyewe za ujasiriamali hajafungiwa chuoni? Isitoshe, hata wanaoweza kupapatisha huo ujasiriamali watatoa wapi mtaji wa kuanzishia biashara? Wapo viongozi wanaopita wakipayuka, 'Vijana turudini mashambani. Maeneo-gatuzi yenu yanahitaji mabarobaro kama nyinyi kulisukuma gurudumu la maendeleo.' Hapa

ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu kwa maelfu ya ekari wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwamakubwa huku wakidai kuwa ni njia ya kuwahakikishia wenyeji hali ya kujitosheleza kwa chakula. Kumbe wanakuja kutufukarisha zaidi! Tunapolalamikia kashfa za unyakazi wa hata vikataa vidogo tulivyo navyo tunapozwa roho kwa, 'Tumeunda tume ya kuchunguza kashfa hii. Waliogawiwa au kununua mali ya umma kwa njia za udanganyifu watakabiliana na mkono thabiti wa sheria.' Ni wazi kwamba mwananchi wa kawaida hadiriki kuziona ripoti za tume hizi au tuseme ripoti hizi huwa wageni wa rafu za makavazi ya kitaifa!

"Na kila baada ya miaka mitano unaambiwa, 'Vijana wenzangu, hii ni awamu nyingine ya kipindi cha utandawazi au utanda na ardhi kama wasemao wataalamu. Tusisikilize mambo ya wale wanaoabudu mitazamo ya kijadi ambayo haifaidi. Vijana wenzetu, ni vyema kumpigia kura kiongozi anayejali mustakabali wa maisha yenu, kiongozi atakayesaidia kuangamiza tatizo sugu la uhaba wa nafasi za kazi.' Tunasombwa kama taka kwenda kuwafanyia kampeni. Tunawanasihi akina mama kuwapigia kura viongozi ambao hata wanatiririkwa na machozi wanapoona ngozi zetu zilivyopauka na kujaa makunyanzi kwa ulitima. Kumbe machozi yenyewe ni ya mamba! Uhitaji wetu unatusukuma kununuliwa kwa vihela vya kushikilia uhai. Tunawapigia kura. Wakati mwingine tunashiriki katika njama zao chafu za kifisadi, tunawasaidia vikongwe wasiojua kusoma na kuandika kumchagua kiongozi afaaye!

"'Mama, unataka KIBOKO, au PAPA?" tunamuuliza ajuza mmoja kijijini.

"'Mimi simtaki huyo Kiboko, namtaka Papa. Kiboko hata chumvi hatoi. Afadhali Papa, amepita hapa mara tatu akatugawia kila mtu shilingi mia mia na vibaba viwili viwili vya unga,' Mama anajibu.

"'Basi tia alama **X** kwenye picha ya Kiboko kuonyesha humtaki kabisa,' anaambiwa kisha kusaidiwa kutia alama hiyo bila kujua kuwa kamchagua huyo huyo Kiboko! Sasa miaka kumi hii, tungali tunabisha hodi kwenye afisi za mabwana wakubwa, si ndugu sasa. Wengine tulikuwa tumeahidiwa makubwa wakati wa vuguvugu la kuwania nafasi za uongozi. Mara, 'Ubalozi wa *Emirates* unahitaji kijana aliyesomea shahada ya uzamifu katika Mahusiano ya Kimataifa kama wewe. Utakuwa wa kwanza kufikiriwa kwa nafasi hii chama chetu kitakapochukua usukani.' Na, 'Wewe tutakuteua kama *Education attaché* huko Uingereza. Nashangaa ni vipi mtu aliye na shahada ya uzamifu katika masuala ya Elimu na Mitaala hajaweza kuwaziwa nafasi kama hizi zinapotokea!' Mara, 'Wewe tutakuteua kama Waziri wa Maslahi ya Kijamii katika jimbo ...'

"Haya yote husahaulika mara tu baada ya uchaguzi na kuvyazwa kwa serikali mpya. Tunaambiwa nchi haina uwezo wa kuzalisha mali. Tunahadaiwa kwa Hazina ya Uwezo ambayo inatarajiwa kuwapa vijana mtaji wa kuanzishia biashara. Hazina yenyewe imeandamwa na madonda ndugu ya ukabila na unasaba. Matarajio yetu kufaidika kutokana na hazina hii yanaenda tenge. Tunaambiwa turudi mashambani tukalime, mashamba yenyewe ni ya wawa hawa waheshimiwa!

Mate yametukauka vinywani tukifunga bahasha za kutumia maombi ya kazi. Aah! Kufa mwana kufa," akasema kwa ghadhabu na kurusha bomu lingine la petroli kwenye gari lililokuwa likipinda kuepuka fujo hiyo, na kujiendea kana kwamba alikuwa amevinyunyizia viwavi dawa.

Baadaye ving'ora vilisikika kwa mbali. Yale malori ya kawaida yanayobeba askari almaarufu katika janibu hizi, 'Fanya Fujo Uone', yakaonekana yakielekeza mianzi ya pua karibu na walipokuwa vijana hawa, vitoza machozi vikahanikiza hewa ya asubuhi, polisi wakawa wanawawinga mabarobaro hawa kama kengewa wala vifaranga au ndege wala nafaka. Hata hivyo, mabarobaro hawa walioonekana kuwa na kisasi na maisha walikita ardhini kama mikuki iliyochomelewa hapo.

"Hatung'atuki," walisema huku wameinua mikono yao juu. Baada ya muda mfupi vifua vyao vilikabiliana na risasi zilizorashiwa vifua hivyo kama marashi, vifua vikawa havina uwezo dhidi ya shaba, vijana wakaanguka mmoja baada ya mwingine, wamekufa kifo cha kishujaa, wamejitolea mhanga kupigania 'Uhuru wa Tatu', kama walivyouita. Machozi yalinitiririka njia nnenne. Niliwahurumia vijana hawa wakembe ambao walikufa kifo walichoweza kukiepuka. Niliihurumia nchi yangu ambayo ilielekea kushindwa kuwahakikishia usalama watu wake.

Wakati tukitazama ubahaimu huu wa Firauni, hatukujua kuwa tulikuwa kuni kwenye uchaga, chuma chetu kilikuwa motoni. Miujiza ya Musa ilikuwa njiani. Siku ya nne baada ya 'mapinduzi' tulisikia hodi mlangoni. Mke wangu Subira ndiye aliyekwenda kufungua. Alisalimiwa kwa kofi kubwa, kisha,

"Wapi kile kidume chako kijoga? Nasikia ni mmoja wa wale waliotuuza, wakampigia kura Mwekevu. Ati, '*As for me and my family we will support our mother.*' Nyinyi ndio vikaragosi wanaotumiwa na wasaliti wa nia zetu kuendelea kutudidimiza kwenye lindi hili la ukata.

Kabla hajajibu lolote alikuwa amekula mikato miwili ya sime, akazirai kwa uchungu. Kisha genge hili la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti wangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa. Nilijaribu kwa jino na ukucha kuwaokoa lakini likawa suala la mume nguvuze! Mahasimu hawa walitekeleza unyama wao na kuniacha bila kunigusa, niuguze majeraha ya moyo.

Hakuna msiba usiokuwa na mwenzake. Nilijizoazoa kujaribu kuwapa wanangu na mke wangu huduma ya kwanza. Hata hivyo, hizi zilikuwa juhudi za mfa maji kwani kabla ya hata kuku kumeza punje ya nafaka, nilisikia sauti ya jirani yangu Tulia.

"Tokeni! Tokeni kama bado mnataka kuishi!"

Sijui ilikuwaje, lakini baada ya dakika chache nilijipata nje ya nyumba yangu, wanangu wawili wamezirai ubavuni mwangu, mke wangu anatoka damu; mchirizi baada ya mwingine. Nilimtazama jirani yangu aliyekuwa amekuja kutuokoa. Kinyume na wale wengine, yeye alinihimiza kusahau tofauti zetu za awali. Alinisaidia kufunganya, akanisindikiza hadi njia panda. Hapo alinikumbatia na kusema,

"Ndugu yangu, Mwenyezi Mungu ndiye hupanga. Nguvu na mamlaka pia hutoka kwa Mungu. Uongozi mpya umezua uhasama kati ya koo ambazo zimeishi kwa amani kwa karibu

karne moja. Inabidi uihamishe aila yako kwa muda kwa sababu ya usalama. Nina imani kuwa huu si mwisho wa kuonana. Huu ni mwanzo wa uzao wa jamii mpya isiyojua mipaka ya kitabaka, jinsia na kikabila. Hali hii ni kama maji ya mto tu ambayo yakipita mahali yamepita, hayarejei. Hali itakuwa shwari, inshallah! Tutalilinda boma lako. Nenda kabla mahasidi wako hawajakupata."

Hapo nilimpungia mkono wa buriani jirani yangu wa miaka mingi, nikapiga moyo konde kukabiliana na hali hii mpya.

Matwana ya abiria ilisimama kando yangu na aila yangu. Utingo aliponiuliza tulikokuwa twaelekea, nilisita kwa kuwa sikujua nilikokuwa nikielekea. Kwa sauti kali iliyojaa chuki aliniambia,

"Mzee, ingia haraka! Huoni huku hutakiwi? Tazama hali ya mkeo na wanao?"

Baada ya kuabiri, matwana ilikaza mwendo kana kwamba ilikuwa inakimbizwa. Dereva hakuiona milima, miteremko wala kuruba. Alilotaka ni kutokomea kokote kule, mbali na zahama iliyokuwa imelifunika eneo zima la Wahafidhina. Ilikuwa safari ndefu yenye shaka na shauku. Mara tunasimamishwa na polisi na kupekuliwa, mara tunayatazama mabasi mazima yakichomwa pamoja na shehena zayo, mara mifyatuko ya risasi ... almuradi kila sekunde ilikuwa na tanzia yake. Sijui tulikuwa tumekwenda kwa siku ngapi, ila ninalokumbuka ni kwamba baada ya muda, gari lilikwisha petroli, dereva akaachama.

"Sasa ni wakati wa kila mtu na malaika wake," dereva akatuambia, "wanaokumbuka angaa Sala ya Bwana wajaribu

kuomba, wanaoweza kupiga Fatiha na wafanye hivyo. Huenda wakadiriki kumtanabahisha Muumba kuhusu udhalimu wa viumbe aliowapa wadhifa wa kumtunzia wana wake!"

Tulijitoma msituni, kila mtu na aila yake. Usiku wa kwanza tulikula mate kutokana na ule ugeni wa kutojua hata kuliko na matunda mwitu. Asubuhi idadi yetu iliongezeka. Inaonekana hapa ndipo magari yote yalipoishia petroli! Hali ya uhitaji ilitutuma kutafuta jinsi ya kujikinga na baridi na umande wa asubuhi, tukakata miti, tukajenga vijumba ambavyo viliezekwa kwa nyasi na kuta zake kukandikwa kwa udongo. Tulibahatika kupata kwamba katika msitu huu ndipo palipopitia Mto wa Mamba. Haikuwa vigumu kupata maji. Changamoto kubwa ilikuwa maji safi ya kunywa. Hata hivyo, hali ambayo ilitukabili haikuturuhusu kuamua kula nazi au koroma. Tulikuwa wasafiri, na ikiwa tangu hapo msafiri wa kikaida huwa kafiri, sembuse sisi ambao tulisafiri bila hiari! Kiu ilipobisha hodi tulijaribu kujikuna tulipojipata, tukanywa maji ambayo tulidiriki kupata tukisema, heri nusu shari. Matokeo ya tendo hili yalikuwa homa ya matumbo ambayo iliwapukutisha baadhi yetu.

Kadiri idadi ya wakimbizi ilivyozidi kuongezeka ndivyo hali ya maisha ilivyotuwia ngumu. Ikumbukwe kwamba wengi wetu tulitoka bila hiari, hivyo hatukuwa tumeitarajia hali hii ngumu. Vijumba vichache tulivyovijenga havikutosha kuhimili idadi ya watu walioongezeka kila mawio. Huduma za kijamii ziliadimika. Ukosefu wa misala ulipelekea kuzaliwa kwa vyoo vya kupeperushwa, usiniulize ni vipi hivi kwani hata mimi nilikuja kuambiwa na bwana mmoja kwa jina Makiwa.

"Ni sandarusi ambazo hutumiwa kama misala bwana. Ndivyo tunavyoishi katika mtaa wa mabanda wa Sombera. Na usidhani ni kuishi huku mnakoishi wewe na huyu mwamu wako, Bwana Wakfu wa Matibabu, ni kupapatika, kufufurishwa na tumbawe za maisha hasa. Sandarusi zenyewe mtu anazitafuta kwenye milima ya taka zinazotolewa huko waishio waheshimiwa kuja kutupwa huku. Utashangaa mtu anavyokhitari kukita jalala katikati mwa msongamano wa vibanda vilivyolaliana na kutazamana kwa jitimai! Hata hivyo, sisi tumeyazoea haya, tumezoea pia kuzitazama roho za vitoto vyetu zikibwakurwa na magarimoshi; vitoto vinapojaribu kujijengea misala katikati mwa reli. Tumezoea kuumbuliwa kwa kuambiwa kwamba tunajengewa nyumba za hadhi kwa gharama nafuu, kutahamaki nyumba zenyewe zimechukuliwa na haohao wanaotoa ahadi. Pole ndugu, itabidi usahau mswala kwa hii mbacha uliyo nayo. Ni muhimu kutumia hiki duni ulicho nacho sasa usije ukapokonywa! Huku ni Roma na unapoenda Roma ..." Jamaa aliniachia kujijazia.

Siku za mwanzomwanzo sikuweza kuitumia misala hii. Nilijaribu kuyarai maumbile yanihurumie lakini maumbile yaliendelea kunidhihaki, hadi nikasema potelea mbali, lisilo budi hutendwa. Nilijizoazoa, nikaitumia misala iliyotumiwa na wenzangu! Nilipoona ku mno na ugonjwa wa kipindupindu umeanza kuenea, niliwasihi wenzangu kuchimba misala, maarufu kwa jina *long drop* siku hizo, Ndugu Waziri Mstaafu akawa katika mstari wa mbele kwa hili. Kumbe hata yeye aliona aibu kuchutama kwenye nyasi huku mijusi wanamkodolea macho!

Unaweza kusema kwamba tatizo la misala lilitatuliwa. Lakini kumbuka mtu huenda msalani baada ya shibe! Tumbo shinda hata haja ndogo haliendi! Ugenini humo hamkuwa na mashamba. Waliokuwa wamebahatika kubeba nafaka haba walizitoa zikatumiwa kwa ujima. Sasa matumbo yalianza kudai haki hata baada ya kujua kuwa haki yenyewe haikuwa mikononi mwetu; haki iliyokuwa mikononi mwa walio na nguvu, ambao ndio waliotufanya kuwa wageni wa pori. Vilio vya watoto wenye njaa vilianza kusikika. Polepole vilio hivi vilianza kupungua; njaa na ugonjwa vimefanya kazi! Wasiwasi ulianza kutuingia. Nilianza kufikiria kuwa hali ikiendelea hivi tutaipungia dunia mkono. Nilihisi kwamba ingekuwa bora kama tungefia katika mazingira tuliyoyazoea; huenda hata tungepata wa kutuomboleza, kuliko kufia ugenini.

"Sasa umeanza kufikiria kama wafuasi wa Nabii Musa ambao baada ya kukosa chakula huko jangwani walimshutumu kwa kuwatoa kule Misri. Walidai kuwa huko Misri wangekuwa wakila matikitimaji yao pamoja na kuwa watumwa! Ndugu Kaizari utahiari vipi kufa?" moyo wangu ulinisuta.

Asubuhi hii ya siku ya kumi na tano tangu kuwasili hapa, Selume alipitia kibandani mwetu kujua hali ya mke na watoto wangu. Selume alikuwa mke wa jirani yetu aliyekuwa mpinzani mkubwa wa Mwekevu. Yeye sasa ameondoka kwake kwa sababu ya kuhitilafiana kimsimamo na wakwe zake. Wakweze walidai kuwa yeye alimuunga mkono Mwekevu, kwamba yeye alikuwa baka ambalo lilitishia kuuletea ukoo wao fedheha. Selume alishindwa kuvumilia shutuma hizi, akafunga virago vyake na kutokomea kokote kule. Sasa Selume anajua maana

ya udugu. Anahiari hali hii duni badala ya kuishi kwenye kasri la dhuluma la mumewe. Ilibidi Selume atangaze kufika kwake kwa mbali kwani kibanda chenyewe kidogo, hutarajii faragha, ndicho sebule, chumba cha malazi …

Selume alitueleza kuwa alikuwa amesikia fununu kuwa upo mradi wa kuwakwamua wakimbizi kutokana na hali hii. Shirika la Makazi Bora lilikuwa limejitolea kuja kuwajengea wakimbizi nyumba bora. Misikiti na makanisa nayo yalikuwa yamekusanya magunia ya vyakula kuwalisha wahasiriwa wa hali hii ya tandabelua. Maneno ya Selume yaliwasha mwenge wa tumaini. Hata mke wangu sasa alionekana kupata ahueni kidogo. Sote tulikaa tukitunga macho barabarani, tukisubiri jinsi waumini wanavyoambiwa wakeshe wakisubiri kuja tena kwa Masiya. Tulingoja, tukangoja, moyoni nikiwa na imani ambayo baba alinijaza kuwa anayesubiri hafi … Hatimaye siku ya ishirini lori kubwa lililoandikwa *Nilikuwa na Njaa Ukanilisha* lilibisha hodi kwenye vibanda vyetu. Sote tulitoka nje kulikimbilia jinsi watoto huwakimbilia mama zao baada ya kuwasili kutoka sokoni siku ya chete. Watoto waliokuwa wakicheza nje wakiwa uchi walikimbia nyuma ya vibanda kujificha wasije wakaonekana uchi na lori hili!

Bwana mmoja aliyekuwa kavaa gwanda refu—haikosi alikuwa kiongozi wa kidini—alitoka na kutusalimu:

"Peace be with you," akasema kwa lafudhi ya Kizungu, japo ni Mwafrika kisha mwenyewe akatafsiri na kusema, "Amani iwe nanyi."

"Iwe pia nawe," waliojua walijibu, huku wengine tukikaa kimya. Hata hivyo maneno yake yalitupa matumaini. Uso wa kila mmoja wetu ulitwaa mng'ao na utulivu ambao sikuwa

nimeuona kwa siku zote tulizokuwa mle. Nilikumbuka kifungu kimoja katika sala za waumini (wakati nilipokuwa nikihudhuria ibada) kilichosema, *"Ninawapa amani, amani yangu nawaachia."* Nilianza kujiuliza ikiwa kweli Wahafidhina waliwahi kuikumbatia amani hii tuliyoachiwa. Na kama tuliachiwa, je, mbona twaiacha kupeperukia nyikani? Kwa nini tusiwaige watoto hawa wanaocheza pamoja bila kujali tofauti zao za kitabaka au kikabila?

Kazi ya kugawa chakula ilianza. Akina mama ambao walikuwa wamepakiwa nyuma ya lori hilo walichukua mikebe, wakaanza kuipa kila familia vibaba kumi vya mahindi na vitano vya maharage.

"Tafadhali pigeni foleni hapa," alisema mama mmoja mwenye mwili uliojazana, ambaye alikuwa amejitanda kanga yenye maandishi: *Mothers' Union.* Huyu pengine ndiye aliyekuwa kiongozi wao. Wengine waliojifunga vitambaa vilivyoandikwa *CWA,* wengine, *Woman's Guild,* na wengine waliovaa hijabu waliingia kazini. Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa watu wenye njaa na tamaa kupiga foleni. Msukumano ulianza hadi pale bwana mmoja aliyevaa mavazi rasmi ya walinda usalama alipojitokeza na kutusihi kuwa watulivu. Tulianza kunung'unika. Wengine tulikumbuka jinsi waungwana hawa walivyotuacha kuhasiriwa na waungwana wenzao huko nyumbani.

"Sasa ana haki gani ya kutuomba kudumisha utulivu baada ya kuivuruga yeye na wenzake? Alikuwa wapi siku kiduka changu ambacho mimi na aila yangu tumekitegemea kwa miaka kumi kilipoporwa na kugeuzwa majivu? Si wao waliotutazama kama wehu wakati tulipokuwa tukililia

usaidizi, angaa kuopoa magodoro ya kuwalaza maskini watoto wetu? Sasa hivi ndio anaona thamani ya utulivu?" Alisema Mzee Kaumu kwa mhemko mkubwa. Waliokuwa nyuma walianza kurusha makombora ya matusi. Askari aliinamisha kichwa na kurudi nyuma, nayo hasira ya umati uliokuwa tayari kumpatiliza mja huyu ikapoa.

Tabia ni ngozi ya mwili. Bwana Waziri Mstaafu ambaye tangu hapo alikuwa amezoea kuwaelekeza watu huko wizarani alijitolea kusaidia kukigawa chakula, donda ambalo lilikuwa limeanza kututa kwa usaha likatulia. Mimi na Selume pia tuliitwa kusaidia. Magunia ya mahindi na maharage, bandali za unga na madebe ya mafuta ya kukaangia yaligawiwa kila familia kwa vipimo sawa. Hata hivyo, huwezi kusema tulipata mafungu sawa. Kuna familia, kama vile ya aliyekuwa diwani wetu hapo awali, Bwana Kute, zilizofanya ujanja ili kupata mafungu zaidi. Familia moja ilijigawa, ikazaa familia nyingine mbili, zikawa familia tatu tofauti! Hatimaye Kute na aila yake waliishia kupata mara tatu ya posho ambayo wengine tulipata! Nani alikwambia kwamba hata chakula cha msaada, hata kilichotolewa kwenye madhabahu ya kidini, hakiwezi kufisidiwa!

Sura ya Tatu

Ni asubuhi. Ridhaa ameketi kwenye chumba cha mapokezi katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Rubia. Macho yake, ambayo tangu hapo yamechoka kutarajia, ameyatunga kwenye dari ya chumba hiki. Anagota sakafu kwa viatu vyake kana kwamba anataka kupata habari fulani kutoka kwayo. Anayemtazama anajua kuwa huyu ni mja mwenye jakamoyo kuu. Hamu yake kuu ni kumwona mwanawe Mwangeka akiwa mzima. Baada ya kuishi katika Msitu wa Mamba kwa miezi sita, Ridhaa, Kaizari na familia yake walibahatika kurudi nyumbani kufuatia mradi ulioitwa na wanaharakati wa kupigania haki za kibinadamu: *Operesheni Rudi Kanaani.*

Asubuhi hiyo ya kuhawilishwa kutoka Msitu wa Mamba, Ridhaa alihisi kama anayetoka Kanaani kwenda Misri. Hakuwa na matumaini ya maisha bora, hasa alipokumbuka kuwa hakuwa na mwenzi wala mtoto wa kuendea. Siku walipoambiwa kuwa watarudishwa kwao ilikuwa siku ya hisia mseto kwa wengi. Hata sasa Ridhaa anapopiga darubini nyuma, anakumbuka Selume alipokuja kwake, macho yamemwiva kwa kilio. Analia kwa sababu hajui ataenda wapi. Mume wake, inasemekana na wambea, amekwisha kuoa msichana wa kikwao. Mwanawe Sara ... Huyo hajui kama watawahi kukutana tena ... Baba mtu alimkatalia katakata!

"Usilie mwenzangu," alisema Ridhaa, "wewe una bahati. Angaa unajua kuwa mwanao yu hai, chini ya hifadhi ya babake. Hawezi kumdhuru. Simba hata akawa mkali vipi ni muhali kumrarua mwanawe. Na wewe Mungu kakupa siha na uzima, unaweza ukajitegemea, una kisomo. Hapo ulipo umehitimu kama mkunga japo hujawahi kuifanya kazi yenyewe. Siku za kuwa 'Mke Nyumbani' zimekwisha. Tukifanikiwa kufika nyumbani salama, nitakutambulisha kwa mkuu wa Idara ya Afya ya Jamii katika Hopitali Kuu ya Tumaini. Ataweza kukuelekeza. Huenda hata akakupa kazi." Hata Ridhaa anapowaza haya, Selume amekwisha kuajiriwa kama muuguzi katika hopitali ndogo iliyojengwa karibu na Kambi ya WWHN.

Ridhaa anakumbuka jinsi kadhia iliyompoka familia yake ilivyomkutanisha na watu kama huyu Selume ambao kwa kweli angewaita ndugu. Katika Msitu wa Mamba alikuwa amesaidiwa kukabiliana na msiba wa kuipoteza akraba yake. Udugu na utangamano na wakimbizi wenzake uliyahuisha maisha yake, ukayajenga upya, ukamfunza zaidi kuhusu thamani ya binadamu. Hakuwa tena yule Ridhaa aliyeishi kwenye kasri, anaendeleza shughuli za kimatibabu bila kuwa na mwao na adha hasa zilizowatafuna binadamu wengi katika jamii pana ya Wahafidhina. Si kwamba Ridhaa alikuwa mkono wa birika. La, Ridhaa aliwasaidia watu aliotagusana nao kwa karibu. Hata hivyo, lililoendelea hasa nje ya mipaka ya ujirani wake halikumshughulisha mno. Masuala yaliyomshughulisha zaidi ni yale yaliyohusu afya ya kijamii, hususan yale yaliyolenga wakfu aliouongoza. Sasa anajua kuwa kuna kupata na kukosa. Anajua kuwa uzima ni upande mwingine wa mauti.

Kwenye Msitu wa Mamba, Ridhaa aliweza kupata huduma za ushauri na uelekezaji kutoka kwa wataalamu mbalimbali. Aliweza kuudhibiti ugonjwa wa shinikizo la damu ambao ulitokana na mshtuko wa kupoteza jamaa na mali yake dafrao moja. Awali akijihisi kama yule Ayubu kwenye kitabu kitakatifu ambaye ibilisi aliifakamia familia na mali yake takriban kutwa moja! Hata alipotoka kwenye msitu, alijiona kuwa na nafuu, alijihisi kiumbe kipya. Wapwa zake—Mwanaheri na Lime—walikuwa wamepata matibabu. Walikuwa wamehudumiwa na vijana wenzao ambao walitumwa na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa huduma za ushauri na uelekezaji katika maeneo mbalimbali ili kupunguza makali ya athari za tandabelua za baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya. Dada yake—Subira—alitibiwa akapona. Mwamu wake, Kaizari, amepona donda lililosababishwa na kuwatazama mabinti zake wakitendewa ukaini na vijana wenzao. Lililobaki kwa Kaizari ni kovu ambalo bila shaka ataliuguza daima. Ridhaa anajua kuwa Kaizari ni afadhali kwa sababu hakuna aliyemtenga na mmoja kati ya jamaa zake. Hata Ridhaa anapomfikiria Kaizari anajiambia, "Heri nusu shari kuliko shari kamili."

Hata alipoketi akimngojea Mwangeka, Ridhaa hakuweza kusahau jinsi alivyosikia aliporudi tena kwenye ganjo lake siku ile. Hisia za manyenzi zilimpakata kukutu, mwili mzima ukamsisimka, uchungu mkali ukampanda kwenye uti wa mgongo, malaika yakamsimama, majasho yakammwagika katika baridi ile ya kipupwe, akanyong'onyea na hatimaye kuzirai. Alipozinduka alijipata palepale katikati mwa kiunzi cha sebule ya lililokuwa kasri lake. Hapo ndipo wanawe Tila na Mwangeka walipokuwa wadogo walizoea kumkimbilia kila mara alipotoka kwenye shughuli zake za kikazi. Hapo ndipo

kijukuu chake kilipozoea kutembea tata na kumwita 'Bubu' naye kila mara akikirekebisha, "Sema Babuuu." Kijukuu kingemtazama kwa utukutu wa kitoto na kusema, "Bubuuuu." Hapo Ridhaa angecheka hadi machozi yakamtoka. Sasa haya yote hayapo. Hazipo na zile pambaja za mkewe Terry, haupo ule utani wa mkewe:

"Umesahau kuwa umekuwa babu? Chepeo utaacha lini kuvaa? Haya imekuandama tangu siku ukimtongoza Fulani; siku za kuchora ramani ya Afrika kwa vyanda vya miguu, hadi sasa? Ama ni hizo mvi unaficha? Nasikia ile *mid-life crisis* ikiwashika wazee ndio hivyo."

Ridhaa alikuwa amejifunza kupuuza utani wa mkewe kwa kusema, "Sema unavutiwa tu. Chepeo hii ndiyo iliyokupa usingizi wa mang'amung'amu siku hizo, sasa waiona udhia. Ama ni mambo ya kisebusebu na kiroho ki papo?"

Hapo Terry angehizika na kuinamisha kichwa; Ridhaa angekuwa ameshinda.

Uyabisi aliouhisi wakati alipokuwa akifikiria haya sebuleni pake siku ile hausemeki. Alilitazama gofu hili kana kwamba analitazama miezi sita iliyopita. Uyabisi huu ndio unaomkumbatia sasa, hata anapojua fika kuwa anamngojea mmoja wa wanawe. Polepole kwenye jukwaa la akili yake kunaanza kuigizwa mchezo wa maisha yake kabla ya kufikwa na yaliyomfika. Anamwona mwanawe, Tila, akitoka shuleni na kuuweka mkoba wake juu ya meza. Anajua kwamba Tila ana jambo.

Tila: Shikamoo baba!

Ridhaa: Marahaba mwanangu. Umeshindaje?

Tila: *(kwa uchangamfu)* Vyema. Baba, leo somo letu la fasihi lilivutia mno.

Ridhaa: Kwani waliwafunza nini huko? Ama ni zile siasa zenu zisizoisha?

Tila: Leo Mwalimu Meli alituelezea jinsi mifumo ya uzalishaji mali ilivyobadilika, kuanzia wakati wa ujima, ukabaila, ubwanyenye, ujamaa hadi sasa tunapopambana na utandawazi. Lakini anasema ujamaa si rahisi kutekelezwa.

Ridhaa: *(kwa wasiwasi)* Kipi kiini hasa cha kufunza mada hii kwa watoto wakembe kama nyinyi? Siku zetu sikumbuki kuona mada hii hata katika mtaala wa kidato cha sita!

Tila: Nadhani umesahau baba. Suala hili ulisema limeshughulikiwa katika kazi za kifasihi kama vile *Mashetani*, ile tamthilia ya Hussein inayoisawiri migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya baada ya ukoloni. Isitoshe, mwalimu alitaka tu kuonyesha kwamba upo uhusiano kati ya mfumo wa kiuchumi na mfumo wa kisiasa. Alituambia kwamba mfumo wa kiuchumi hudhibitiana na mfumo wa kisiasa. Utawala huteuliwa maksudi kuendeleza mfumo uliopo wa kiuchumi kwa maslahi ya watawala na tabaka ambalo linazimiliki nyenzo za uzalishaji mali.

Ridhaa: *(kama aliyeudhika)* Naona mmeanza kuingilia nyanja ambazo ni michezo ya wengine na wanastahili kuachiwa wao.

Tila: Lakini baba, unajua hatuwezi kuyafumbia macho mabadiliko yanayozikumba jamii zetu. Kwa mfano, kura ya maoni ya hivi majuzi yaonyesha kwamba majimbo mengi nchini yanamuunga

mkono Bi. Mwekevu Tendakazi. Ameongoza kwa asilimia sitini. Mpinzani wake wa karibu wa kiume ana asilimia thelathini. Mwalimu alisema kuwa wakati umefika kwa jamii kuacha kupima uwajibikaji wa mtu kwa misingi ya kijinsia. Wote, waume kwa wake, wapewe nafasi sawa.

Ridhaa: Si kwamba napinga hili. Ningekuwa hasidi wa usawa wa kijinsia nisingewapelekeni nyinyi shuleni. Ningemshughulikia Mwangeka tu ambaye jamii inaamini kuwa ndiye mrithi wa mali yangu. Hata hivyo, naona kwamba ni mapema mno kuanza kulitolea hukumu suala la nani anaongoza. Huku kutakuwa kukata mbeleko kabla ya mtoto kuzaliwa.

Tila: *(akichekacheka)* Dalili ya mvua ni mawingu baba. Mara hii kama wapiga kura tumeamua kujaribu mbinu mpya za kilimo. Haya matumizi ya visagalima yameanza kupitwa na wakati.

Ridhaa: Tila! Kumbuka hapo ulipo hata kura yenyewe huna! Naona wamekutia maneno ya uchokozi. Ngojea kipindi kingine cha uchaguzi kifike, utakuwa na haki ya kuchukua kura na kumpigia mwanamke umtakaye. Kwa sasa itabidi utosheke na chaguo letu!

Tila: Lakini baba, sijasema tunataka kiongozi mwanamke. Sisi tunataka kiongozi yeyote, awe mwanamke au mwanamume, atakayeweza kulielekeza jahazi hili letu kwenye visiwa vya hazina. Tufikie kilele cha maendeleo pale tutakapofikia malengo ya kimaendeleo ya

kimilenia. Kiongozi ambaye ataendeleza zaidi juhudi za kukabiliana na wale maadui ambao wewe daima huniambia kuhusu: umaskini, ujinga, magonjwa, *(akisita kumtazama baba)* uhaba wa nafasi za kazi na ufisadi. Je, huu sio uliokuwa muono wa waliopigania uhuru? Siyo ambayo viongozi waliochukua hatamu za uongozi kutoka kwa watu weupe waliyofanya juu chini kutekeleza?

Ridhaa: Na nani kasema viongozi waliopo hawajajikuna wajipatapo? Huoni hata wahasiriwa wa magonjwa sugu kama vile iri na hata UKIMWI wana dawa za bei nafuu za kuwawezesha kudhibiti hali hizi? Je, serikali haijaanzisha sera ya elimu bila malipo kwa shule zote za msingi? Haijagharamia karo ya shule za kutwa katika shule za upili? Kumbuka pia na ule mradi wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi kuanzia darasa la kwanza ana kipakatalishi chake? Ushaona? Hivi karibuni nchi inafikia ile *Vision 2030* hata kabla ya 2030 yenyewe! Je, ni tume ngapi za kuchunguza kashfa za kifisadi ambazo zimeundwa? Hizo si juhudi za kupigana na ufisadi? Serikali imetumia bilioni ngapi katika shughuli ya kuhesabiwa kwa watu mwaka jana? Unajua sababu ya shughuli hii? Viongozi wanataka kupata takwimu sahihi zaidi na za kutegemewa, zitakazowawezesha viongozi kujua mahitaji ya kiuchumi na kijamii ya kila jimbo. Huduma zitaweza kutolewa kwa urahisi zaidi katika kila eneo la ugatuzi.

Tila: Na umaskini, je, baba? Mara nyingi hukuona umejishika tama ukilalamikia asilimia kubwa ya

raia ambao hawamudu hata gharama ya matibabu ya kimsingi. Si wewe unayesema kwamba vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano husababishwa na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa lishe bora, pamoja na wazazi na walezi kutopata elimu kuhusu njia za kujikinga dhidi ya baadhi ya magonjwa?

Ridhaa: *(kwa msisitizo)* Kumbuka kwamba haya malengo ya kimilenia hayajaanza kupigiwa shabaha sasa. Kilichobadilika ni istilahi ya kuyarejelea tu. Mojawapo ya haki za kibinadamu ambazo wanaharakati wa mapinduzi walizipigania ni matibabu bila malipo kwa wasiojiweza kiuchumi, na elimu ya lazima, na bila malipo kwa watoto wote, kufikia umri wa miaka kumi na mitano. Na nadhani kile ambacho mwalimu wenu angewasisitizia zaidi ni kwamba vijana wana jukumu la kuelimishana kuhusu nafasi ya kila mmoja wao katika kuuboresha uongozi uliopo sasa. Watumie vipawa vyao kwa njia endelevu ili kusaidia katika kuzalisha nafasi za kazi badala ya kungojea serikali iwatilie riziki vinywani. Nchi haijengwi kwa mihemko na papara za ujana. Na suala la umaskini? Naona hili ni tatizo la kijamii. Mathalan, watu wanaoishi katika sehemu kame wanastahili kujitahidi kuvumbua mbinu za kuyahifadhi maji ya mvua. Pia, kila eneo la ugatuzi halina budi kuwashajiisha wataalamu wake kujizika katika utafiti ili kuvumbua rasilimali zinazopatikana katika maeneo haya,

hili litayawezesha maeneo yenyewe kuzitumia rasilimali kwa njia endelevu. Haya yoye yatasaidia kupunguza mng'ato wa uhawinde.

Tila: Watayahifadhi vipi maji haya kama mvua yenyewe hainyeshi? Baba, wewe mwenyewe unalalamikia kiangazi ambacho kimezikumba sehemu mbalimbali nchini. Isitoshe, mwalimu asema kwamba asilimia kubwa ya wakazi wa sehemu kame haiwezi hata kumudu kula mara mbili kwa siku. Hizo hela za kununulia matangi ya kuhifadhia maji na kufanyia utafiti watazitoa wapi?

Ridhaa: Basi watumie maji ya mabomba! Si lazima wahifadhi ya mvua! Na huyo mwalimu naona anapanda mbegu za uhasama kati ya viongozi na vijana. Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu za kuvulia, nao wanaona wangoje kuletewa samaki!

Tila: *(akionyesha kuvunjika moyo)* Baba! Umekuwa kama yule kiongozi wa Kifaransa, unayeniambia wewe kila mara, ambaye alipoambiwa kuwa wanyonge hawakuwa na mkate alisema, *"If there is no bread let them eat cake!"* Watu wengi huko mashambani hutegemea mashamba, mvua haijakubali kunyesha kwa muda. Wengi wa wanaofanya kazi za ajira, hufanya kazi za kijungu jiko. Sasa mabomba yatatoka wapi? Na hata kama mabomba yenyewe yangekuwapo, juzi nimesikia katika runinga kuwa bwawa la Fanisi ambalo ndilo lililotegemewa sana kutoa maji kwenye

sehemu kame halitasambaza maji tena kwa sababu kiwango cha maji kimeshuka sana. Mabomba yenyewe yamejikaukia!

Ridhaa: Serikali imeanzisha mpango wa kusambaza huduma za maji na umeme katika sehemu za mashambani, hususan zile kame. Wanachohitaji ni subira tu. Na nadhani mwalimu wenu alisahau kuwaambia kuwa katika baadhi ya sehemu mna machimbo ya mawe ya ujenzi, vito, na hazina za mafuta. Wenyeji wana jukumu la kutumia raslimali hizi kujiendeleza.

Tila: Alituambia hayo pia. Lakini tayari kuna kampuni za kibinafsi ambazo zimetumwa huko kuchimbua madini haya. Isitoshe, kampuni zilizoshinda zabuni za kuyachimbua madini haya ni za kigeni. Uchimbaji wenyewe unafadhiliwa na wawekezaji wa kigeni. Raia watafaidika vipi? Fedha zinazotokana na rasilimali hii yahofiwa kuwa zitaishia kwenye mifuko ya wageni. Zinatumwa kuendeleza nchi za haohao wawekezaji wanaodaiwa kuwa wahisani.

Ridhaa: Ni kweli, lakini kumbuka kampuni hizi zimebuni nafasi za kazi. Wenyeji wamepata ajira!

Tila: Ambayo mshahara wake ni mkia wa mbuzi. Baba, kile ambacho raia wanahitaji ni mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi na sera zenyewe za uongozi! Na naona awamu hii, kama asemavyo mwalimu, wingu la mabadiliko limetanda.

Ridhaa hakuacha kushangazwa na upevu wa mawazo wa mwanawe Tila. Waliweza kukesha wakijadiliana kuhusu

masuala nyeti kana kwamba wao walikuwa marika. Tila alipenda sana masuala yaliyohusiana na sheria, haki na siasa. Alijua kuwa siku moja atakuwa jaji katika mahakama kuu.

"Siku hiyo," alizoea kumwambia babake, "ndipo kesi za jinai ambazo zimeselelea mahakamani kwa miongo miwili au zaidi bila kusikizwa, faili zake zitapatikana zilikojifungia na kuamuliwa! Ndipo washukiwa ambao wamewekwa rumande kwa miaka yote hiyo wataonja utamu wa haki."

Sasa Ridhaa anapotazama picha iliyo mbele ya macho ya akili yake, anajua fika kuwa Tila wake hayupo, kilichobaki ni kumbukumbu zake, kumbukumbu ambazo zinang'ata kama mkia wa nge, kumbukumbu ambazo kila mara zilifungua chemchemi za machozi, yakalovya kifua chake. Sasa anapotazama nyuma anaona kuwa ule utabiri wa 'wingu la mabadiliko' wa mwalimu ulikuja kutimia. Viongozi wengi wa awamu ya awali walibwagwa chini na vijana chipukizi. La kuhuzunisha ni kwamba wengi walishindwa kabisa kukubali ushinde, hasa yule ambaye alikuwa anagombea kilelecha cha uongozi. Kulingana naye, nafasi hii iliumbiwa mwanamume, na kupewa mwanamke ni maonevu yasiyovumilika!

Alipita kila mahali akisema, "Hili ni wingu la kupita na bila shaka wingu la kupita halipaswi kumtia mkulima matumaini. Tutapambana, sheria tunaijua." Kauli zake ziliwajaza hamasa masahaba wake, wakaanzisha fujo, fujo ambazo zilionekana kuwa cheche moja ya moto, zikapuuzwa! Kumbe zingekuwa jahanamu ya kuangamizia juhudi za miaka hamsini za raia kuijenga jamii yao! Cheche hizi ndizo zilizoichoma aila ya Ridhaa, ndizo zinazouunguza moyo wake hata sasa.

"Ndege kwa jina PANAMA 79 iliyotarajiwa kufika saa tatu unusu sasa ndio inaipiga pambaja sakafu," sauti nyororo

ya kike ilitangaza. Ridhaa aliisikia sauti hii kwa mbali japo alikuwa akiutazama ubao ambao huandikwa ratiba ya kuwasili kwa ndege. Tangazo hili ndilo lililomrudisha katika mandhari yake ya sasa. Hakujua alikuwa ameyaishi maisha yake ya awali kwa muda mrefu tangu saa moja unusu asubuhi. Alijaribu kuangaza macho yake aone anakoenda. Macho yalijaa uzito wa machozi ambayo alikuwa ameyaacha yamchome na kutiririka yatakavyo. Alikihimiza kiwiliwili chake, kikaamka. Anakwenda kumlaki mwanawe.

Mtu na mwanawe walitazamana kimya, kila mmoja akitweta kwa mpigo wa kasi wa moyo. Wanataka kukimbiliana na kuvaana ila hakuna anayetaka kuanza. Umbali ulio kati yao, japo ni hatua tatu tu, waonekana kama upana wa Bahari ya Shamu wakati Waisraili walipokuwa wakikamia wokovu wao kutokana na dhuluma ya Wamisri. Ridhaa alihisi kana kwamba anaona mzuka wa Mwangeka. Ingawa Mwangeka alimtumia barua meme kila uchao, baba mtu hakuamini kuwa angerudi nyumbani akiwa hai. Alikuwa ameumwa na nyoka, bafe hasa, na bila shaka mwenye kuumwa na nyoka akiona ung'ongo hushtuka. Polepole picha halisi ya mwanawe ilianza kurejea akilini, ikamsadikisha kuwa anayemkazia macho ni kifungua mimba wake. Fahari ya uzazi na ulezi iliyeyusha woga na shaka, akanyoosha mikono yake kumkumbatia mwanawe. Mwangeka alijitupa kifuani mwa babake kwa mwanguko mkubwa, jinsi alivyozoea kumwangukia zamani akiwa amelala juu ya kochi, wakati akimwigizia mpiganaji miereka maarufu kwa jina 'Yoko' au Yokozuna. Ila wakati huu Ridhaa hakumkemea mwanawe kwa kile alichozoea kukiita *Roughness*. Alikiacha kitendo hiki kiyafufue maisha yake na familia yake. Walishikana kukutu, kila mmoja akimwambia

mwenzake kimoyomoyo, "Ni hai! Sijafa!" Ikawa ni kama Yesu anamhakikishia 'Tomaso Asiyeamini', "Tazama, hii mikono yangu. Nipe mkono wako, utie ubavuni mwangu. Usikose kuamini tena. Amini!" Mwangeka alidiriki kusema, "Baba! Baba yangu!"

"Mwanangu, karibu nyumbani. Karibu kwenu. Sikujua kama tutawahi kukutana ukiwa hai. Hali iliyoikumba jamii yetu hivi karibuni imeyafanya maisha kuwa jambo la bahati nasibu. Huko ulikoenda ulitumwa kudumisha amani; kujenga. Sasa unarejea kwenu kupata tumekuporomosha kwa viganja vyetu wenyewe. Nakusikitikia mwanangu, kuwa huna hata familia ya kuendea. Wanuna wako wote wameangamia. Mkaza mwanangu na maskini mwanao waliunguzwa na moto, wasibaki hata mafuvu ya kuzika! Huna hata makaburi ya kuwekea hayo makoja ya maua unayoyatunga akilini mwako."

Mwangeka aliinua kipaji chake, akatazamana na baba yake.

"Baba amekonga zaidi. Uso wake umeshamiri weusi na unyonge," alijisemea akilini, "sasa amemshabihi babu Mwimo zaidi, hasa kule kupwaya kwa ngozi yake."

Mwangeka anapowaza haya ya babu anatetemeka kidogo na kutabasamu. Bila shaka amekumbuka kitu lakini huu si wakati wa kudekeza fikira kama hii. Na hakika mja huyu alikuwa kabadilika! Si yule Ridhaa ambaye Mwangeka alizoea kumwona miaka michache iliyopita. Si yule baba ambaye angekimbizana naye kila jioni, wakicheza mchezo wa baba na mwana, akiingia mvunguni mwa meza, nyuma ya milango ... Siye baba ambaye Mwangeka, kwa utundu wake wa kitoto, angemnyang'anya stetheskopu yake, na

kuitia kwenye shingo yake yeye Mwangeka, kisha anamlaza baba yake juu ya kochi; baba ni mgonjwa wa Dkt. Mwangeka! Daktari anausikiliza mpigo wa moyo wa muwele wake. Baba mtu akijaribu kufurukuta anatishiwa kudungwa sindano! Siye! Siye hata kidogo! Kilichobakia ni lile tabasamu lake la daima, lililozoea kumhakikishia usalama siku zote, tabasamu ambalo lilidhihirisha meno meupe pepepe yenye mwanya mkubwa wa kuvutia, mwanya ambao Ridhaa alikuwa amezoea kumwambia Mwangeka kuwa mwanya huo ndio ndoana ambayo aliitumia kumvulia mama yake! Hata Mwangeka anapolitazama tabasamu hili sasa hivi, anahisi kama amezingirwa na uzio imara. Sasa anajua yote ni salama. Anakumbuka wimbo ambao mama yake alizoea kumwimbia kila mara baba yake alipokuwa ameenda katika safari zake za kikazi. Siku hizo Mwangeka angeonekana kuwa dhaifu na mwenye mashaka. Mama mtu angemshika mabegani na kumwimbia mkarara mmoja wa wimbo pendwa wa kidini:

Salaama, salama
Rohoni, rohoni
Ni salama, rohoni mwangu

"Asante baba," hatimaye Mwangeka alidiriki kusema, "nafurahi kwamba nimekuona. Nilipoona yaliyotokea humu kupitia kwenye runinga, na mitandao mingine ya kijamii; ubadhirifu wa mali, uchomaji wa watu kama makaa, msongamano na magonjwa katika kambi, kisha barua meme iliyonijuza kuhusu msiba uliotupata, niliingiwa na kihoro kisicho na kifani. Hata hivyo, nimekuwa nikiyafuatilia matukio ya humu. Hata kura zilipohesabiwa upya kisha mpinzani wa Mwekevu kukubali kushindwa na kutoa wito kwa raia kusahau

yaliyopita na kuganga yajayo, nilijua kuwa nchi hii imepiga hatua moja katika safari ndefu ya kupata afueni kutokana na tufani za baada ya kutawazwa. Nawapa heko vijana wenzangu kwa kugundua kuwa wanatumiwa na viongozi wenye tamaa kama vipulizi vya kupulizia sumu mshikamano wa kijamii. Sasa ninaamini usemi wa Tila wa kila mara kuwa: "Usicheze na uwezo wa vijana, wao ni kama nanga. Huweza kuzamisha na kuiongoa merikebu. Inasikitisha kwamba badala ya kuliongoa jahazi letu wameligongesha mwamba bila kujua."

Ridhaa aliitikia maneno ya mwanawe kwa mgoto wa kichwa. Moyoni alijua kuwa bado palikuwa na kazi ngumu ya kujenga upya ukuta ambao ufa wake ulikuwa umepuuzwa. Ni kweli kuwa jamii ya kimataifa ilikuwa imeingilia kati na kurejesha amani, lakini hii, bila yeye na raia wenzake kuziunga mkono juhudi za viongozi za kurejesha kuaminiana na kuthaminiana, licha ya tofauti zao, ilikuwa amani ya kifauongo tu. Ndio, anakubaliana na sera ya marehemu binti yake Tila, kwamba vijana wanapaswa kuelimishwa zaidi kuhusu natija ya amani, wao ndio wengi, ndio mhimili wa jamii yoyote ile. Hata hivyo, elimu yoyote, bila kielelezo chema kutoka kwa wanaoitoa elimu yenyewe, ni sawa na juhudi za mfamaji. Ridhaa alishusha pumzi kama kuli ambaye ameutua mzigo mzito bandarini, akamkabidhi mkono Mwangeka, akamwambia:

"Twende mwanangu," akasema Ridhaa, "unahitaji kujipumzisha kutokana na adha za anga. Tumezungumza tukasahau mwili una machovu. Mengine tutayazungumza baadaye."

Sura ya Nne

Mwangeka alikuwa kaketi mkabala mwa kidimbwi cha kuogelea, nje ya jumba lake ambalo japo lilisimama kwa haiba kandokando mwa ufuo, kwake yeye jumba hili lilikuwa makavazi, si ya kumkumbusha turathi za jamii yake, bali ya kumtonesha donda lililosababishwa na kifo cha mke wake Lily Nyamvula.

Siku ile baada ya kutoka uwanja wa ndege walifululiza moja kwa moja hadi kwenye gofu la baba yake Ridhaa. Hapakuwa na haja ya kuelezewa lolote. Kila kitu kilikuwa wazi. Mbele ya macho yake mlisimama kiunzi cha lile lililokuwa kasri la babake. Majivu yaliyokuwa mabaki ya kilichokuwa kwenye kasri lile bado yalibakia pale pale, kama yalivyokuwa siku hiyo ya siku. Kila kitu kilikuwa wazi. Majivu na mashizi haya ni miili ya mama yake, wanuna wake, mkewe na mtoto wake. Alimtazama baba yake kana kwamba anataka kuhakikishiwa jambo, naye Ridhaa akamjibu kwa mtazamo uliojaa imani, "Mwenye macho haambiwi tazama." Ambalo halikumkaa Mwangeka vyema akilini ni kiini cha baba yake kutoyaondoa mabaki ya jumba hili.

"Je, kwani baba amekuwa mwehu! Kwa nini hata hakushikana na majirani akachimba ile *mass grave* na kuyazika majivu haya?" Alijiuliza Mwangeka.

Baba mtu alimkazia tu macho, kana kwamba anamwambia, 'Kuna mambo ambayo sharti yatendeke kinyume na kaida za kimaumbile; si lazima maisha ya binadamu yafuate kanuni zilezile kila mara. Wakati mwingine nadhari ya binadamu hutulia tu pale anapodengua hali. Sijui kama kijana umesoma ile nadharia ya *deconstruction*. Ni muhimu pia ujue kwamba ikiwa unataka kujiokoa au kuzoea hali mbaya inayokukabili, ni muhimu kujiingiza katika hali yenyewe, ukaikabili vilivyo ili uache kuiogopa, au iache kukuathiri vibaya. Hii ndiyo sababu nikapaacha mahali hapa jinsi palivyo licha ya rai za jamaa na marafiki kupabadilisha. Najua huenda usiyaelewe haya. Hata hivyo, ishi, utakuja kuyatambua kijana.'

Matone mazito ya machozi yalitunga machoni, Mwangeka akayaacha yamdondoke na kumcharaza yatakavyo. Wakati huo hata nyanya yake angekuwapo kumwonya dhidi ya kulia kama msichana, angempuuza. Yapo mambo ambayo ni faradhi, hata kwa mwanamume! Alihitaji kuliondoa komango ambalo lilikuwa limefunga mishipa ya moyo wake. Uvuguvugu uliotokana na mwanguko wa machozi haya uliulainisha moyo wake, ukampa amani akali. Moyo wa Mwangeka sasa ulijaa utulivu. Usidhani ni utulivu wa kuridhika kwa jambo. La hasha! Ni utulivu unaotokana na imani na mazoea ya kila mtu kuwa mja hana hiari. Akili yake ilimkumbusha methali aliyozoea kumtolea mpinzani wake darasani kila mara Mwangeka alipomshinda kuwa, wino wa Mungu haufutiki. Sasa ndio Mwangeka anauona wazi ukweli wa methali hii. Hili ndilo lililompata na bila shaka halikuweza kufutika. Jambo ambalo alizidi kujiuliza ni, "Je, binadamu aliandikiwa kumpoka binadamu mwenzake maisha?"

"Mwanangu," alisema Ridhaa siku hiyo baada ya kutoka kwenye uwanja wa ndege, "maisha yalitubadilikia mara tu baada ya kuondoka kwako. Tuliandamwa na msiba baada ya mwingine. Kwanza nilipoteza majumba yangu mawili. La kwanza ni lile lililokuwa katika mtaa wa Zari. Ilisemekana kuwa wahandisi na masoroveya hawakunishauri vyema, kwamba jumba hili, pamoja na mengine mengi, yalikuwa yamejengwa kwenye sehemu iliyotengwa kwa ujenzi wa barabara mbadala. Ilibidi yabomolewe ili shughuli za kujenga *bypass* zianze kwa dharura kwa kusudi la kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu. Mpaka sasa hiyo *bypass* haijaanza kujengwa! Yasemekana shughuli za kutangaza zabuni ya kandarasi ya ujenzi bado zinaendelea. Hatukupewa fidia yoyote kwani sisi ndio tuliokuwa na hatia. Ulikuwa mwiba wa kujichoma ati! Waliotuuzia viwanja hivi waliingia mitini. Jumba jingine ambalo nilikuwa nimewapangishia wafanyabiashara nalo lilichomeka. Inasemekana kulikuwa na hitilafu ya umeme. Nguvu za umeme na mlipuko wa gesi vililisagasaga jengo zima, likawa unga tifutifu. Watu wengi walifia humo ndani kwani shirika la zima moto lilitaahiri kufika, nao wenye maduka hayo, kwa kuhofia kuporwa kwa mali yao na roho zinazoupania uhai, wakaifunga milango yote ya kuhepea. Hata walipotanabahi kuwa maiti haiwezi kuiba, na kufungua malango haya, ni roho chache tu zilizokuwa zimenusurika."

Ridhaa alisita, akajipangusa kijasho kilichokuwa kimetunga kipajini mwake, akatoa kitambaa mfukoni na kuyafuta machozi ambayo yalikuwa yameanza kumpofusha, kisha akaendelea.

"Msiba huandamwa na mwingine. Miezi mitatu baadaye ami yako Makaa, ambaye alikuwa akifanya kazi kwenye machimbo ya mawe ya Nuru, alichomeka asibakie lolote. Kisa na maana, alikwenda kuwaokoa watu ambao walikuwa wakipora mafuta kutoka kwenye lori ambalo lilikuwa limebingiria. Inasemekana kuwa umaskini uliwasukuma watu hawa kuchukua kisichokuwa haki yao! Mmoja wa wahasiriwa alisikika akiuliza, 'Ya nini kuacha mali nyingi hivi kuiosha sakafu na hali watu wanatafunwa na umaskini mithili ya mafunza? Tutayasomba mafuta haya. Yatapata matumizi hivi punde. Madereva wa wakubwa watayachanganya na yale waliyofyonza kwa mirija kutoka kwenye magari ya waajiri wao, na kuwauzia wenye magari ya kibinafsi. Hawa wakijitia ucha Mungu na kudinda kununua, kuna walinda usalama wenye njaa, watayanunua na kujua watakapoyatoa kama kafara!'

"Baada ya muda, lori lilivamiwa na nzige ambao hawakuwa na hadhari. Rai za wapita njia za 'Jamani injini ya lori hili bado inanguruma na huenda moto ukazuka' ziliangukia masikio ya fisi. Kutanabahi miili ya waja iligeuka kuni. Moto ulitutuma kwa hasira. Ami yako alipoona binadamu wanaokumbatiwa na moto huku wakitimua mbio, imani ilimtuma kwenda kuwaokoa. Kumbe anakwenda kuingia kwenye mtego wa panya unaowanasa waliomo na wasokuwemo! Ndimi za moto kutoka kwenye lori lililolipuka zilimvamia pia, akaungana na roho nyingine zilizokuwa zimesalimu amri. Serikali ilitayarisha mazishi ya umma, tukayazika mabaki ya wahasiriwa wote katika kaburi moja. Ila sidhani tulibahatika kuwa na sehemu yoyote ya mwili wa ami yako. Pengine tuliyozika ni nafsi yake tu!"

Ridhaa alishusha pumzi na kuendelea, "Haya yote niliyakabili kwa msaada wa wanuna wako, mama yako na mkaza mwanangu. Nilianza kuyajenga maisha yangu upya hadi siku hii ambayo niliitazama familia yangu nzima ikiniponyoka kutoka kwenye kitengele changu. Ndio, Mwangeka ulizoea kuniita Dkt. Ridhaa lakini siku hiyo niliamini kuwa mganga hajigangi. Katika maisha yangu yote kama mwanafunzi wa udaktari, na baadaye masomo ya uzamili katika taaluma ya upasuaji, sikuwahi kujihisi kama asiyeweza kuyahimili maisha yake jinsi nilivyohisi siku hii. Hapa nilipo nina uzoefu mkubwa katika utabibu. Nimewaokoa wagonjwa wengi kutokana na magonjwa sugu. Nimewatoa wengi mikononi mwa iziraili. Hata hivyo, nilishindwa kabisa kuuzima moto uliokuwa ukiiteketeza nyumba yetu. La, sikushindwa kwani hata sikuwepo tendo lenyewe lilipotokea. Ninachokumbuka ni kwamba asubuhi hiyo ya dhiki niliitwa hospitalini kumfanyia majeruhi mmoja upasuaji. Huyu alikuwa ameumizwa sana katika mkurupuko wa watu waliokuwa wakiandamana dhidi ya matokeo ya uchaguzi wa wawakilishi wa eneo-gatuzi katika kata yao. Walinda usalama waliwatupia vitoza machozi baada ya kuwafumania wengi wao wakipora mali kwenye maduka yaliyokuwa karibu. Katika kule kukimbia, mhasiriwa huyu alianguka akakanyagwa na waliokuwa wakihepa na mali ya wizi, na kuumia vibaya. Mishipa yake ya hisi iliathirika vibaya, ikabidi tumfanyie upasuaji wa uti wa mgongo."

Ridhaa aliendelea, "Basi nikiwa njiani kurejea nyumbani, nilisikia sauti ya kite ya mama yako, kisha mlipuko mkali. Yote yakaisha. Nimeishi maisha ya kinyama ya kupigania chakula na wahitaji wenzangu. Nimeonja shubiri ya kuwa mtegemezi

kihali na mali. Lakini katika yote hayo, nimejifunza mengi. Nimejua thamani ya maisha, udugu na amani." Ridhaa alimaliza usimulizi wake na kushusha pumzi kama mpagazi aliyekuwa ameutua mzigo mzito. Alimtupia jicho la huruma Mwangeka ambaye uso ulikuwa umesawijika kwa sikitiko.

"Maskini mwanangu, hata maisha ya unyumba hakuwa ameyakinai. Amekuwa mjane hata kabla ya ubwabwa wa shingo kumtoka!" Aliwaza Ridhaa.

Mwangeka hakuishi na baba yake kwa muda mrefu baada ya kurejea kwake. Kwanza, hakuweza kustahimili uchungu uliosababishwa na kuamka kila asubuhi kutazama mahali ilipoangamia aila yake. Kila siku alimshawishi baba yake akibomoe kiunzi kile cha nyumba, naye baba mtu alikataa katakata. Alishikilia kuwa hilo ndilo kaburi la ukumbusho wa familia yake. Pili, ilibidi Mwangeka ayaanze maisha yake upya, atafute mbinu za kumwezesha kukabiliana na hali yake ya ukiwa. Atafute ushauri kutoka kwa wataalamu, auuguzie moyo wake mbali na babake.

Baada ya kurejea katika shughuli zake za kawaida kazini, Mwangeka alitafuta kiwanja cha kujengea nyumba. Baba yake alimtahadharisha dhidi ya kuanza ujenzi kabla ya uchunguzi kufanywa kuhusiana na kiwanja chenyewe. Siku hizo masuala kuhusu umiliki wa ardhi hayakupigwa darubini kama ilivyo sasa. Visa vya watu kuuziwa hata sehemu zilizokuwa maziara vilikuwa vimeongezeka. Walioangukia mtego huu, baada ya kuchora ramani zao, walipigwa na butwaa walipowapeleka wahandisi na mafundi na kupata kuwa makaburi yamejikita kwenye viwanja vyao! Haikuwa ibra hata kuuziwa kipande cha ardhi ambacho kilikuwa tayari kimeuzwa, mtu ukapewa

hatimiliki bandia, huku ile halali imetwaliwa na mnunuzi wa kwanza. Wakati unapotaka kujenga unaambiwa, "Ndugu, ardhi hii si yako."

Wengine ambao hawakubahatika kugundua njama za kifisadi walidiriki kujenga majumba ya kifahari ambayo baadaye yalikuja kugeuzwa vifusi, kisa na maana, yamejengwa kwenye uwanja wa ndege au maeneo yaliyotengewa barabara. Baada ya panda shuka za kuhakikisha uhalali wa stakabadhi hii na ile, hatimaye Mwangeka alipata kipande cha ardhi karibu na ufuo wa bahari. Kwa vile Mwangeka alikuwa mhandisi wa ujenzi, haikuwa vigumu kwake kupata wahandisi na wachora ramani bora kwa sababu ya mtandao wake wa kikazi. Kazi ya ujenzi ilianza na baada ya takriban mwaka mmoja na nusu Mwangeka akahamia kwake.

Hata anapokitazama kidimbwi hiki, mawazo yake yako mbali kule-e-e alikoanzia maisha. Anakumbuka changamoto za ukuaji wake. Anawakumbuka wanuna wake, Kombe, Mukeli na Annatila, ambaye wakimwita Tila. Anapomkumbuka Annatila mwili unamzizima kidogo, anatabasamu kisha tone moto la chozi linamdondoka. Kumbukumbu ya Annatila inavuta taswira ya mnuna wake mkembe ambaye alifariki dunia akiwa na umri wa miaka sita. Mwangeka alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili tanzia hii ilipowafika.

Katika jamii ya Mwangeka, kifo kilifuatwa na viviga vya aina mbalimbali, yakiwamo maombolezi. Shughuli za matanga ziliandamana na uimbaji wa mbolezi kabla na wakati wa mazishi. Basi baada ya kifo cha mtoto huyu, majirani walikuja kuihani familia ya Bwana Ridhaa, na bila shaka kuna waliokuwa wakilia wakizunguka ua wa nyumba. Wengine

walilia wakiimba na kuzunguka kaburi. Siku ya mazishi kilio kilizidi hata kikakebehi juhudi za elimu ya kisasa. Mwangeka alishangaa kumwona Dkt. Ridhaa, kama alivyozoea kumwita baba yake, akilia. Wapo akina mama ambao walijifunga mkaja kulia huku wakizunguka jeneza la marehemu. Haya yote Mwangeka na wanuna wake waliyashuhudia kwa kuajabia. Kwao ulikuwa kama mchezo tu wa kuigiza. Kwa hakika Mwangeka mara moja moja alionekana akiwacheka akina mama hawa kwa jinsi walivyokibuni kilio, wakakikuza hadi kikawa kemi, wakawa wanakimbia wakilia huku wameshikilia vichwa vyao kwa mikono miwili kana kwamba wanahofia kuwa vitaanguka!

Mwangeka anakumbuka Jumamosi moja wiki mbili baada ya mazishi ya ndugu yake. Alikuwa ametoka shuleni, siku hizo walimu walikuwa wameng'ang'ania kuwafunza Jumamosi wanafunzi waliokaribia 'ICU' kama walivyoliita darasa la nane. Walidai kuwa hii ndiyo njia mwafaka ya kuwapiga msasa. Mwangeka alimpata Tila na wenzake nyuma ya nyumba wakimngojea, macho yametwaa wekundu wa kutiwa, yamepakwa mate, ndiyo machozi ati! Tila alimvuta na kumnong'onezea kitu sikioni. Yaliyofuata Mwangeka angeishi kuyajutia hadi sasa. Tila alivuta boksi lililokuwa limetiwa mwanasesere wao kwa jina Dedan Kimathi, ndiyo lakabu waliyokuwa wamempa marehemu ndugu yao—Dede. Alililweka katikati yao kisha akaanza kuvuta kilio. Wengine walijilazimisha kupiga ukemi, eti wanaomboleza kifo cha Dedan Kimathi. Walianza kulizunguka lile 'jeneza' wakiimba mbolezi ifuatayo:

Kwaheri we Kim wetu kwaheri
Kwaheri, kwaheri
Kwaheri we Kim kipenzi chetu kwaheri
Kwaheri na malaika wakungoje.

Umewaacha wazazi kwa majonzi
Kwaheri, kwaheri
Umewaacha na nduguzo kwa ukiwa
Kwaheri na mababu wakulaki peponi.

Wimbo huo ulirudiwarudiwa, ukiandamana na vilio vya kujitia. Mirindimo ya miguu yao ilijenga wizani ambao ulizidisha hali ya ukiwa na maombolezi. Hatimaye boma la Mzee Ridhaa liligeuka kuwa uwanja wa maombolezi. Machozi ya dhati yalitwaa nafasi ya mate, watoto wote, akiwemo Mwangeka, wakalia kwa shake na imani.

Katika hali hii, watoto hawakuwa na mwao kuhusu kuja kwa baba yao. Ridhaa alikuwa amefika dakika thelathini zilizopita na kujibanza kwenye kiambaza cha jiko ili kushuhudia mazishi haya. Aliwatazama wanawe wakiigiza mazishi ya marehemu ndugu yao, akawaona polepole wakigeuka kuwa wehu. Fundo chungu lilitunga kooni mwake, akahisi kama anasagwasagwa na wana aliowazaa. Hakujua jinsi alivyotoka alipokuwa. Aliutwaa mshipi wake kutoka kiunoni, akamshika Mwangeka kwenye ukosi wa shati lake na kumhujumu kwa mshipi huu mpaka viguu vyake vikapata alama. Juhudi za Mwangeka za kujitetea hazikufua dafu. Mwangeka alisema kuwa Tila ndiye aliyewashawishi kuomboleza, naye baba akasema kwamba

Mwangeka ndiye kifungua mimba, anastahili kuwa kielelezo chema kwa wanuna wake, bali si kuwa bendera ya kufuata upepo.

"Tila ni mtoto, tena msichana. Vipi dume kubwa kama wewe litafuata mkondo kama maji bila nadhari?" alifoka baba kwa ghadhabu zilizozidishwa na majonzi.

Mwangeka anapokikumbuka kisa hiki anashangaa kwa nini hakupata hata fursa ya kuomboleza kifo cha Annatila.

Baada ya kipigo hiki cha babake Mwangeka aliapa kuwajibika zaidi. Aliinamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. Hapo ndipo alipokutana na mkewe Lily Nyamvula. Siku hizo Nyamvula alikuwa akisomea uanasheria. Mwangeka alihitimu masomo yake, akajiunga na kikosi cha wanamaji, jambo ambalo liliwashangaza wengi. Siku hizo watu walikuwa na imani potofu kuwa uanajeshi ulitengewa tu watu wa viwango vya chini vya elimu. Hata hivyo, hili ndilo alilolitaka Mwangeka. Na tangu hapo alikuwa ameanza uhandisi akiwa katika shule ya msingi, siku za mizaha yake na binamu yake Mwangemi, maarufu kwa lakabu Tesi, siku alipovumbua gari la kienyeji!

"Kwa kweli hizo zilikuwa siku," alijiambia Mwangeka huku akitaka kukumbuka kisa chake na Tesi, lakini akayakandamiza mawazo haya.

Ukiwauliza marafiki wa chuoni wa Mwangeka watakwambia kwamba Mwangeka kujiunga na vikosi vya usalama ni kuipoka taaluma ya uhandisi mhimili maalum. Hata hivyo, Mwangeka alitamani kutoa huduma yake ya uhandisi katika vitengo vinavyoshughulikia usalama wa wananchi, awahudumie raia wengi iwezekanavyo. Huu

kwake ndio uliokuwa uzalendo. Mwanzoni Nyamvula aliipinga hatua hii ya Mwangeka. Kulingana na Nyamvula, kuwa askari wa vita kulikinzana na imani yake, hasa kwa vile Nyamvula alisema yeye ni *Born again*. Mwangeka alimsisitizia kuwa kulinda usalama si sawa na kuua. Nyamvula alipoona kuwa msimamo wa Mwangeka hautetereki, aliridhia shingo upande. Mwangeka aliajiriwa na kupanda ngazi moja baada ya nyingine hadi alipoenda kudumisha amani kwingine na mkewe kufa kutokana na ukosefu wa usalama nchini mwao! Huu ukawa mwisho wa ndoa yao ya miaka mitatu!

"Kama ningeusikiliza ushauri wa Tausi wangu labda ningeweza kuiokoa aila hii ... labda mke wangu angekufa kifo cha faraja ... labda ningemwona maskini mwanangu ambaye nimewahi kumwona kwenye picha ambazo Tausi wangu alinitumia," aliwaza Mwangeka huku akimeza funda la mate machungu. Magharibi imeingia. Anainuka kuenda kupambana na usiku wenye upweke na hamaniko isiyo na kifani.

Sura ya Tano

Msitu wa Mamba uligeuka kuwa nyumbani kwa maelfu ya watu waliogura makwao bila tumaini la kurudi. Wapo waliotumwa na mioyo yao kutamani kurudi kwao. Hata hivyo walijiasa, wakasema kuwa hata kule walikokuwa wakiishi hakukuwa kwao; walikuwa maskwota! Waliamua kulimbukia maziwa na asali ya Kanaani hii mpya, isiyokuwa na mwenyewe, kama walivyodai. Matokeo ya uamuzi huu yalikuwa kukata miti kwa ajili ya kupata mashamba ya kupandia vyakula na kwa ajili ya ujenzi, polepole mioshi ikaanza kuonekana ikifuka kutoka kwenye msitu ambao tangu hapo ulikuwa marufuku kwa binadamu. Usicheze na binadamu apatapo nyenzo ya kujiinua! Kabla ya miaka miwili kuisha, mahali hapa palikuwa pametwaa sura mpya—majumba yenye mapaa ya vigae, misitu ya mihindi na miharage, maduka ya jumla, viduka vya rejareja … almuradi kila mtu alijifunga mkaja kutunisha kibindo chake; kufidia alichokuwa amekipoteza hapo awali!

Familia ya Bwana Kangata ilikuwa miongoni mwa zile zilizoselelea kwenye msitu huu. Kwa Kangata na mkewe, Ndarine, hapa palikuwa afadhali. Hawakuwa na pa kwenda kwani hata kule ambako walikuwa wakiishi awali, hakukuwa kwao. Walikuwa wamelowea katika shamba la mwajiri wao ambaye alikuwa akiishi jijini. Waliishi hapa kwa muda mrefu

hata watu wakadhani kuwa hii ilikuwa milki yao. Wengine hata walidhani kwamba Kangata na familia yake walikuwa akraba kindakindaki ya mwajiri wao. Kwa hakika hata watoto wa Kangata walipokwenda shuleni walijisajilisha kama wana wa tajiri wa baba yao! Walikuwa wakiitwa Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na Akelo Kiriri. Kiriri lilikuwa jina la mwajiri wa Kangata. Mpaka sasa kifungua mimba huitwa Lunga Kiriri-Kangata. Hilo la Kangata lilikuja kuongezwa katika utu uzima baba mtu alipoona kwamba huenda jina lake likafifia kabisa.

Kangata na mwajiri wake walikuwa wamesekuliwa kutoka mtaa wa Matunda katika zile zahama za baada ya kutawazwa. Tajiri wake alikufa muda mfupi kutokana na kihoro cha kufilisika na ukiwa aliokuwa ameachiwa na mkewe Annette na wanawe ambao walipata kile wazalendo wa kikwetu hukiita *Green Card* na kuhamia ughaibuni. Juhudi za Kiriri za kumshawishi mkewe asimnyime ushirika wa wanawe ziliangukia moyo wa Firauni. Mama mtu alikuwa ameamua kwamba hapa hapamweki. Alikuwa amehudumu katika afisi za umma kama mhazili mwandamizi kwa miaka mingi mpaka kazi hii akaiona inamfanya kusinyaa, hana hamu tena. Alipoifikiria kila asubuhi, kama alivyosikika akisema, alihisi kinyaa. Wanawe walipokwenda kusomea ng'ambo kama wafanyavyo wana wa viongozi ambao wanaiona elimu ya humu kama isiyowahakikishia mustakabali mwema raia wake, yeye alistaafu mapema akapewa kile kibunda cha mkupuo mmoja almaarufu *Golden Handshake*, akachukua *Green Card* na kuwafuata, licha ya rai ya mume mtu akae naye waondoleane upweke.

Bwana Kiriri aliachiwa watumishi na vimada wake, kama alivyodai mke wake Annette. Baada ya wana wa Kiriri

kumaliza masomo yao, walibakia huko huko Uzunguni kufanya kazi. Baba mtu kila mara aliwarai kurudi nyumbani angaa kusaidia kuziendesha baadhi ya biashara zake lakini kila mmoja alishika hamsini zake huko ng'ambo.

"*This country has nothing to offer.* Nchi ambayo hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mishahara ya mkia wa mbuzi! Mimi sitakufa maskini. Acha niwekeze huku mbali ambako sina hofu ya mali yangu kuibwa au kuchomwa na waivu wangu," alisikika akisema Songoa, kifungua mimba wa Kiriri.

Kabla ya kifo chake, Kiriri hakuisha kuibua mijadala nafsi akilini mwake kuhusu Waafrika ambao aliwaona kama waachao mbachao kwa mswala upitao.

"Kipi kinachowavuta raia kuhamia ughaibuni?" angeiuliza nafsi yake pale ambapo mzigo wa simanzi na ukiwa ulipokilemea kifua chake. "Je, ni huo mshahara mnono unaowageuza kuwa watumwa wa kufanya kazi kidindia ati kwa kudai kuwa nchi za ughaibuni ni *twenty-four-hour economies?* Ni hizo kazi za kujidhalilisha, mtu kwenda kuwauguza maajuza waliotelekezwa na aila zao kwenye makao ya wazee na watu wenye mahitaji maalum? Ni zile ndoa kati ya vijana wakembe wa Kiafrika na vikongwe vilivyochungulia kaburi?" angeendelea kujiuliza Kiriri huku akishangaa ikiwa mkewe amegeuka wale wake ambao pindi wafikapo ng'ambo hufunga ndoa na waume wengine, kisa na maana, ndio njia ya pekee ya kufukuza upweke na kulimbuka riziki, au kwa kutaka kujikwamua kwenye tope la uhawinde?

Kangata alibahatika kufika kwenye Msitu wa Mamba ambapo, kutokana na uzoefu wake katika kilimo, aliweza

kuendeleza kilimo chenye natija. Miaka mitano imepita. Kangata na mkewe Ndarine wameipa dunia kisogo. Lucia Kiriri–Kangata ameolewa katika ukoo wa Waombwe ambao awali walikuwa maadui sugu wa ukoo wa Anyamvua. Kwa kweli ukoo mzima ulipinga ndoa hii kwa jino na ukucha. Isingekuwa kwa msimamo wa Kangata usiotetereka, Lucia angebakia kuozea kwao bila mume. Ami zake walikuwa wamekataa katakata.

"Utamwozaje mwanetu kwa mtu wa ukoo ambao huvaa nguo ndani nje? Ukoo ambao unazaa majoka ya mdimu ambayo hata kiporo cha juzi ile hayawezi kukupa?" alisikika ami ya Lucia akilalamika.

"Hao waombwe msemao ndio waliomkuza Lucia wakati ambapo nyinyi nyote mliniita kidengereka. Bwana Kiriri aliyadhamini masomo ya mabinti zangu licha ya kujua kuwa sisi ni Nyamvua. Mlikuwa wapi wakati huo? Hizo tofauti zinakuja sasa hivi? Si nyinyi mliokuwa hata mkipinga elimu ya mabinti hawa? Hamkusema kwamba kuwapeleka shule ni kufisidi rasilimali? Leo sasa mnamwona mwanangu ametononoka si haba na kuwa Mungu amemfungulia milango ya heri, ndio mnamthamini?" Kangata akaiambia jamaa yake.

Hatimaye ukoo haukuwa na budi kukubali muungano huu, muungano ambao uliyeyusha chuki kati ya nasaba hizi mbili. Ikawa watu hawawezi kuamini kuwa hizi ni zile koo ambazo hazingeweza kupikika katika chungu kimoja!

Ya Akelo Kiriri–Kaango hayajulikani. Baada ya kukamilisha masomo yake ya kidato cha nne inasemekana alisalitika kimapenzi na dereva wa malori yanayosafirisha bidhaa hadi Zambia. Dereva huyu kwa jina Kaango alimwoa, akamjengea

nyumba katika gatuzi la Mbuyuni. Tetesi zinasema kuwa Kaango na Akelo walipata watoto wawili. Mmoja kwa jina Ngaire na mwingine Mumbi. Hakuna ajuaye walikopelekwa na misukosuko ya miaka mitano iliyopita. Akelo mwenyewe hakuwa na mazoea ya kuwaambia ndugu zake kuhusu maisha yake. Mama yake alizoea kusema, "Akelo amechukua tabia za bibi mzaa baba. Kiumbe huyu alipenda kujificha, ati mama amemkasirisha! Baba angeiamrisha familia nzima kutamba kijijini kote kumtafuta. Kumbe muda huo wote ajuza mwenyewe amejificha nyuma ya ghala la mahindi!"

Lunga Kiriri-Kangata ndiye anayeishi katika milki ya marehemu babake katika Msitu wa Mamba. Lunga Kiriri-Kangata amesomea kilimo. Awali alikuwa ameajiriwa kama afisa wa kilimo nyanjani. Ndiye aliyekuwa akiwaelimisha raia kuhusu mbinu bora za kilimo. Ungemsikia marehemu babu yangu, Mungu amlaze pema peponi, akisema, "Afisa wa *ndilikasa* (hii ndiyo lafudhi ya kwa akina babu ya *agriculture* au zaraa) amesema tusilime karibu na mito, tuchimbe mitaro kuzuia mmomonyoko wa udongo, tupande miti inayostahimili ukame ..." Na kwa kweli Lunga Kiriri-Kangata alikuwa amirijeshi wa uhifadhi wa mazingira. Hata tukiwa shuleni, ndiye aliyekuwa mwasisi wa Chama cha Watunza Mazingira Wasio na Mipaka. Siku hizo akikiita kwa lafudhi ya lugha yake ya kwanza *Environmental Conservatists Without Boarders*. Kila Ijumaa wakati wa gwaride ungemsikia akituhutubia, kwa mhemko:

Mkuu wa shule, walimu na wananafunzi wenzangu, suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumeona jinsi misitu ilivyovamiwa na viongozi wenye mate ya fisi. Nasikia baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali za umma

wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kuwapoka makazi yao. Maelfu ya maekari ya misitu yamefyekwa na kujengwa viwanda. Badala ya miambakofi na miti mingine inayosafisha hewa, michai imetwaa nafasi yake. Wanaohusika na matendo haya wanapoulizwa hudai kuwa michai si adui wa mazingira! Wengine wanasema kwamba misitu haina budi kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula, kwani jamii sharti ijitosheleze kwa chakula. La kuhuzunisha ni kwamba hawa hawa wanaosema hivyo ndio wanaokita majengo ya kifahari katika sehemu ambazo zinastahili kutengewa upanzi wa chakula! Wengine wamediriki kunyakua hata madhabahu kwenye Mlima wa Nasibu ili kujenga hoteli kubwa za kitalii. Wazee wetu hawana hata pahali pa kuchomea kafara! Tunakata miti bila kupanda mingine. Tazameni shuleni humu! Hata mabustani ya maua tunashindwa kuyastawisha! Tukiendelea hivyo, bila shaka sehemu yetu itazidi kuwa jangwa!

"Lunga, huishi kunishangaza," angejisemea Kimondo, mwanafunzi mwenzake Lunga, "mtu anayekusikiliza atadhani kwamba umekulia katika mazingira sawa na sisi wanyonge ambao uwepo wetu unaamuliwa na matajiri. Inashangaza kwamba huwazii kwamba hata pale ambapo baba yako amelowelea palikuwa msitu tu, tajiri wake akapabadilisha. Baba yako hasa ndiye anayeliendeleza shamba lenyewe. Wewe hujui kwamba umaskini unaweza kuupujua utu wa mtu, akatenda hata asiyoyakusudia kutenda. Na kweli huwezi kujua kwani, tangu hapo hujawahi kula mate, ukalala bila kupata lepe la usingizi kutokana na mng'ato wa njaa, na huku baba yako anavuna kahawa katika shamba kubwa la Mzungu. Baba mtu anakuhadithia kila siku jinsi mwenye shamba

anavyopata mamilioni ya fedha. Unapomuuliza baba kwa nini hata hamudu kuwanunulia sare mpya za shule anasema, 'Mwanangu, ujira wenyewe ndio huo, ila tunajitahidi.' Mwenzangu Lunga, bila shaka hujawahi kuamka asubuhi, unakeng'etwa na tumbo; homa ya matumbo imekuandama. Mwalimu anapokuandikia barua kwenda kutibiwa katika kituo cha afya kilichoko ndani ya kijiji ambacho mwenye kahawa amewajengea wafanyakazi, muuguzi anakishika kilimbili chako na kukupeleka kwa daktari. Daktari, Mwafrika mwenzako, anakukazia macho na kumwambia muuguzi, *'His father is a casual labourer. We cannot treat him. The company does not have any medical scheme for casual labourers.'* Muuguzi anayasikiliza maneno haya, na baadaye kuwa mkalimani wako, anadhani huelewi lugha hii. Sijui, Lunga, kama umewahi kujiuliza kama huduma bora za afya zinastahili tu kwa watoto wa walio nacho. Je, mwana wa kibarua, ambaye ndiye anayezalisha mali ya kuwezesha kuwepo kwa hiyo *medical scheme*, hastahili kupewa huduma ya matibabu? Naona umekuwa ukuni kwenye uchaga, unaoucheka ulio motoni," Kimondo angekamilisha uzungumzi wake na kujipangusa matone ya jasho yaliyokuwa yametunga kipajini mwake.

Sasa Lunga ni mkulima stadi. Marafiki zake wamempa jina la msimbo *Mkulima Namba Wani.* Ametononokea si haba katika msitu huu. Hadiriki kuwaza kwamba msitu huu unastahili kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye! Kabla ya jaala kumleta hapa, Lunga aliuona mstakabali wa maisha yake ukiporomoka. Alikuwa ameipoteza kazi yake. Akiwa mkurugenzi wa kampuni ya Maghala ya Fanaka, alipinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ambayo yalikuwa

yameagizwa kutoka ughaibuni. Mahindi hayo, licha ya kuwa na rangi ya njano, yalihofiwa kuwa yameharibika. Huko ughaibuni yalikotolewa yalisemekana kuwa hatari kwa usalama hata wa panya! Wataalamu wa masuala ya lishe, baada ya kushinikizwa na vigogo wenye shehena za mahindi haya, walitia sahihi kuidhinisha uuzaji wa mahindi haya. Lunga alipopinga uuzaji wa mahindi haya aliambiwa, "Sikiliza bwana, mhitaji siku zote ni mtumwa, tangu lini maskini akabagua? Mahindi haya ni kama tumepewa bure kupunguzia makali ya kutojitosheleza kwa chakula ambako kunaing'ata nchi hii. Kuyakataa mahindi haya ni kama kuidhinisha kifo cha mamilioni ya raia ambao hawamudu kujinunulia hata kibaba cha unga."

Rai ya wakubwa hata hivyo haikumnyamazisha Lunga. Aliendelea kulipinga tendo hili kwa jino na ukucha. Alimkabili mkurugenzi wa kitengo cha uhakikishaji wa viwango na ubora wa bidhaa na kumwambia,

"Ni kweli kwamba nchi hii inakabiliwa na tatizo la kuwahakikishia raia wake kujitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, hali yetu ya uhitaji haipaswi kutumiwa kama kibali cha matajiri kufurisha masoko yetu kwa bidhaa duni. Kinachohitajika ni kuwahimiza raia kutumia ardhi kwa njia endelevu. Wasisitiziwe umuhimu wa kuacha kujenga katika ardhi ambayo inastahili kutumiwa kwa kilimo, wala si kuwauzia sumu kwa bei rahisi."

Lunga alijua kwamba msimamo wake huu ungempalia makaa. Lakini alihiari kuipoteza riziki yake ili kuyaokoa maisha ya wanyonge wasio na hatia. Mwezi mmoja baadaye, akiwa ofisini mwake, akili yake kaizamisha kwenye shughuli ya kuibua mikakati ya kukabiliana na janga la njaa nchini,

Lunga alipokea barua ya kumfuta kazi. Barua hii ilikuwa fupi lakini yenye kukata kama sime.

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Kitaifa ya Uhifadhi wa Nafaka,
S.L.P. 4115-0340,
Gharika.

Mei 2, 2009

Bwana Lunga,

KUH: KUSTAAFISHWA

Kutokana na gharama ya uzalishaji mali ambayo inaendelea kupanda kila uchao, shirika hili limekumbwa na changamoto kubwa ya kifedha. Halmashauri inayosimamia shirika hili imeamua kupunguza idadi ya wafanyakazi katika ngazi za juu, kama hatua mojawapo ya kudhibiti gharama ya uzalishaji.

Shirika hili linasikitika kukuarifu kuwa wewe ni mmoja wa walioathirika na kwamba umeachishwa kazi kuanzia tarehe 31 Julai mwaka huu.

Tunakushukuru kwa kuwajibika kwako kazini, pamoja na mchango wako katika kuliendeleza shirika hili. Twakutakia kila la heri katika shughuli zako za kitaaluma.

Wako mwaminifu,

Jkalima

Bwana Kalima
Mwenyekiti
Halmashauri ya Kitaifa ya Uhifadhi wa Nafaka.

Lunga aliisoma barua hii mara mbili. Alishangazwa na ukosefu wa fadhila wa waajiri wake. Licha ya kujitolea kwake usiku na mchana kulijenga shirika hili, anasindikizwa kwenda nyumbani kwa mistari michache ya maandishi! Kweli fadhila ya punda daima ni mashuzi! Hata hivyo, hakujuta kwani alijua alikuwa ametenda wajibu wake. Alipokuja katika Msitu wa Mamba, alikuwa amezuumu kumhamisha baba yake, amtafutie makao kwingine kwani, kulingana naye, haikuhalisi binadamu kuwapoka wanyama makazi yao; ni dhuluma. Alizoea kusema, "Hapa ndipo Edeni pao. Tukipanyakua tutawazongomezea wapi?"

Aliyoazimia Lunga siyo aliyoyatenda. Mara tu macho yake yalipokumbana ana kwa ana na zao la mahindi lililotamalaki kwa heba katika ekari thelathini na tano ambazo zilikuwa milki ya baba yake, moyo wa Lunga ulitwaa uchu ambao uliulemaza uadilifu wake. Tamaa ya kulima maekari na maekari zaidi ilimkumbatia, akatwaa mundu, akakata miti zaidi. Hakukumbuka kupanda mingine. Alipanda mimea zaidi kwa ajili ya kuuza; si pareto, si mboga, vyote vilinawiri katika mashamba yake. Ule wito wake wa kuihifadhi misitu kwa manufaa ya vizazi vijavyo ukafia kwenye vilindi vya tamaa yake. Hakuwa na chochote baada ya kupigwa kalamu na kufukuzwa kwenye nyumba ya kampuni. Sasa anamiliki, si nyumba tu, bali pia na mashamba makubwa. Anafuga kuku, bata, mbuzi na ng'ombe. Anaweza kuwaajri watu kufanya kazi katika mashamba yake. Sasa Lunga ni Lunga Kiriri. Jina la Kangata limeanza kujifia. Unaweza kumtia kwenye safu ya Kiriri ambaye alikuwa mwajiri wa babake.

Unapomwuliza ilikofia ile jadhba yake ya kupigania uhifadhi wa misitu hukwambia, "Ndugu, kunako matanga

kumekufa mtu! Ulimwengu umenifunza kutumia fursa niliyo nayo kuyaboresha maisha yangu. Mungu mwenyewe alitupa ulimwengu tuutawale, sio ututawale. Rasilimali tuitumie wala si kuifumbika ardhini kama kiazi kitamu. Tusije tukawa sawa na yule mtumishi kwenye kitabu kitakatifu ambaye alichimbia talanta chini badala ya kuizalisha! Alihofia uchoyo wa bwana mwenye mali lakini alikuja kuhasirika yeye mwenyewe. Tamba na ulimwengu ndugu yangu, utajua. Nilipojaribu kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika. Hata niliokuwa nikiwatetea hakuna aliyenyoosha dole kuniauni! Wote walijinyamazia kana kwamba sikuwakinga dhidi ya kifo kilichowakodolea macho! Wapo waliosema kuwa wangu ulikuwa msiba wa kujitakia!"

Mashamba ya Lunga na wenzake yaliendelea kutuna kwa mazao, jamii ya Msitu wa Mamba nayo ikaendelea kuwanda, na kama kaida ya maumbile, tofauti za kitabaka zikazidi kudhihirika. Kundi la kwanza la 'wakimbizi' lilipofika hapa—lile la akina Ridhaa, Kaizari na Kangata—hamkuwa na tofauti kubwa. Jamaa hawa walikuwa wamelazimika kuja hapa. Walikuwa wahitaji, wote, wakapigania vyakula vya misaada, wakala majani mwitu na vingine, pamoja. Sasa jamii hii imekua na kutwaa uchangamano, uchangamano wa mtu kukumbuka kuwa yeye alitokana na ukoo mtukufu na jirani yake alikopolewa na ukoo wa walalahoi. Mpito wa wakati ulivyaza matajiri kama Lunga ambaye hakufanya ajizi kuwakumbusha wenzake kuwa alichimbuka kwenye jadi ya kifahari ya Kiriri. Kulikuwa pia na maskini ambao kupata kwao ahueni kulitegema utashi wa matajiri. Dau la mnyonge tangu lini likaenda joshi? Polepole uhasama ulianza kutishia kuisambaratisha jamii ya Msitu wa Mamba. Viongozi, kwa

kuhofia kovu kuwa jeraha, walianza kampeni za kuwaelimisha raia kuhusu umuhimu wa kuishi kwa amani licha ya tofauti zao za kiusuli. Hata hivyo, hizi zilikuwa juhudi za mfa maji. Awamu ya kwanza ya vita vya wenyewe kwa wenyewe ilianza; walinda usalama walitumwa kukabiliana na mgogoro huo. Busara yao ya kuwasaka wahalifu kwa mitutu ya bunduki iliwaacha wengi wakiwa wafu, watoto wakabaki wanawakiwa.

Kisa hiki kiliyafungua macho ya viongozi, wakatanabahi kuwa kwa kweli wakazi hawa walikuwa wakiishi hapa kiharamu. Vyombo vya habari havikukawia kutoa wito kwa chama tawala kuwatafutia watu hawa mahali kwingine, vidonda vya zamani vikaanza kutoja damu. Watu hawakuchelea kukumbuka jinsi walivyopoteza mali, aila zao, na hata maazimio yao katika maisha, wakalazimika kuishi kama wanyama. Na leo hii wakati wamejiinua kwa jasho lao wenyewe, sasa imekuwa wanaishi katika ardhi ya wenyewe! Itakuwaje ardhi iwe ya wenyewe na wao wasihesabiwe miongoni mwa hao wenyewe? Ama ni ile hali ya washika dau na wenye dau? Walipokuja hapa ardhi hiyo haikuwa bikira, wakautifua udongo wakalima? Kwani kuna walioumbiwa kumiliki na wengine kukosa? Na ikiwa kweli wao si wamiliki wa ardhi hii, kwa nini wakapewa hatimiliki? Ama nazo hizo ni bandia? Walihisi jinsi mtu ahisivyo wakati anapochochwa jicho na mpinzani wake katika kinyang'anyiro cha miereka. Wengine walithubutu kufanya maandamano dhidi ya uamuzi huu. Hata hivyo walikuwa wapiga mbizi nchi kavu, maskini wakaishia kuumiza nyuso zao! Maandamano yao yalisalimiana na risasi na vitoza machozi. Wengi wao walikufa katika misiba iliyorejelewa kuwa ya kujitakia. Wachache

walifanikiwa kurudi kwao katika awamu ya pili ya *Operesheni Rudi Kanaani*. Wengine kama Lunga, ambaye tangu hapo hakujua kitovu chake hasa, walitimuliwa pamoja na familia zao. Hawakujua walikokuwa wakipelekwa hadi baada ya miezi mitatu, Lunga alipogundua kuwa amerudishwa kwenye Mlima wa Simba ambako inaaminiwa mababu zake walikuwa wamehamia kutoka Kaoleni, siku za biashara ya watumwa. Lunga haishi kushangaa kwa nini marehemu baba yake hakuwahi kumtajia haya! Ama kulowelea kwa Bwana Kiriri kulimfanya Kangata kujinasibisha na kujitambulisha naye kiasi cha kujihesabu mmoja na Kiriri mpaka akakifisha kitovu chake?

Msitu wa Mamba sasa ulibaki tasa. Hakuna anayejua yalikokwenda mahindi ya akina Lunga. Mapaa ya majumba, ambayo taratibu yalifunikwa na miti iliyosongamana, yaligeuka kuwa rangi ya hudhurungi. Mto uliokuwa hapo karibu, ambao ulikuwa umeanza kukauka, sasa ulianza kutiririsha maji. Jambo la kushangaza ni kwamba, ingawa tulitangaziwa kuwa msitu huu ni marufuku kwa binadamu, usiku wa manane husikika milio ya malori na matrekta yakibeba shehena za mbao, makaa na mahindi! Haijulikani ni wanyama gani wanaotekeleza haya, lakini hata ni mazoea ya msitu huu kufuka moshi mara kwa mara. Watu husema kwamba huenda hawa ni wachinja kafara ilhali wengine husema pengine ni *bushfire!*

Sura ya Sita

"Umulkheri! Rudi darasani!" alitamka Mwalimu Dhahabu kwa upole na ucheshi wake wa kawaida. Umulkheri aliyaambia macho yake yatoke huko mbali yalikokuwa yametanga, akayarudisha darasani, yakatazamana na ya Mwalimu Dhahabu bila yeye Umulkheri kumwona mwalimu mwenyewe. Tangu Umu—kama Umulkheri alivyoitwa kwa kifupi—ajiunge na shule hii katika kidato cha pili, anajihisi kama samaki aliyetiwa kwenye dema. Haya ni mazingira mageni kwake na hakuja hapa kwa hiari. Baridi ya mahali hapa inamsinya, si kama kwao ambako kulikuwa na hari.

"Kwetu? Kwani mimi nina kwetu tena?" alizoea kujisuta Umu.

Ni kweli kuwa Umu alikuwa na kwao, ila sasa hana. Amebaki kuishi kwa hisani ya mkuu wa shule ya Tangamano, ambaye, kwa ushauri wa Wizara ya Elimu, alimsajili Umu na wengine watano shuleni humu.

Umu alikuwa mwana wa pili wa Bwana Lunga Kiriri-Kangata. Uongozi ulipoamua kuwahamisha hadi Mlima wa Simba, yeye ndio alikuwa anajiunga na kidato cha kwanza. Kuhamia Mlima wa Simba hakukumkalia vyema Lunga. Moyo wake ulikataa katakata kuyakubali mazingira na hali

hii mpya. Alijiona kama mfa maji ambaye anakabiliwa na mtutumo wa mawimbi ya misiba, mmoja baada ya mwingine. Alikumbuka kazi yake. Yeye alikuwa mtu mwenye chake. Alikuwa mwenye heba zama zile alizokuwa kinara wa shirika. Mlimwengu aliyang'wafua haya kutoka kiganjani mwake jinsi mbwa ang'wafuavyo mnofu wa nyama kutoka kwenye mfupa, akamtoa kashata mdomoni, akamfuta kazi! Alikumbuka mali yake ambayo aliichuma kwa viganja vyake katika Msitu wa Mamba. Sasa ameipoteza. Ameyapoteza maisha yake, amewapoteza ndugu na marafiki zake. Wanawe walisomea katika shule za kifahari, sasa fidia aliyopewa na serikali haitoshi hata kuwapeleka katika shule za watu wa kima wastani.

Mkewe Lunga, Naomi, naye ni miongoni mwa wale ahali ambao hata wanapoolewa hawasahau uhusiano wao na nasaba zao. Hawatulii kuyapalilia maisha ya unyumba. Daima hujiona wageni katika familia za wakwe zao. Naomi alikuwa haachi kufanya nongwa kwa kutolewa kwenye ulinzi wa aila yake na kupelekwa huko mbali na wazazi wake. Nyumba ambayo familia ya Lunga ilijengewa na serikali, Naomi aliiona kutokuwa kufu yake. Siku moja Naomi alimwambia Lunga jinsi Mzungu mmoja, kwa jina Billy, huaminika kuwa aliambiwa na mchumba wake Sally! Sijui kama umewahi kuisoma au kusimuliwa hadithi hii ambayo, kwa sababu ya kupitishwa kwenye vinywa vya mafanani wengi, imesarifiwa na kuzaliwa upya.

Hadithi inayosimuliwa hapa ni tofauti na nilivyoisoma kwenye riwaya fulani. Billy, inasemekana, alikuwa mlowezi nchini humu. Baada ya kufariki kwa wazazi wake, Billy alijenga jumba la kifahari, kisha, wasemao husema, kama Mungu alivyoona mwanzoni mwa ulimwengu, Billy naye

akaona si vyema mwanamume kuishi peke yake. Billy akawaza na kuwazua. Mwishowe aliamua kurudi kwao ughaibuni na kumtafuta kipusa. Billy aliona kwamba hakuweza kupata mke stahiki yake kwenye bara la giza. Basi huko kwao alichumbiana na Sally, akamleta nchini humu. Alimpeleka kwa bashasha kuu kumwonyesha kasri ambalo wangeishi baada ya kufunga nikahi.

"Darling, this will be your home soon after our honeymoon," alisikika muungwana huyu akisema. Sally aliinua kipaji chake, akamtazama Mzungu kwa jicho la hasidi na kusema,

"This is a nest. I cannot live here, not now, not ever." Kipusa akawa ameliona jumba la mpenziwe kama tundu la makinda, akachukua virago na kurudi kwao ughaibuni. Hakujali kuwa amemwacha mwenzake akitapatapa kwa maumivu ya kusalitiwa. Aliutia moyo wa Billy ufa ambao ulivuja hisia za unyonge, chuki na kinyongo. Wambea husema kuwa Billy alichukia wanawake kuanzia siku hiyo. Jumba hilo, inasemekana na waliokuwapo, kuwa limetolewa kama kivutia watalii!

Naomi, sawa na kipusa huyu wa Kizungu, alimwambia Lunga, "Haya siyo niliyotaka. Hivi sivyo nilivyotaka kuwakuza Umu na wanuna wake." Huu uliishia kuwa mkarara katika ushairi wa makiwa kwa Lunga kila mara hadi pale lile alilohofia Lunga lilipotokea. Lunga aliamshwa asubuhi moja na mlio wa rununu yake kuashiria kuwapo kwa ujumbe mfupi. Alifurukuta, akatupa mkono wake upande wa mkewe. Badala ya mkono kugusa kiwiliwili, uligusa hewa! Moyo wake ulianza kupiga mithili ya ngoma alipoanza kuusoma ujumbe mfupi ambao uliashiria mwanzo wa mkondo mpya wa maisha ya familia yake.

Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao.

Kwaheri.

Naomi

Lunga alihisi kama aliyechomwa kwa joto la tanuri. Hili ni pigo la tatu kutoka kwa walimwengu. Tofauti ni kwamba hili linauma na kudhalilisha zaidi kwani Lunga alijisabilia kwa hali na mali kumridhia na kumpendeza mkewe. Kwamba analilipa penzi lake kwa kumwachia adha za malezi ni jambo ambalo Lunga hakuweza kulistahimili. Alijaribu kubofya simu yake kumjibu mkewe kumwambia, kama alivyosema mwimbaji mmoja wa rara nafsi, 'Umeteua kipindi kinachofaa kuniacha, Naomi,' lakini mkono wake ulimkataza kujidhalilisha zaidi. Alimeza funda chungu la mate na kuamua kusalimu amri ya usaliti wa Naomi.

Mwaka mmoja wa kwanza ulikuwa mgumu mno. Japo majirani walimsaidia kama ndugu, Lunga ilibidi kuwa baba na mama wa watoto wake, na hilo usilione kuwa jepesi. Katika hali hii, Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao.

Asubuhi moja Umu aliamka na kujipata yu pweke nyumbani mwao. Ndugu zake wawili, Dick na Mwaliko, walikuwa wametoweka! Alijaribu kumwita kijakazi Sauna kumjuza haya lakini alisalimiwa na cheko la mwangwi wa sauti yake katika sebule iliyokuwa imegeuka kuwa kubwa kama ukumbi. Umu aliachama. Hakujua awatafute wapi

ndugu zake wakembe. Dick alikuwa katika darasa la saba naye Mwaliko alikuwa katika darasa la kwanza. Taswira ya visa vya watoto waliotekwa nyara ilimjia akilini mwake, ikakifanya kichwa chake kuwanga kwa maumivu. Alijaribu kuuliziaulizia kutoka kwa majirani asipate wa kumwauni. Mwishowe alipiga moyo konde akaenda kupiga ripoti katika kituo cha polisi.

"Mimi ni Umulkheri Lunga. Ninasomea Shule ya Upili ya Mtende. Nimekuja kutoa taarifa kuhusu kupotea kwa ndugu zangu Dick na Mwaliko," alisema Umu, huku amemkazia macho askari wa zamu kwa kuhofia kutosikika.

"Unasema watoto walipotea? Unajuaje walipotea?" aliuliza askari wa zamu.

"Kwa sababu hawako nyumbani. Nimewatafuta mchana kutwa. Hawapo wala hawajaonekana na majirani," Umu alieleza.

"Kutoonekana hakumaanishi wamepotea," alidakiza askari mwingine kwa ujeuri, "kwanza walikuwa wamevaa vipi walipoondoka nyumbani? Walibeba nini? Walikwambia wanaenda wapi? Kwa nini watoto wenyewe hawajaandikisha kupotea kwao kwenye *OB?*" Maswali ya askari yule yalifuatana moja baada ya lingine.

"Sasa nitajuaje walichokuwa wamevalia nami sikuwaona? Mtu hukwambia anapotoroka au kutoroshwa? Na hiyo *OB* ni nini?" alijisaili Umu kimoyomoyo, kisha, "Sijui afande," akajibu.

"Unasema pia kuwa kijakazi wenu hayupo?" akauliza askari.

"Ndio, afande," akajibu Umu.

"Na hakukujuza anakokwenda?" aliongezea askari yule.

"La!" Umu alijibu huku uso wake ukidhihirisha kuudhika.

"Jina la huyo kijakazi?" akauliza askari yule wa kwanza.

"Sauna, Auntie Sauna. Lakini Mwaliko anamwita Mummy," Umu alijibu.

"Basi wewe rudi nyumbani. Watoto siku hizi wana mazoea ya kutekwa nyara na vijakazi wao. Tutachunguza haya. Tukiwapata tutawajuza wazazi wako," yule afisa aliyemuuliza swali la kwanza akamwambia.

Umu alitaka kudakiza kuwa hana wazazi lakini alijiasa. Hakukuwa na haja ya kuonyesha donda hili kwa viumbe ambao hawana imani. Alijizoazoa na kujiendea zake nyumbani.

Maisha ya Umu sasa yalichukua mkondo mpya. Siku ile baada ya kuwapigia polisi ripoti, ilibainika kuwa wanuna wake walikuwa wametekwa nyara na Sauna. Haya ndiyo yaliyokuwa mazoea ya Sauna. Sauna alikuwa chui ambaye hakupigwa na mshipa kujifanya mwema kwa waajiri wake ili aaminiwe, naye apate fursa ya kuwaiba watoto na kuwapeleka kwa bibi mmoja ambaye aliwatumia katika biashara ya nipe nikupe, na katika ulanguzi wa dawa za kulevya.

Machozi ya uchungu yalimtiririka Umu. Hakuamini kuwa ndugu zake wadogo sasa walikuwa mali ya mtu, watumiwe kama vitega uchumi na mjasiriamali ambaye aliwatumia binadamu kama malighafi!

"Auntie Sauna! Kumbe ile imani na uchangamfu wako na ahadi ya kututunza baada ya kifo cha baba ilikuwa siasa ya kutuondoa hofu, tukuamini na kukupa fursa ya kututenda!" alijisemea Umu. Alimlaani mama yake ambaye aliwatelekeza kwa ubinafsi na ukatili mkuu. "Kipi kinachompa mama

uyabisi wa moyo hata akawaacha wanawe?" alijiuliza Umu. Fikira za kila aina zilijitoma akilini mwake, zikataka kumwangusha. Alipiga darubini kwenye mustakabali wake, akajiona akikabiliwa na tatizo kama la ndugu zake. Alijiona akichukuliwa danadana na majanaume katika madanguro mbalimbali. Wazo hili lilimtia kigegezi, malaika yakamsimama na mwili kumsisimka. Katika hali hii, alifikia uamuzi wa mkataa, kwamba hapo hapamweki tena, atatanga na njia aone jaala itakapomfikisha. "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu. Nitatafuta haki ilikojificha," alisema Umu.

Asubuhi moja mbichi ilimpata Umu kwenye kituo cha garimoshi, akiwa amewasili kutoka Mlima wa Simba, yu katikati mwa jiji. Baridi ya vuli ilikuwa inamtafuna. Mtafuno huu ulivotana na mkeketo wa njaa kwenye uchango wake. Woga mkubwa ulimkumbatia kwa kutojua alikokuwa. Ingawa alikuwa ameishi katika Jiji la Karaha siku zile baba yake akiwa mkurugenzi, hakuwahi kutembea jijini peke yake. Kila alipokuja jijini Jumapili alikuwa kaandamana na wazazi wake kwa ibada. Siku nyingine aliandamana na shangazi yake kununua bidhaa kama vile nguo za shangazi, na mara zote hizo walikuwa wakipelekwa na dereva. Sasa huu ni mji mpya kwake. Ametengana nao kwa muda tangu zama za kuhawilia kwao Msitu wa Mamba.

Umu anapolitazama jiji analiona kama bahari isiyo na kikomo. Hata hivyo, Umu yu tayari kuanza maisha upya katika jiji hili. Hajui vipi, lakini moyoni ametia nia, na penye nia bila shaka njia hupatikana. Ataanzia hapa kuyabadilisha maisha yake ya dhiki kuwa ya heri. Atatafuta msaada kwa mhisani

yeyote. Huenda akapata pa kuishi na hata kuyaendelezea masomo yake! Huenda hata akawapata ndugu zake! Fikira za ndugu zake zilimfanya kuzizima na kuishiwa na nguvu.

"Nitawapata wapi hawa maskini na hali sijasikia hata fununu yoyote kuwahusu? Lakini Mungu si Athumani, huenda sadfa ikatukutanisha," moyo wa Umu ulimkumbusha na kumwelekeza kuchukua hatua kutoka mahali ambapo miguu yake dhaifu ilikuwa imejikita.

Umu alijikokota kwa hadhari, akachukua barabara iliyoelekea kushoto. Alifikia mzunguko mkubwa penye njia panda. Hatimaye alichukua barabara iliyoelekea kushoto. Alipoinua macho yake alikiona kibao kilichoandikwa *Church Road,* na mara akakumbuka ilikoelekea barabara ile. Aliwahi kupitia hapo zama za utukufu wa baba yake. Hata sasa Umu anakumbuka akiwapata ombaomba wengi walioishi hapa karibu na kanisa la Mtakatifu Fatma. Anakumbuka alivyomsihi mama yake kumpa noti ya shilingi mia moja amkabidhi mmoja wa ombaomba wale.

"Mum pliz, just a 'red'! These guys are needy!" alimwambia mamake.

Mama mtu alijibu kwa mabezo, *"These are pretenders. They have been sent by their stinking rich relatives. I can't give them even a penny."*

Hata hivyo, Umu alishikilia chuni apewe pesa hizo, hadi mama alipotoa shilingi ishirini na kumtupia Umu. Umu alitia mkono ndani ya mfuko wa dangirizi yake, akatoa shilingi mia mbili alizokuwa amedunduliza kutokana na mapeni aliyokuwa akipewa na baba yake kama masurufu, akampa mvulana mmoja ombaomba.

"*Poa* sana *sistee*, we ni *mnoma*. Siku moja *nitakuhelp* hata mimi," akajibu yule mvulana.

"*Eazie*, nenda ukanunue *loaf*. *Na promise* hutanunua *glue pliz, pliz bratha*," Umu alimwambia huku akitabasamu.

"*Promise*," alimjibu kijana yule huku akikenua vijino dhaifu vilivyotwaa rangi ya hudhurungi kwa ugaga.

Leo Umu anashangaa iwapo bahati itamvutia usaidizi hata kutoka kwa yule maskini wa Mungu. Moyoni anasema kwamba hata akampa jamvi la kuuweka ubavu wake usiku kwenye mitaa, atashukuru tu.

Barabara ilimwongoza hadi kwenye mkahawa mkubwa mkabala mwa kanisa. Nje ya mkahawa huo mlikuwa na kundi la vijana wa mtaani, kubwa, kama wingu la nzige. Wengi wao walikuwa na macho mekundu ya kutisha, wengine wameshika gundi, wengine vipande vya mikate, wengine wamebeba vifurushi vya bidhaa za kubadilisha kwa nyingine almaarufu Mali kwa Mali, ambavyo kweli vilikuwa vimesheheni matambara yaliyokuwa yameokotwa kwenye mapipa ya viwanda vya kutengenezea nguo; yanakwenda kuwa ganda la muwa kwa chungu. Vijana walikuwa wakivitangaza vitambara hivi kwa wenzao wakitaka kuvibadilisha kwa vipande vya mkate. Umu aliyaangaza macho yake kuona kama atampata yule rafiki ambaye yeye Umu alimfaa kwa jua la kiangazi. Anatamani sasa amfae kwa mvua ya masika ambayo tayari imeanza kumpiga. Hakumpata, wala hakuona aliyekaribia kufanana naye. Alikata tamaa. Laiti angalijua angalimuuliza jina lake! Labda hata hawa wenzake wanamjua. Aliamua kuendelea na safari yake. Huenda atampata pale kanisani.

Kabla hajatembea hatua chache kutoka pale, alisikia sauti ikiita,

"Kipusa!"

Alipogeuka alipata ni yule kijana, kazaliwa upya! Nadhifu! Meno meupe!

"Unanikumbuka? Mimi ninaitwa Hazina. Ndimi yule ombaomba uliyeonyesha imani siku zile. Miaka mingi imepita lakini mtu hamsahau mhisani wake. Serikali iliniokoa kutokana na kinamasi cha uvutaji gundi na matumizi ya mihadarati. Nilipelekwa shuleni nikasoma, nina elimu japo akali. Tulijengewa makao ambapo mimi na wenzangu tunaendelea kusaidiwa na kupewa mbinu za kukabiliana na changamoto za maisha. Wengi wetu ni maseremala, waashi na mafundi wa juakali. Mimi nilibahatika kujifunza upishi na huduma za hotelini katika chuo kimojawapo. Hivi sasa ninafanya kazi kama mhudumu katika hoteli hii. Njoo unywe chai," Hazina alieleza.

Umu alimtazama Hazina, kaduwaa.

"Huyu ambaye mama alimwona kuwa gae, kumbe sasa ndiye chombo cha kunivusha bahari hii ya dhiki?" alijisemea.

Alimfuata Hazina hadi hotelini ambako alikula shibe yake. Alimsimulia Hazina mkasa wake huku mito ya machozi ikichimbuka kwenye chemchemi na kuwatiririka wote wawili. Hazina akimwonea imani Umu kwa kuharibikiwa na maisha katika kipindi ambapo alihitaji hifadhi ya wazazi. Umu, machozi yake kwa upande mwingine, yalikuwa mchanganyiko wa furaha na majonzi. Furaha kwa kuona kuwa rafiki yake huyu amefaulu kujitoa katika hali ya utegemezi.

Huzuni kwa sababu anahisi kuwa ndugu zake wawili huenda ndio waliochukua nafasi ya Hazina katika mitaa ya miji. Hazina alimwahidi Umu kuwa atamsaidia. Alimpeleka moja kwa moja hadi kwenye makao yao, akamjulisha kwa mama aliyesimamia makao hayo. Mama huyu aliitwa Julida.

Julida alimgusa Umulkheri begani na kumwambia,

"Usijali mwanangu. Hapa patakuwa penu kwa muda. Tutawasiliana na Idara ya Watoto kuhusu suala la ndugu zako. Watatafutwa na watapatikana. Serikali imezindua hazina ya kuyafadhili masomo ya watoto kama wewe. Wizara ya Elimu itakupa uhamisho katika shule ya hapa karibu."

Mwezi mmoja baadaye, Umu alijiunga na Shule ya Tangamano, akaingia katika kidato cha pili ambako alijipata kuwa mgeni wa pekee na bila shaka mgeni, kama alivyo kuku mgeni, hutambulika kwa urahisi. Mwalimu Dhahabu hakukawia kutambua unyonge uliokuwamo machoni mwa Umu. Hakusita pia kutaka kujua usuli wa mwana huyu kutoka kwa mwalimu msimamizi wa darasa la Umu. Mwalimu huyu aliyahadithia masaibu ya Umu, naye Bi. Dhahabu akawa haishi kumhimiza Umu kuwa jasiri kukabiliana na hali hii yake mpya. Hata hivyo, ilimwia vigumu Umu kusahau yaliyopita. Tangu lini mavi ya kale yakaacha kunuka?

"Vipi mtu utasahau ya kale na hali unaiishi hiyo kale?" aliwaza Umu kila mara mwalimu alipomkumbusha arejeshe mawazo darasani.

"Je, mtu husahau sinema za kweli anazoona maishani? Nani katika umri mdogo kama huu wangu aliyewahi kushuhudia mawi kama niliyoyashuhudia? Binadamu kumhusudu mwenzake hadi kumfutisha kazi. Mtu unamtazama jirani

yako anachinjwa bila mwombezi, majizi yakiivamia mali ya watu, nyingine inakatalia migongoni mwao! Mama mzima akiwaacha wana ... Utasahau vipi hali yako? Na hata huku kusomeshwa ni kugeni, walimu wageni, mbinu mpya za kufundisha ... walimu wanakuja darasani kila mara, nasi kwetu hatukuzoea haya?"

Umu aliendelea kuhimizwa na wenzake ayazoee maisha haya mapya.

"Una bahati sana mwenzangu," alisema Kairu siku moja, "wewe hujapitia tuliyopitia. Tulitendwa ya kutendwa. Siku hiyo tulipofurushwa kwetu kama taka tulitanga bila kujua tuendako, mama mbele sisi nyuma, mama amebeba kitindamimba ambaye baadaye alishindwa kukamilisha safari; roho yake changa ikakatikia hapohapo mgongoni mwa mama, amemezwa na njaa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu. Mama alituelekeza kando ya njia, tukaingia kichakani kiasi. Sijui alikotoa kiserema alichokitumia kuchimba kaburi lenye kina cha haja, tukaufukia mwili wa ndugu yetu huku kilio cha uchungu na jitimai kikihanikiza kote.

Baada ya kiviga hiki, mimi, mama na ndugu zangu wengine tuliendelea na safari bila kujua kipaji na kisogo cha safari yenyewe. Hatimaye nguvu zilituishia, mama akatuashiria tuketi kando ya njia, tukawa tunangojea kifo. Mara wakaja watu waliokuwa wamevaa mavazi yaliyoandikwa IDR; tukasombwa na kutiwa kambini, tumejaa kama sisimizi, watoto kwa watu wazima. Hali ilikuwa ngumu, tukawa tunalala katika kibanda kimoja na wazazi wetu, hata waliobahatika kuwa na wazazi wote wawili! Miiko ilivunjwa! Hata hivyo, tulijipa kuamini kwamba haya ndiyo yaliyokuwa majaliwa yetu, tulikuwa

wenye haja, maiti hasa, na tangu hapo maiti hachagui sanda wala jeneza. Tulivumilia, tukawa tunaishi kwa tumaini tukidhani hali itatengenea, tukitumaini kwamba tungerudi kwetu. Lakini, lo! Wanasema wajuao kuwa msitu ni mpya, ila nyani ni wale wale. Uongozi mpya haukuleta ahueni yoyote katika maisha yetu! Kilichobadilika ni kwamba tulipewa ardhi zaidi ya kujengea mabanda zaidi ili kupunguza msongamano katika mabanda ya awali! Bado tu pale pale. Nilikwenda hapo nikiwa katika darasa la sita. Sasa ni katika kidato cha pili. Tungali tunasubiri kurudishwa nyumbani! Ila sioni kama pana *nyumbani* pema zaidi ya mle kambini ambamo tunaishi bila kujali tulikotoka. Vumilia, mwenzangu. Zingatia masomo yako kwani ndiyo yatakayokuvua kutoka lindi hili la huzuni." Baada ya kusema haya Kairu alitulia kwa muda kama mtu anayevuta fikira, kisha kuendelea.

"Una bahati kupata mfadhili, mimi mzazi wangu wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki, na baada ya ule mzozo wa nani kamiliki Ziwa Kuu, biashara imepigwa na mawimbi makali. Nasikia wavuvi wa humu mwetu wanahofia kuvua huko kwa sababu wameambiwa kuwa japo ardhi ambayo ziwa limesimama ni yao, maji ya ziwa si yao! Hivyo inasemekana kuwa hawafai kuvua huko, kwamba samaki ni wa wanaoyamiliki maji! Matokeo ya mzozo huu yamekuwa masikitiko kwa familia nyingi. Samaki wamekuwa adimu sokoni na bila shaka bei yake inaweza kutabirika. Kwa mtu maskini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzishia biashara nyingine, maisha yamekuwa magumu zaidi. Hata karo yangu imebidi amlilie mwalimu mkuu amruhusu alipe kidogokidogo hadi mwisho wa mwaka. Mara mojamoja

nimewahi kumwuliza mama kwa nini asimwombe baba, ambaye nasikia ni mwenye chake na lake, anilipie karo. Hata hivyo mama huwa hanijibu, anachonipa ni mtazamo unaouliza swali, 'Nitamwambia vipi mtu mwenye familia yake kumkimu mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa?' Kila mara hujiuliza ikiwa watoto huwa na hadhi tofauti, nje au ndani ya ndoa. *Count your blessings,* Umu."

Wakati huu wote Umu alikuwa katega sikio ndi! Anaitia hali ya Kairu kwenye mizani, anaelekea kuuona msiba wake kuwa mwepesi sasa.

"Baada ya kurudishwa nyumbani kutoka Msitu wa Mamba, baba yangu, Mzee Kaizari, aliweza kuyajenga maisha yetu upya. Alijenga nyumba kufu yetu palepale penye lile ganjo," alihadithia Mwanaheri baada ya Kairu kumaliza kisa chake. "Mimi na ndugu Lime tulirudi shuleni mlemle kijijini mwetu tu. Haikuwa vigumu kuyazoea maisha tena kwani wanafunzi wenzetu walitupenda mno. Lime alikuwa hodari katika michezo ya kuigiza—ile ya kitoto. Alikuwa mcheshi mno, kwa hivyo kutokuwapo kwake shuleni kuliwafanya watoto kumpeza. Mimi sikuwa hodari sana katika michezo lakini nilikuwa najaribu kupalilia kipawa changu cha kughani mashairi mepesi. Majirani nao walimsaidia baba kukabiliana na hali yake mpya. Ingawa mara nyingi baba alikuwa na hofu kuwa tungeshambuliwa tena, majirani walimhakikishia kuwa hawangeruhusu jambo lolote kuusambaratisha tena udugu baina yao. Hali ya utulivu ilitawala tena. Hata hivyo, walisema wasemao kwamba pang'okapo jino pana wasiwasi. Uhusiano kati ya marehemu mama yangu na mavyaa yake ulikuwa umeingia ufa. Nasikia kwamba mama mkwe daima

humwonea gere mkaza mwanawe, kwa kumwona kama aliyekuja kumbwakura mwanawe. Hali hii ilizidishwa na tofauti ya kikabila kati ya mama na baba," alisita kiasi, akatikisa kichwa na kisha kuendelea.

"Nasikia mama yangu ametoka kwenye jamii ya Bamwezi, baba mnajua jamii yake bila shaka. Daima mama alichukuliwa kama mgeni, si katika boma letu tu, bali pia katika kijiji kizima. Haikuwa ibra kumsikia nyanya akimrejelea mama kama *Mũki,* yaani 'Huyo wa kuja', na kusema kwamba msichana wa Bamwezi, hata akiwa na umri wa miaka tisini ni msichana wa Bamwezi tu. Haya yalilengwa kumkumbusha kwamba yeye hakuwa wetu. Uhasama ulizidi baada ya vurugu za miaka mitano iliyopita. Nyanya alimwona mama kuwa chanzo cha kuharibiwa kwa mali yetu, kwamba ndiye aliyewafanya majirani zetu kutuchomea boma ili watuondolee gugu ambalo liliutia najisi utambulisho wetu. Nilimtazama mama akidhoofika kiafya kwa majonzi ya kutengwa na wale aliowadhania ni aila yake. Sikujua kilichokuwa kinamdhili siku hizo, ila nilikisia kuwa mlikuwa na mvutano kati yake, baba na nyanya."

Alisafisha koo na kuendelea kwa sauti iliyolemaa.

"Jahazi letu liligonga mwamba asubuhi moja nilipoamka na kupata kibarua juu ya meza ndogo iliyokuwa chumbani mwangu. Kibarua hicho kilikuwa kimehifadhiwa ndani ya bahasha ndogo nyeupe yenye picha ya moyo. Niliifungua barua kwa viganja vilivyokuwa vinatetemeka na kuyafikicha macho yangu ili kuona aliyekuwa ameiandika. Hata hivyo macho yalikataa kuona wakati huo. Woga huweza kumtia mtu

upofu wa muda! Hatimaye moyo wa shauku uliyashurutisha macho kukisoma kile ambacho kilisomeka kama ujumbe wa mauti.

2/6/2009

Mpenzi Mwanaheri,

Utakapoisoma barua hii sitakuwa hapa, pengine hata sitakuwa katika ulimwengu huu. Ila jua ya kwamba imenibidi kuondoka. Sikudhamiria hata siku moja kuwaacha wewe, Lime, wala baba yenu. Lakini uvumilivu wangu umeshindwa kuniletea mbivu. Nimemeza shubiri kwa miaka mingi, kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiwa kwa nisiyoyatenda.

Nimechoka. Nimechoka kukilovya kifua changu kwa machozi kila mara. Nimechoka kuitwa mwizi wa mayai ambayo kuku wenyewe watagao nimewafuga mimi! Nimechoka kuitwa mwizi wa mali yangu! Nimechoka kupigania penzi la mwenzi na mavyaa, na mwenzi mwenyewe haoni ananipagaza machungu.

Najuta sana kwa kuwaaacha, wanangu. Hata hivyo naomba jambo moja tu kwako. Tafadhali umtunze Lime, na zaidi mno, mtiini baba yenu na kuyazingatia masomo yenu.

Mwenyezi Mungu awaepushie maovu yote. Asitokee mja akawadhulumu furaha yenu jinsi ulimwengu ulivyonihini utulivu. Kwaherini wanangu. Tutaonana siku moja, inshallah.

Mama yako mpendwa,
Subira.

Mwanaheri alimaliza kuwasomea wenzake barua hii, barua ambayo alikuwa ameiandika upya kwenye moyo na akili yake, barua ambayo kila mara alipoisoma, hisia za maonevu ziliuchocha moyo wake, akahisi kama aliyekanyagwa kwa daluga, ila hakujua wa kushtakia.

"Baada ya miezi miwili," Mwanaheri aliendelea kuhadithia, "baba alikwenda kumtafuta mama kwao asimpate. Alijuzwa kuwa mama alikuwa ameenda mjini Kisuka kuzumbua riziki. Baba alifululiza mjini kumfuata mama, majuto yamemjaa kifua. Miezi miwili, mitatu, minne, mitano, sita ... Hata alipompata alikuwa amejifia chumbani mwake wiki mbili zilizopita, tayari mafunza yanafanya kazi yake, chupa ya kinywaji kikali ubavuni pake. Baba alizoazoa kilichobakizwa na uozo, tukakizika. Kaburi limesimama kwa kedi nje ya nyumba yetu kama ukumbusho wa mama yetu Subira ati. Linaloumiza zaidi ni kuamka kila asubuhi kumtazama baba ambaye amebaki gofu tu. Uchungu uliojiandika usoni mwake unazidi hata ule uliomkumbatia siku alipotutazama mimi na Lime tukifanyiwa unyama na vijana wenzetu."

Mwanaheri alimaliza usimulizi wake ghafla na kushusha pumzi nzito. Matone mazitomazito ya machozi yalikuwa yakimdondoka. Umu na Kairu walimwacha autue mzigo wake. Hadithi yake Mwanaheri ilisomeka kama ya Umu, tofauti ni kwamba Naomi, mama yake Umu, hakumjuza kuwa ameondoka. Sasa Umu alianza kuhisi mzigo wake ukiwa mwepesi zaidi.

"Shogangu nakwambia, mara nyingi mwalimu anapofundisha mawazo yangu hutangatanga," aliendelea Mwanaheri. "Hujiuliza kwa nini mama alitekeleza kitendo

hiki cha ubinafsi. Lakini huja nikamlaani shetani kwa kujishughulisha na mambo ambayo siwezi kuyabadilisha. Vipi binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika? Nimeamua kufuata ushauri wa Mwalimu Dhahabu wa kuandama elimu kama nyenzo ya kuniwezesha kuleta mabadiliko katika jamii. Kama mama yangu angetafuta mikakati bora zaidi ya kuhusiana na wakwe zake badala ya kukata tamaa, kuukebehi utu wake kwa kututelekeza, na kujikabidhi kwa mauti, huenda maisha yangu na ya ndugu yangu yangekuwa bora zaidi. Kulelewa na mzazi mmoja kuna kero, hasa ikiwa mzazi huyo anaandamwa na majuto daima." Mwanaheri sasa alikuwa akikizuia kilio ambacho kilikuwa kinataka kumvamia tena.

Wakati wote huu Zohali alikuwa anausikiliza utambaji wa marafiki zake huku amebana kekevu za kilio zilizokuwa zimemvamia. Moyoni mwake mlikuwa na mvutano mkubwa. Je, awatolee wenzake dukuduku lake au aendelee kulizika moyoni mwake jinsi alivyozoea? Hatimaye alishusha pumzi na kuanza kukisimulia kisa chake, macho kayatunga kwenye ukuta kana kwamba kisa chenyewe kilikuwa kimeandikwa pale.

"Mimi nilikuwa mtoto wa nyumba kubwa," Zohali alianza kwa sauti ya chini, "babangu alikuwa mkurugenzi katika Shirika la Utoaji wa Huduma za Simu, mamangu alikuwa mwalimu mkuu wa shule maarufu ya kitaifa. Si kwamba sikulelewa nikaleleka, la! Baba na mama walikuwa walezi wema. Mimi na ndugu zangu hatukupungukiwa na lolote; si pesa za masurufu, si ushauri ... vyote tulipewa. Maisha yangu yalianza kwenda tenge nilipojiunga na kidato cha pili. Unajua

hali ya mtafaruku wa kihisia inayowapata vijana katika umri huu. Niliikumbatia hali hii kwa papara za ujana, kutahamaki nikajipata nimeambulia ujauzito. Naikumbuka vizuri sauti ya mwalimu mkuu wakati alipotoa hukumu ya kifo:

"'Dadake Zohali, samahani sana lakini uchunguzi unabainisha kwamba Zohali ni mjamzito. Nimekuita hapa ili uweze kumrejesha nyumbani. Akijifungua wazazi wake wanaweza kumtafutia shule nyingine,'" Zohali aliigiza sauti nzito ya mwalimu mkuu.

Zohali aliwatazama wenzake kwa zamu, kana kwamba anatathmini taathira ya maneno yake kwao, kisha akaendelea.

"Dada Tima alimtazama mwalimu mkuu kwa mshtuko mkubwa, akashusha pumzi na kutikisa kichwa. Yaliyotokea kuanzia siku hiyo hayaelezeki. Nimelala kwenye barabara za jiji, pamoja na watoto wengine wa mitaani, nimetumia gundi ili kujipurukusha na hali ya ukiwa na kuumbuliwa, nimepigana na majitu yaliyotaka kuuhujumu utu wangu kwa kuninyanyasa kijinsia. Hata wenzangu walipoona siku yangu ya kujifungua imekaribia na kunipeleka kwenye kituo cha Wakfu wa Mama Fatma, siwezi kukwambia ni mangapi niliyokuwa nimeyapitia."

Zohali alitua pumzi nzito kisha akaendelea, "Namshukuru sana Mtawa Pacha ambaye aliniokoa kutoka kinamasi cha uguliko la moyo. Siku ile nilipofika katika makao haya, mtawa huyu hakukawia kuniuliza iwapo nilikuwa na wazazi. Nami kwa kukumbuka kusimangwa na kudhalilishwa nilikotendewa kabla ya kuamua kutoroka kwetu, nikamlazia kuwa mimi ni yatima, kwamba wazazi wangu walikufa miaka

minane iliyopita, na mimi na umbu zangu tulihamia jijini kutafuta riziki baada ya kupokonywa urithi wetu na jamaa za wazazi wetu. Pacha aliyeonekana kutoyaamini maneno yangu alinidadisi:

"'Una hakika na unayoyasema?'

"'Nina hakika,' nilimjibu kwa sauti thabiti huku nikijiuliza moyoni, 'Kwa nini nisiwe na hakika? Kwa nini nishuku jibu langu na hali nimeisha kukiua kitovu changu siku nilipokivuka kizingiti cha lango la boma la baba?'

"Mtawa Pacha alitikisa tu kichwa na kuniahidi kwamba baada ya kujifungua angenirejesha shuleni. Hivi mnionavyo nastahili kuwa katika kidato cha nne, lakini uzazi na ulezi umenipotezea miaka yangu miwili. Mtawa Pacha ndiye aliyenitafutia nafasi katika shule hii. Hapo alipo hajui kwamba mama yangu ni mwalimu mkuu katika shule mashuhuri nchini. Natamani sana kumwambia Pacha kwamba nina wazazi lakini moyo umekataa katakata. Nitamwambiaji nina wazazi na hali waliisha kunikana wakati nilipohitaji pendo lao? Fikiria wewe, umeambulia ujauzito katika umri teketeke, hata hujui kuwa wewe ni mjamzito kwa vile hata hedhi yenyewe hujaiona. Kisha ufukuzwe shule, unajikokota nyumbani, moyoni ukiamini kwamba ng'ombe akivunjikia mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa, kwamba hata kosa lako likawa kubwa vipi, teke la kuku halimuumizi mwanawe. Unaingia sebuleni mwenu na kuwaangukia miguuni wazazi wako. Halafu unaloambiwa ni, 'Umeipaka mashizi familia hii, umeipoteza bahati yako kwa kufuata utashi wa moyo wako. Kaa hapa nyumbani uilee mimba yako, ukiisha kujifungua, utamtafuta baba mtoto msaidiane malezi.'

"Wenzangu, madhila niliyopata nyumbani mwetu hayaelezeki. Baba alisema kwamba hakuwa na pesa za kumlipa kijakazi tena. Kazi za nyumbani zikaniangukia mimi. Si kufua, si kupiga deki, si kupika ... almuradi kila siku ilikuwa na adha zake. Linalonisikitisha zaidi ni kwamba hata mama, ambaye anajua uchungu wa kulea mimba, hakutoa sauti kunitetea. Aliridhia yote aliyoamua baba kunihusu. Haya yalinitia uchungu na unyanyapaa ambao ulinifanya niwafishe wazazi wangali hai. Hata mwanangu Nasibu sijawahi kumwambia kwamba ana babu au bibi. Ila najua kwamba itabidi siku moja nimwambie ukweli mtumishi huyu wa Mungu ambaye amejisabilia kunilea kama mwanawe," Zohali aliyakamilisha masimulizi yake na kuyaondoa macho yake kwenye ukuta ambapo yalikuwa yameganda.

Muda wote huu Chandachema alikuwa anawasikiliza mafanani hawa, kimya cha kaburi kimezifumbata hisi zake. Hata mpigo wa moyo, na pumzi hazisikiki. Inachofanya akili yake ni kusoma na kusimulia kisa cha maisha yake, kisa ambacho kilishabihiana kama sahani na kawa na cha ndugu zake hawa. Hata alipoanza kuwasimulia akina Umu hadithi yake, chozi ambalo lilikuwa linamtiririka muda wote huu lilikatika, akashusha pumzi ndefu, akatwaa tabasamu na kuutoa undani ambao alikuwa kaufumbika miaka yote hiyo.

"Nahisi kama nasoma matini moja na ya dada Zohali," alianza Chandachema, "maisha yangu yalijaa shubiri tangu utotoni. Sikumbuki nikimwona mama yangu. Ninalokumbuka ni kwamba nililelewa na maskini bibi yangu ambaye, katika utu uzima wake, hakuisha kufanya nongwa akisema, 'Huyu mwanangu Fumba atakuja kunifisha kabla

ya siku zangu. Mtu atamringaje binti ya watu, amvurugie masomo yake, kisha amtelekezee kijijini kwa wazee wake? Na uwe ule msimamo wa wazazi wa Rehema, kwamba mwanao sharti akamilishe masomo yake baada ya kujifungua, kwamba Rehema hawezi kuolewa na mwalimu wake. Lakini huku kuniletea mtoto mimlelee, si haki. Mahitaji ya mtoto yenyewe hatumi, nimebaki kutumia kidogo ninacholetewa na dada zake kumtunza huyu mtoto.'

"Kama alivyotabiri, bibi alikufa nikiwa katika darasa la kwanza. Wakati huo *auntie* zangu walikuwa wameolewa, tukabaki mimi na bibi huyu kuliwazana. Nasikia baba yangu Fumba alikuwa kahamia Uingereza na familia yake, anafundisha katika chuo kikuu. Nyota yangu ilizimika baada ya mauko ya nyanya. Mwezi wa kwanza baada ya tanzia hii, nilihifadhiwa na jirani, nikawa naenda shuleni na kurudi hukohuko, mimi na watoto wake watatu ambao tukisoma pamoja. Mwezi wa pili nilianza kuona mabadiliko. Ule uchangamfu aliokuwa nao Satua, mke wa jirani, uliyeyuka ghafla kama umande kwenye jua la asubuhi; ikawa ni, 'mgeni siku ya kwanza, siku ya pili chukua jembe ukalime'. Satua alianza kulalamikia hili na lile. Alilalamikia kuisha haraka kwa sukari, alilalamikia matumizi kiholela ya sabuni ya kuogea, alinung'unika kuhusu kubanana kwa jeshi la watoto kwenye chumba cha malazi ... almuradi kila kitu kilikuwa na doa machoni mwa Satua. Hata nilipong'amua kwamba akufukuzaye hakwambii toka, nilikuwa nimepitia mengi.

"Nilifunganya kidogo nilichokuwa nacho, nikapitia kwenye boma la marehemu nyanya yangu, nikalitia kufuli lango la boma na kujikabidhi kwa ulimwengu. Niliuliziaulizia kitovu cha mama yangu kutoka kwa majirani lakini sikupata

habari za kutosha kupafika mahali hapa. Hata maelezo aliyonipa jirani mmoja katika mazungumzo yetu hayakufaa kitu.

"'Mama yako,' alifafanua Katini, 'ni mzaliwa wa Pwani. Huko ndiko baba yako Fumba alikokuwa akifundisha alipokutana naye. Fumba alisuhubiana na Rehema akiwa kidato cha tatu. Wewe ni zao la uhusiano huo. Tendo la Fumba la kumwendea kinyume mwanafunzi wake lilimsababishia kuachishwa kazi kwa muda, na baadaye kuhamishiwa eneo lingine. Baada ya kuzaliwa kwako baba yako alitaka kumwoa Rehema lakini wazazi wa Rehema wakakataa. Walichokifanya wazazi hawa ni kumkabidhi Fumba mtoto wake. Naye, kwa kutokuwa na mke, akakuleta ulelewe na nyanya yako.'

"'Lakini si baba alikuja kuoa?' nilimuuliza Katini.

"'Ndio alioa. Lakini unajua wanawake wa siku hizi walivyo; hawana moyo wa kumlea mwana wa mwenzao. Wanachelea kwamba kile kitovu kilichomuunganisha baba na mama mtoto kitamea tena. Wanasema kwamba kumlea mtoto wa mwanamke mwingine ni kuhatarisha masilahi yao katika ndoa,' akanijibu Katini.

"Usimulizi wa Katini ulinikatisha tamaa zaidi. Nilijua kwamba hata nikamtafuta mama, huenda naye ameolewa, na katika jamii yetu nasikia mtoto ni wa baba. Kwa hivyo hata huko alikoolewa mama sitakuwa na hadhi yoyote, nikaona nitachukuliwa kama mpita njia aliyekuja kuvuruga utulivu wa familia yao. Moyo uliniambia niende kwa shangazi yangu, lakini nilijikanya. Nilijiuliza, ikiwa baba na mama hawawezi kunilea, sembuse shangazi? Haihalisi kumwongezea Shangazi

Waridi mzigo. Hapo alipo hata ndiye anayegharamia masomo yangu kwa kidogo anachokipata kutoka kwenye vikataa vyake.

"Binadamu aliumbwa kupambana na ulimwengu na kutumia rasilimali aliyopewa na Mungu kuyaboresha maisha yake. Najua nimepewa akili razini, nina azma ya kujiendeleza masomoni. Najua nitahitimu masomo yangu siku moja, na kurudi hapa hapa petu kupajenga upya. Sitarajii kutatokea mtu kunyakua ardhi hii ambapo nimemzika mpenzi nyanya yangu!" Ari hii ilinifanya nijitome kwenye njia nisiyojua kikomo chake.

"Akili na miguu yangu ilinielekeza katika kijiji kimoja wanakoishi wafanyakazi wa shamba la chai la Shirika la Chai la Tengenea, kinachomilikiwa na Mzungu mmoja aliyekuwa mlowezi nchini. Mzungu huyu, kwa jina Richard, alikufa mara tu baada ya Uingereza kuikabidhi nchi hii uhuru. Hata hivyo, familia yake bado inalimiki shamba hili, kama Wazungu wengine wanavyoyamiliki mashamba ya michai na mibuni pamoja na mashirika mengi ya utengenezaji wa mazao ya mimea hii nchini. Kining'inya wa Richard ndiye Afisa Mkuu Mtendaji wa shirika hili hivi sasa.

"Ukiniuliza ni kwa nini niliamua kuja hapa nitakwambia kwamba nilijua pana shule hapohapo shambani. Pili, nilijua kwamba iwapo ingetokea kwamba singekuwa na wa kuyakidhi mahitaji yangu ya kimsingi, nyanya yangu alikuwa amenifunza umuhimu wa kufanya kazi. Hapohapo katika shamba hilo, ningeweza kuchuna majani chai Jumamosi na hata wakati wa likizo ili kujikimu.

"Asubuhi moja ilinipata ndani ya afisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu, Bi. Tamasha, alisikiliza kadhia yangu kwa makini. Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi.

"'Unaweza kuanza masomo katika darasa la pili. Nitamwomba mzazi mmoja akupe hifadhi,' alisema Bi. Tamasha.

"Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha yangu katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Bwana Tenge na mkewe, Kimai, walinichukua kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkafahamiana na kunguni wake? Ninayowaambia ni asilimia ndogo mno ya niliyoyaona. Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hichohicho kimoja; ndicho cha malazi, ndicho cha mapokezi, ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvunguni mwa kitanda cha wazazi. Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka danguro wakati Bi. Kimai alikuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu ... hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za kisaikolojia nilizozipata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigo mkubwa kwa wahisani wangu. Si kwamba waja hawa walinibagua, la! Kusema hivyo kutakuwa

kuwapaka mashizi bure. Hata hivyo nilihisi kwamba nimepata mbavu za kufanya angaa kibarua kidogo, na kuwatua wawili hawa mzigo wa kuninunulia sare na madaftari.

"Nilianza kuchuna majani chai kwa malipo kidogo nikiwa darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kufanya kazi kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipitia hukohuko. Nyakati nyingi nililala humohumo katikati ya michai, wakati mwingine kwa marafiki wangu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipoufanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

"Wakati huo Bwana Tenge alikuwa ameisha kupewa uhamisho, akaenda kufanya kazi katika shamba lingine. Ndivyo wafanywavyo wafanyakazi hawa; kuhamishwa kila uchao bila mtu kuwazia kwamba wana watoto wanaoenda shule, na kwamba kuhamahama huku kunawavurugia masomo wana hawa. Nalishukuru shirika la Kidini la Hakikisho la Haki na Utulivu kwani ndilo lililonivua kutoka ziwa la uhitaji. Siku ile baada ya matokeo ya mtihani wa darasa la nane, mwalimu mkuu alitaka kukutana na mfadhili wangu nami nikamweleza kuwa nilikuwa nimeacha kabisa kuishi na mfadhili huyu nikiwa darasa la sita ingawa kwa kweli nilikuwa nimehama hapo awali.

"'Huo ndio wakati alipopata uhamisho?' aliuliza.

"'Ndio mwalimu. Kumbuka kuwa huo ndio wakati hata Kemi na Duma walipoacha kuhudhuria madarasa. Wazazi wao walikuwa wamepewa uhamisho,' nilimwambia.

"Bi. Tamasha aliinamisha kipaji, amehizika kwa kutokumbuka jambo la muhimu kama hilo, pengine kwa kuwa shuleni humu imekuwa ibada kwa watoto wa wafanyakazi hawa kuacha shule, hata kwa sababu zisizo na msingi. Bi. Tamasha alimwita Bwana Mwenge, msimamizi wa Idara ya Ushauri na Uelekezaji shuleni, akamsimulia kisa changu. Bwana Mwenge alinishika begani na kuniambia,

"'Usijali, Bi. Mdogo, mradi una ari na hamasa ya kusoma, utasoma. Kuzaliwa maskini si kibali cha kuishi kimaskini katika aushi nzima. Upo wakati dau la mnyonge linapoenda joshi, likashinda la mwenye nguvu.'

"Baada ya juma moja nilijipata katika makao ya watoto mayatima ya Jeshi la Wajane wa Kristu. Makao haya yalianzishwa na wanawake wajane kwa lengo la kuwapa hifadhi watoto mayatima, watoto waliotupwa na mama zao, na wale wenye wazazi au walezi wahitaji. Mimi sasa naishi huko, ndiko nyumbani hasa. Ila nina muono mkubwa. Nitajitahidi kwa jino na ukucha katika masomo yangu. Azma yangu ni kuwa mwanasheria au afisa mkuu wa masilahi ya kijamii. Siku moja nitakuwa mtetezi wa haki za kibinadamu, hususan haki za watoto," Chandachema alimaliza usimulizi wake na wakati huohuo taa zikazimika, ni wakati wa bweni kufungwa na wanafunzi kulala.

Sura ya Saba

Ni alasiri moja ya joto kali. Mwangeka na mkewe, Apondi, wameketi kwenye behewa la nyumba yao. Macho yao yameelekezwa kwenye kidimbwi ambamo wanao watatu—Sophie, Ridhaa na Umulkheri—wanaogelea, mara wanapiga mbizi, mara wanafukuzana. Anayewatazama Mwangeka na Apondi kwa mbali anawaona kama walezi wawili ambao wako makini kutazama kujipumbaza kwa wanao. Hata hivyo ukichunguza kwa makini utapata kwamba wawili hawa hawaoni chochote japo wanatazama. Kila mmoja, Apondi na Mwangeka, amepotea kwenye ulimwengu wake.

Mwangeka anapomtazama Apondi anatabasamu. Ukurasa wa kitabu cha akili yake unafunguka. Kisa cha kukutana kwao kinakunjuka.

Miaka mitatu ya ujane ilikuwa imemdhihaki Mwangeka vilivyo. Jumba lake hili, japo lilijaa watumishi, lilikuwa kama karakana kubwa lenye wahandisi wengi ambamo kila mmoja alikuwa akishughulikia mashine yake. Babake, Ridhaa, alikuwa amehamia humu kwa muda, akiishi naye. Unaweza kusema kwamba hawa walikuwa wajane waliokomaa. Walililiwazana. Lakini hebu niambie wewe iwapo kuna ushirika katika hisia za ukiwa. Ushirika ni mojawapo ya mahitaji ya binadamu kulingana na vitengo vya mahitaji vilivyopendekezwa na

mwanasaikolojia Maslow katika ule msonge wake maarufu wa mpangilio wa mahitaji kulingana na thamani yake. Hata hivyo, ni wazi kwamba ushirika ambao Mwangeka alihitaji si wa baba, na wawili hawa walijua hili kifai. Alihitaji mtu wa kumpembeja, kumliwaza na kumzomea kwa mtazamo tofauti na wa mzazi. Alihitaji mwenzi katika uzazi na malezi. Ridhaa aliyaelewa haya na kila mara alimhimiza mwanawe.

"Mwanangu, jua langu li karibu kuchwa. Nilikuwa ninamwomba Maulana siku zote akuregeshe nyumbani ukiwa hai. Uweze kuuendeleza ukoo wetu, niweze kupata wajukuu. Umekiomboleza kifo cha mkeo vya kutosha. Hiyo ndiyo heshima anayostahiki mke. Sasa muda umefika. Hutakuwa na lawama duniani na hata ahera iwapo utafunga akidi," Ridhaa alimuusia Mwangeka jioni moja baada ya chajio.

"Baba, hata mimi nimeliwazia jambo hili kwa muda. Hata hivyo, moyo wangu umekuwa yabisi. Hisia zangu zimekufa ganzi. Nimeshindwa kumsahau mke wangu Lily, na Becky mtoto wangu. Singependa kumchukua mwana wa watu kuja kujaza pengo aliloacha mke wangu tu. Utakuwa uhayawani," Mwangeka alimjibu babake.

Baba mtu alimtazama mwanawe kwa imani. Laiti kungalikuwa na kilimbo cha mapenzi! Angalimpa mwanawe kubwia ili apate kuamsha hamu ya kupenda tena.

"Lakini," alijiambia, "wakati ndio mwamuzi. Itakuja siku atakapotokeza hurulaini wake. Siku hiyo hicho kiharusi chake cha muda kitapona. Ataifungua kufuli kubwa iliyoufunga moyo wake na hiyo itakuwa siku ya kumwaga chozi la heri," Mzee Ridhaa alijiambia haya huku kimuyemuye ambacho

kilikuwa kimehamia na kuishi moyoni mwake tangu kutoweka kwa familia yake kikipungua kwa sekunde.

Baba mtu aliendelea kungojea kwa matarajio makuu, kila jioni akimchunguza mwanawe kuona kama kumetokea badiliko lolote, kwani, kama alivyojua Ridhaa, uso mara zote ni msaliti mkubwa wa moyo wa kupenda. Nalo jambo la sudi huenda kwa sudi. Siku moja Mwangeka alikuwa miongoni mwa maafisa waliohudhuria warsha kuhusu jukumu la vikosi vya askari katika kudumisha usalama, amani na maridhiano nchini. Warsha hii ilikuwa imeandaliwa na Shirika la Msalaba Mwekundu. Hapo ndipo alipokutana na Rachael Apondi, ambaye alifanya kazi katika Wizara ya Vijana na Masuala ya Kijinsia. Apondi alikuwa na shahada katika taaluma ya masuala ya kijamii. Apondi alikuwa mmoja wa wawasilishaji wa makala katika warsha hii.

Zamu ya Apondi ilipowadia, alijitoma ulingoni kuzungumza. Mwangeka alivutiwa naye mara moja! Ule mtindo wake wa uwasilishaji, kule kupanda na kushuka kwa sauti yake, ucheshi wake wenye hadhari, namna alivyoiteka hadhira yake ... vyote vilishindana kuikamilisha haiba ya binti huyu. Mwangeka hakuamini jinsi alivyotekwa bakunja na mzungumzaji huyu. Na hayo yasikushangaze kwani tangu hapo ipo nadharia tete kuwa wahandisi hawana hulka ya kuvutiwa na binadamu. Wao wamezoea kuzungumza na mashine ambazo hazijui kuzungumza kwenyewe!

"Mabibi na mabwana," alianza Apondi, "suala la usalama haliwezi tena kupuuzwa. Usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu. Kwa hakika, tunaweza kusema kuwa usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi. Bila usalama

binadamu hawezi hata kushiriki katika shughuli za kuzalisha mali, hivyo hata mahitaji mengine ya kimsingi kama vile chakula, malazi na makazi hayawezi kukidhiwa. Kila mja ana jukumu la kudumisha amani na usalama. Hata hivyo, wafanyakazi wa umma, na hasa polisi na wanajeshi, wana jukumu kubwa zaidi la kudumisha usalama na amani. Si kwamba wengine tunaambiwa tupakate mikono kungojea kulindwa, la hasha! Kila mmoja wetu anastahili kuhakikisha kuwa ameepuka vitendo vya kihalifu. Inahalisi pia kila mtu kuwaangaza wahalifu wakati wote. Vikosi vya polisi na wanajeshi vimefunzwa maarifa ya kukabiliana na kadhia za jinai na upelelezi. Kwa hivyo wana dhima kubwa zaidi ya kudumisha amani. Aidha, wana ujuzi wa njia mwafaka za kutatua migogoro na kupalilia maridhiano. Wanajua ni lini watashambulia na ni lini watarudi kinyumenyume kuepuka shambulizi la adui. Kwa hivyo tunawasihi mwajibike zaidi katika kazi zenu. Katika kozi zenu mmefunzwa *Effective Communication and Conflict Resolution*," alisema na kutulia kiasi kabla ya kuendelea.

"Suala la polisi na wanajeshi kutatua mizozo midogomidogo kwa makeke na bunduki ni jambo ambalo limeanza kupitwa na wakati; ni sawa na kumuua chawa kwa fimbo! Raia wanahitaji zaidi ushauri badala ya vipigo. Kutatua tofauti zetu kwa vita ni kama kufukuta moto zaidi, na amani tuliyoazimia kupata haipatikani. Vilio vya raia kuhusu kile wanachokiita *extra judicial killings* vimehanikiza kote. Huenda tusiwe wahusika katika visa hivi. Hata hivyo ni vyema kutahadhari kabla ya hatari. Wakati mwingine, ndugu zangu, amani haiji kwa ncha ya upanga!"

Apondi alitongoa haya na mengine mengi. Aliwaonya walinda usalama dhidi ya kutaahiri kufika pahali palipotokea mkasa.

"Wapo baadhi yetu ambao mkasa unapotokea wanangojea vikosi kutoka Israeli kuja kuwaondoa manusura kutoka kwenye vifusi vya mabaki ya majengo! Wakati waokoaji hawa wanapofika, bila shaka nusu ya roho tayari huwa zimepotea! Kumbukeni methali isemayo, 'Ulingo wa Kwae haulindi Manda.' Jukumu la kudumisha amani na usalama ni letu. Usalama hauji bila ya kujitolea mhanga. Na kujitolea mhanga huku si kushika bunduki tu, bali pia kujiasa dhidi ya njama za kifisadi na nyendo nyingine hasi. Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea, inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe, na baadaye wanagawanya ngawira nao! Wengine wetu tumeyaacha magari makuukuu barabarani, kisa na maana, wenye magari haya ni miamba isiyogusika. Wengine nasi tumeshindwa kabisa kudhibiti hasira zetu. Ufyatuaji ovyo wa risasi umesababisha vifo vya wananchi wasio na hatia. Watetezi wa haki wanalilia kile wanachokiita *Untimely deaths of innocent people, many of whom are youth.* Kumbukeni kwamba hata mtu akiwa mhalifu, ana haki, ana haki ya kufikishwa mahakamani na kushtakiwa kabla hajapewa adhabu yoyote.

"Kwa hayo machache nawasihi nyote tuungane ili kudumisha amani na usalama nchini mwetu. Asanteni."

Apondi alitoka jukwaani akisindikizwa na makofi ya hadhira yake. Mwangeka alimsindikiza kwa macho zaidi ya makofi. Alikuwa hajifai kwa hisia. Barafu iliyokuwa

imegandia moyoni mwake ilianza kuyeyuka na moyo kutwaa uvuguvugu. Hatimaye uyabisi wa moyo wake umetoweka!

"Huyu binti ananikumbusha marehemu mke wangu Lily. Ujasiri wake, ufasaha wa lugha, utundu wake, mwanya kwenye meno ya juu ..." alijisemea Mwangeka huku akielekea alikokuwa Apondi kumpa mkono wa tahania.

"Hongera kwa uwasilishaji mzuri. Naitwa Mwangeka," Mwangeka alisema kwa kigugumizi cha kujitia.

"Vizuri kukujua," alijibu Apondi bila kuzingatia aliyoyasema wala hisia za aliyetoa kauli ya awali. Baadaye, hata hivyo, Mwangeka alipata fursa ya kufahamiana zaidi na Apondi wakati wa chamcha.

Huu ndio uliokuwa mwanzo wa usuhuba na uchumba wa mwaka mmoja ambao kilele chake kilikuwa kufunga ndoa. Apondi alikuwa mjane wa marehemu Mandu. Mandu alifia ughaibuni, katika shughuli za kudumisha amani huko, nyumbani kukarudi jina tu, akawa amekufa kizalendo na kishujaa. Hata hivyo, kilio alichomwachia Apondi na Sophie, mwanawe wa miaka miwili, hakikumithilika. Kifo hiki kilimtia Apondi woga, akachelea kuhusiana na mwanamume mwingine asije akafa na kumwachia ufa mwingine wa moyo. Miaka sita baada ya kufiwa ndipo alipokutana na Mwangeka, hadithi zao zikawa zinatambwa sawa. Usawa wa hali zao ukalitilia gundi penzi lao, wakapanga kuoana. Mzee Ridhaa alipoarifiwa kuhusu uhusiano huu, alishusha pumzi, akasema kama yule mtawa wa hekaluni katika Biblia,

"Sasa Baba mtumishi wako anaweza kupumzika kwa amani, kwa maana macho yangu yameona ufufuo wa mwanangu Mwangeka."

Aliwaoza wanawe kwa taadhima kuu huku machozi ya heri yakikilovya kidari chake.

******

"Pongezi Rachel," sauti ya muuguzi ilisikika mawazoni mwa Apondi, umejaliwa kijanaume jamali kwelikweli."

Apondi alikumbatiwa na furaha isiyo na kifani, ghafla uchungu wa uzazi na zingizi ya baada ya uzazi ikamwondokea. Alikitazama kitoto kilichokuwa kimewekwa kwenye kisinia na muuguzi, kinafanyiwa viviga vya mwisho kabla ya kukabidhiwa kwa mama mzazi. Machozi ya furaha yalimtiririka. Mashavu yake laini yaliyokuwa yamesawijika kwa uchungu na mikemeo ya chumba hiki cha kujifungulia yalitwaa nuru. Alishusha pumzi ya utulivu na kusema,

"Huyu ataitwa Ridhaa. Ndiye bavyaa yangu ambaye amenikubali katika familia yake licha ya kwamba koo zetu zimebaidika kama ardhi na mbingu. Hatimaye Sophie amepata mwenzake, naye Baba Ridhaa amepata fidia, japo ukufi, kwa familia yake iliyoteketea."

Mwangeka na Apondi walikuwa wameamua kuwa watoto wao wawili, Sophie na Ridhaa, walitosha kuikamilisha familia yao. Sisemi kwamba wangeweza kutiwa katika lile kumbo la wazazi ambao hukerwa na vinywa vingi vya kulisha. La! Hasha. Mwangeka na Apondi walikuwa mkono wazi. Maskani yao yalimiminika wahitaji kutoka katika kila upembe wa eneo-gatuzi lao, nao hawakurudi kwao mikono mitupu.

Kuzaliwa kwa Umulkheri katika familia ya Apondi na Mwangeka kulikuwa zao la ukarimu wao. Baada ya Umulkheri kujiunga na Shule ya Tangamano, mama aliyekuwa

akiyasimamia makao ambamo Umu aliishi alishirikiana na mwalimu mkuu wa Tangamano kumtafutia mfadhili. Kila mwisho wa muhula Umu alionekana mwenye mawazo mazito. Alikosa ule uchangamfu na matarajio ya mwanafunzi anayekwenda nyumbani kwa likizo. Kila wakati mwalimu angempa ripoti kuhusu maendeleo yake shuleni, Umu angetiririkwa na machozi. Mwalimu Dhahabu alishindwa kuelewa kwa nini Umu alikuwa akilia na hali ndiye aliyekuwa mwanafunzi bora katika darasa lake.

"Umulkheri," aliita Mwalimu Dhahabu siku moja, "kipi kinachokuliza? Mbona huna bashasha za kijana wa umri wako? Unapapenda unapoishi?"

"Ni kweli kuwa ninapapenda ninapoishi," alisema Umu, "mimi hutunzwa vyema katika makao hayo. Hata hivyo, nina hamu ya kuishi nyumbani kuliko na wazazi kama waishipo wenzangu. Ingawa wengine wanaishi kwenye kambi, hao hupata wazazi wao humo, wakawasimulia visa vya shuleni, wakawaonyesha ripoti zao, wakawaambia hofu na maazimio yao. Mimi nimekosa hayo. Natamani kuwa na mama. Mama yangu alitutoroka, lakini moyoni nahisi kuwa yu hai. Huenda nikampata nikimtafuta."

Mwalimu Dhahabu aliyasikiliza maneno ya Umu kwa makini. Mshale wa huruma ulimfuma moyoni, akataka kumkumbatia na kulia naye lakini akajirudi. Baada ya kufika nyumbani jioni hiyo, Mwalimu Dhahabu alimpigia simu rafiki yake wa utotoni Apondi. Alimweleza kadhia ya Umu. Apondi alikubali kumchukua Umu kama mtoto wake wa kupanga. Alimwambia Mwalimu Dhahabu kuwa atawasiliana

naye baada ya kushauriana na mumewe Mwangeka. Mwangeka hakuwa na pingamizi yoyote kuhusu kuwa mlezi wa Umulkheri.

"Hii ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mungu amenifidia yule mwanangu aliyekufa," Mwangeka akamwambia mkewe.

Umu alipata wazazi wapya. Humo ndimo alimomalizia siku zake za likizo. Wao ndio waliomlipia karo. Ingawa mwanzoni Umu aliwaona wazazi wake hawa kama titi la nyati ambalo hukamuliwa kwa shaka, alikuja kuwazoea na kuwapenda kwa dhati. Polepole lile donge chungu lililokuwa moyoni kumhusu mama yake lilianza kupungua. Banguzi alilokuwa akiuguza moyoni tangu kuondoka kwa mama yake asubuhi hiyo chungu liliacha kutoa usaha na kuanza safari ya kupona kutokana na pendo alilolipata kutoka kwa wazazi hawa wapya. Sasa alikuwa tayari kumsamehe mama yake hapa duniani na ahera. Aliwazia pia kumsamehe Sauna. Hata anapolitamka jina hili mawazoni mwake, Umu anashangaa alikotokomea kiumbe huyu. "Je, huko alikomezewa na ulimwengu ndiko alikowazongomeza Dick na Mwaliko? Ama yeye hakuwa na watoto, akaona awachukue ndugu zangu awalee? Je, huku ndiko kukosa mwana akaeleka jiwe? Na iwe hivyo, kwa nini hakutumia njia halali akawapanga rasmi wanawakiwa hawa?" Umu alijiuliza maswali haya mfululizo.

Sura ya Nane

"Leo uwanja wa ndege una baridi na mzizimo kuliko siku nyingine zote," aliwaza Dick huku kasimama katika mlolongo mkubwa wa watu ambao walingoja kuingia kwenye afisi za forodha kukaguliwa. Hata anaposimama hapa, Dick anakumbuka siku alipoanza kusafiri kwa ndege. Siku hiyo kiwewe kilikuwa kimemkumbatia kwani kazi ya 'kubeba dafina', kama walivyoiita biashara haramu ambayo alikuwa kalazimishwa kufanya siku hizo, ilikuwa imewaingiza wengi kwenye nyavu na madema ya polisi, wakatiwa mbaroni. Siku hizo alikuwa mwanagenzi katika uga huu. Na asiwe vipi mwanagenzi, kinda wa miaka kumi kuingizwa katika biashara ya aina hii? Zipo siku alipotetemeka nusura ajisaliti. Lakini alizoea kujipa moyo. Kila mara alipopatwa na kiwewe alijiambia, " Dickson, wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera. Na mama yako, mama yako hakuwapo tangu hapo. Angekuwapo asingekuacha kutimbwa na ulitima!"

Miaka kumi ya adha na mashaka imepita. Sasa Dick amekomaa. Ilibidi akomae kwani ulimwengu haukuhitaji 'mtoto wa mama', kama alivyozoea kumwambia kijakazi Sauna ambaye alimtosa katika kinamasi hiki cha kulangua

dawa za kulevya. Dick amesafirisha maelfu kwa maelfu ya vifurushi vya dawa hizi. Mwanzoni hakuwa mraibu wa dawa hizi lakini ilibidi ajizoeshe, kwa usalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi ilibidi kuzimeza dawa zenyewe ili kwenda kuzitapika kwenye masoko ughaibuni. Hili lilitokea wakati mashine za forodhani zilipopata makali zaidi siku nyingine na kung'amua shehena kutoka mifukoni ambamo zilishonelewa vibindoni mwa chupi!

Siku ile baada ya kuibwa na kijakazi Sauna, Dickson alipelekewa baba mmoja tajiri ambaye alijitia kumpeleka shuleni. Kumbe alikuwa kapelekwa katika chuo cha kuhitimu kama mvunja sheria! Masomo yake yalifikia ukingo siku alipovuka kizingiti cha nyumba yao pale Mlima wa Simba. Tajiri wake huyu, kwa lakabu Buda, alimfunza mbinu za kujikimu, akamwingiza katika biashara hii. Siku za mwanzomwanzo alikataa kushiriki hadi pale alipotishwa na kuambiwa kuwa angetupwa nje, asingiziwe wizi, na tangu hapo alijua malipo ya wezi katika jamii hii isiyokuwa na nadhari; kutiwa tairi na kuchomwa moto! Wazo la kupatishwa adhabu ya aina hii lilimtetemesha Dick. Alikumbuka jinsi rafiki yake Lemi alivyofishwa kwa njia hii.

Lemi alikuwa ametoka nyumbani na dadake Tindi ambaye alikuwa mwanafunzi katika chuo kikuu. Ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa Lemi. Dada mtu alitaka kwenda kumnunulia ndugu yake wa umri wa miaka kumi na mitano kinywaji. Mama akatoa ruhusa, akaonya pasitokee mtu akarejea baada ya saa kumi na moja magharibi. Maskini hakujua hiyo ingekuwa siku ya mwisho kumwona mwanawe akiwa

hai! Sherehe ilianza vyema, mtoto akala shibe yake, kisha akamwambia dadake,

"Usiku umekuwa mpevu, twende tusije tukamtia mama kiwewe."

"Bado ni mapema. Acha nisakate midundo miwili kisha twende," dadake akamjibu.

Lemi alipelekwa kwenye chumba cha kutazamia runinga ili kusetiriwa asione asiyostahili kuyaona! Binti akaingia uwanjani. Mirindimo ya miguu, mipigo ya makofi na minenguo ya viuno ikaendelea bila kujali mpito wa wakati, wala mtoto aliye chumbani peke yake. Sijui kama unajua jinsi hawa vijana wa vyuo vikuu walivyo! Wengi wao wameshindwa kabisa kutofautisha mchana na usiku!

Hakujua vipi, lakini Tindi alishtukia alfajiri inabisha hodi. Lemi macho yalikuwa yamemwiva kwa kilio, usingizi na machovu ... Hata asubuhi jua lilipotaka kuchomoza, Tindi alimshika mkono mnuna wake wakaelekea nyumbani. Huko nyumbani mama alikuwa amewasaka akaviisha vituo vya polisi! Hatua chache kabla ya Lemi na dadake kufika kwao kulitokea vurumai. Mama mmoja ambaye alikuwa ameraukia matwana ya kumpeleka kazini alikuwa akipiga ukemi, amenyang'anywa rununu yake, akawa anakimbia kuelekea walikokuwa Lemi na dadake kwa msaada. Kumbe anawaelekezea balaa! Umati wa watu uliokuwa umesikia kamsa ya mama huyu uliwaelekea akina Lemi, unataka kuwavaa kwa mawe na tairi. Dadake hajui vipi, lakini alitundika guu begani na kumwachia Lemi ulimwengu. Anasema hakukuwa kupenda kwake. Maumbile ya binadamu ya kujifikiria yeye kwanza yalimfanya kukimbia.

Nyuma Lemi alisalimiwa kwa mawe na mateke. Baadaye alivikwa pete ya tairi kiunoni. Muda si muda alimwagiwa petroli na kutiwa moto. Msalie Mtume za mama aliyeibiwa ziliangukia masikio ya viziwi. Moyo wa Lemi ulisalimu amri kabla ya kufikishwa hospitali na Wasamaria wema walioletwa na dadake Lemi baada ya udugu kumkumbusha kuwa alikuwa amemwacha mnuna wake hatarini!

Dick alipokumbuka kisa hiki cha Lemi aliunasihi moyo wake kukubali kuingilia biashara hii haramu, mwenye nguvu asije akamtumbukiza kaburini. "Huenda nikapata mbinu ya kujinasua baadaye," alijiambia. Na usidhani kisa hiki tu ndicho kilichomsukuma kusalimu amri ya Buda. Dick alihitaji chakula na mahitaji mengine. Dick aliupiga moyo konde, akasema, "Potelea mbali, lisilo budi hutendwa. Hii ndiyo riziki niliyoandikiwa na Mwenyezi Mungu. Ikiwa kweli haya siyo niliyoumbiwa, kwa nini Mungu akamuua baba yangu mpendwa? Kwa nini akampagaza mama yangu ubinafsi na wazimu uliomfanya kuiacha familia yake? Kwa nini akamtuma kijakazi Sauna kuja kuisambaratisha familia ya baba? Haya ndiyo aliyoyataka Mungu kwani, tangu nitoswe kwenye dimbwi hili, hakujatokea isimu ya mtu, hata dada yangu mpendwa Umu kuja kunitafuta. Sijawahi kuwaona maafisa wa usalama kwenye jumba la Buda wakija kuuliza kinachoendelezwa humo. Hata wanaofika humo huingia kwa tabasamu na kutoka kwa vicheko."

Mawazo hayo yalimpa Dick ujasiri zaidi, akapiga mbizi kwenye biashara hii kwa hamasa za ujana. Miaka mitano ya kwanza ilijaa hekaheka. Dick alisafiri kwingi na kuona mengi. Aliweza kuchuma pato si haba, pato ambalo aliliona

kuwa halali yake baada ya ulimwengu kumpoka maisha yake. Hata hivyo, wakati ulifika, akaamua kuwa hakuumbiwa uhalifu. Asubuhi moja akiwa chumbani, kwenye hoteli moja ya kifahari huko ng'ambo, dhamiri yake ilianza kumsumbua, moyo wake ukamsuta.

"Dick, hii kazi ni ya kujiumbua. Jitazame hapo ulipo. Umepata pesa nyingi katika umri mbichi. Lakini, je, una utulivu? Ni mara ngapi umeponea tundu la sindano kunaswa na mashine za forodha? Je, isingekuwa mwajiri wako kuvilainisha viganja vya maafisa wa forodha, wewe na wenzako msingekuwa mmeozea kwenye magereza ya kitaifa na kimataifa kama wengine wengi wanavyofanya? Unaweza kudai kwamba siku za mwanzomwanzo ulikuwa mnyonge, hukuwa na nyenzo za kukabiliana na mishawasha na vitisho vya mwajiri wako. Sasa umekia vilele vya anga, ukajifunza mbinu za kujiokoa. Kwa nini usijikwamue kutoka tope hili la uhalifu?"

Mawazo haya yalimsukuma Dick kufikia uamuzi wa mkataa, akajinasua kutoka kwa kucha za mwajiri wake huyu. Aliacha biashara hii haramu na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya umeme. Sasa ameanza kujitegemea, hasaa amejiajiri. Ameamua kufungua ukurasa mpya katika maisha yake. Amekwisha kuhitimu masomo katika chuo cha ufundi ambako alijifunza teknolojia ya mawasiliano ya simu. Ameweza kuyadhamini masomo yake kwa pesa ambazo alikuwa akidunduliza siku za biashara haramu na baada ya kujitegemea. Sasa amepanua mawanda yake ya kibiashara. Anauza vifaa vya simu. Husafiri ng'ambo mara kwa mara

kununua bidhaa ili kuyauzia mashirika yanayotoa huduma za mawasiliano.

******

Asubuhi hii ya umande Dick alikuwa katika safari yake ya kawaida; yeye na kijana mwenzake ambaye alikuwa mwajiriwa wa Dick. Alikuwa ameratibiwa kuabiri ndege ya saa moja asubuhi kuelekea ughaibuni ambako alizoea kununua mali yake. Hata alipokuwa akingojea kufunguliwa kwa afisi, fikira mchafukoge ziliivamia akili yake. Mawazo yake yalirudi nyuma, akayakunjua maisha yake ya siku za Mlima wa Simba. Alimuwazia mama yake kwa masikitiko makuu. Alishangaa jinsi ulimwengu unavyoweza kummeza binadamu, akawa hata hawawazii vifaranga wake! Fikira zilimkumbusha baba yake, akamwona katika dakika ya mwisho ya uhai wake, uso wake unaonyesha kuvunjikiwa, anamkazia macho na kumwambia,

"Dick mwanangu, walimwengu ni hasidi. Ndio walionisababishia uwele. Ishi, mwanangu, utawaona."

Machozi yalitaka kumtiririka Dick lakini akayakanya. Amezoea kufanya hivi katika miaka yote ya hamaniko. Anakumbuka ule msemo wa babake wa daima kuwa umaskini haupaswi kukabiliwa kwa kilio. Moyo wake ulimtuma tena kumkumbuka dadake Umulkheri. Anamwona Umulkheri, uso wake laini wenye imani. Anakumbuka alivyomwambia baada ya kutoweka kwa mama yake.

"Di, usijali. Mimi nitawakimu kwa viganja hivi vyangu. Hamtapungukiwa na lolote."

Dick alikuwa na maswali chungu nzima ambayo hayakuwa na wa kuyajibu, "Yu wapi kiumbe huyu? Alipatwa na yapi? Je,

na ndugu yangu mdogo? Ipi hatima yake? Yu hai? Je, aliweza kunasuliwa na yeyote kutoka mataya ya kijakazi Sauna?"

Wakati Dick akiwaza kuhusu familia yake, hakujua kwamba dadake Umulkheri alikuwa nyuma yake kapiga foleni. Umulkheri anasafiri ng'ambo kwa shahada yake ya uhandisi katika masuala ya kilimo. Siku zile baada ya kuchukuliwa na Mwangeka na Apondi, Umu alijifunga nira masomoni akafuzu vyema katika mitihani yake. Aliamua kuwa mhandisi katika uwanja wa kilimo; bila shaka anafuata nyayo za babake ambaye alikuwa mtaalamu katika uwanja huu. Daima mwana wa nyoka huwa nyoka na mwana wa mhunzi asiposana hufukuta! Safari ya Umu leo imesibu kisadfa tu. Alikuwa amepanga kusafiri wiki iliyopita lakini cheti chake cha usafiri kikawa kimechelewa; unajua hizi afisi za kimwetu za uhamiaji! Kilikuwa hakijatiwa sahihi na mzalendo mmoja.

Asubuhi Umu aliamka moyo wake ukiwa mzito. Anahisi kana kwamba anaiacha familia hii yake mpya bila matarajio ya kurudi. Anahisi jinsi alivyohisi alipokuwa anatoka Mlima wa Simba kuelekea jijini. Hata hivyo anapiga moyo konde kwani, kinyume na hapo awali, Umu anajua aendako. Anajua pia kuwa amejiambia kuwa baada ya masomo yake atawatafuta ndugu zake kwa msaada wa wazazi wake wapya. Japo hajawahi kusikia habari za ndugu zake tangu waondoke kwao, moyoni ana hakika kuwa wako hai.

"Maskini ndugu yangu mdogo! Maskini Dick! Binadamu waliwasokomezea wapi?" Umu alijisemea kimoyomoyo.

"Umu, ndege iko karibu kuanza safari," alisema Mwangeka, "ni vyema kuwaaga ndugu zako."

Dick aliyasikia maneno hayo akilini mwake kwa mbali.

"Umu?" aliwaza Dick, "amesema Umu? Nimewahi kulisikia jina kama hilo. Huyo si dadangu? La! Hawezi kuwa Umulkheri. Huyo tulimwacha kwenye Mlima wa Simba. Labda kijakazi Sauna alikwenda kumtupa kwenye lindi fulani la uhalifu."

Umu alinyanyuka kutoka kitini, akaenda alikokuwa mamake Apondi. Alimpiga pambaja katikati ya kekevu za kilio.

"Mwanangu Umu," alimkumbusha mama mtu, "mimi na babako hapa tumekulea kwa mapenzi. Tumekufunza njia za kukabiliana na mazingira mapya. Usiende huko Uzunguni ukasahau kilichokupeleka huko. Uzungu usikutie kizunguzungu ukasahau maadili tuliyokufunza. Mungu akujalie yote mema."

Ulikuwa wakati wa Mwangeka kumuaga bintiye. Alimshika mkono na kumwambia, "Siku tuliyokuja kukuchukua kutoka kwa Mwalimu Dhahabu ilikuwa siku ya heri kwangu. Nilihisi kana kwamba naja kumchukua marehemu mwanangu Becky. Umekuwa binti yangu wa kweli, rafiki wa dhati, msiri wangu. Hata ninapokupeleka ng'ambo najua kuwa utarudi nyumbani baada ya masomo yako. Sitasahau kamwe hisani yako na pendo lako la milele. Sitasahau ulivyokuwa ukiniambia, 'Baba, rudi duniani,' wakati ambapo uliona kwamba mawazo yangu yalikuwa yamekia vilele vya mbingu, wakati fikira zangu ziliponikokota kurudi kwenye masaibu yaliyoipata familia yangu ya awali." Baba mtu michirizi ya machozi ilimtoka njia nnenne, akaiachilia ikilovye kifua chake.

"Umulkheri, tutaku*misss* sana. Kwa nini unaenda? Mbona usisomee katika chuo kikuu cha hapa nchini?" alisema Sophie kwa sauti kubwa ya dhati.

Hilo lilitosha kumwamsha Dick kutoka lepe lake la muda. Aligeuka na kutazamana ana kwa ana na Umulkheri. Umulkheri alidhani anachezewa shere na macho yake. Mikono yake ilimwachilia dadake Sophie, moyo ukawa unamwenda mbio. Mwangeka ambaye alikuwa ameyaona mabadiliko yaliyomkumba Umu alimkaribia, akawa anamwangalia Umu, kisha yule kijana aliyekuwa anamkazia macho, anaona mshabaha kati yao, anataka kuamini kuwa huyu ndiye Dick ambaye Umu huwa hamtoi kinywani lakini anashindwa. Ghafla sauti kubwa ikasikika hewani.

"Umu! Dadangu Umu!" Aliita Dick na kukimbia alikokuwa Umu. Walikumbatiana kukutu huku wasafiri na aila yote ya Mwangeka ikiwatazama kwa mshangao. Milizamu ya machozi ilichimbuka kutoka visima vya kila mmoja wao, wakalia kimyakimya, wakiambiana kimoyomoyo yale yote yaliyowakumba. Hata waliposikia kwa mbali sauti ikitangaza kuwa abiria wanaoabiri ndege Tumaini waanze kuingia, walijua kwamba jaala ilikuwa imewakutanisha, kwamba hawatawahi kutengana tena.

Sura ya Tisa

Ewe chupa wangu ninayekuenzi
Kama mboni ya jicho langu
Mwendani wangu
Tazama
ulivyo shujaa
Asohisi shinikizo la majabali
ya mahangaiko
Ola jinsi ulivyonizingira
ukanijaza kwa tuo
maji matamu kunipa
yakawa dawa mujarabu
ya kuuguzia banguzi
walonisababishia mahasidi.

Chupa yangu, najua wananicheka hawa
wachunguliao kwenye madirisha
Walio kwenye roshani zao
Wakipunga pepo baada
ya kujaza matumbo yao
Sasa waole
Wananicheka
Wanasema,

"Mtazame Bwana Dengelua.
Anapita
na chupa yake kibindoni."

Lakini ...
Wewe hushangai?
kwani wanawashwa
Na pilipili iliyo
kwenye uchango wa mwengine?
Kwani wasitake kukuli
kilichotufanya mimi na wewe
kuwa marafiki wa kufa kuzikana?
Kwani wasimulize
alonirithisha huno mkanja?
kwa utu kunipoka
akanibakishia kaka,
La!
Kiunzi cha mifupa?

Wali wakifanyani?
Alipokuja Bwana Mabavu
shamba la asili akatwaa
ati ni yake milki
alonunua,
si kurithishwa,
na mkoloni?
Wali wakiwazani?
alipotuonyesha hatimiliki bandia
nasi mithili ya vifaranga,

waliomwona mwewe,
tukajikunyata kwa uoga
tusitoe hata kauli moja
kupinga ubahaimu huu?
Dhiki ya ukosefu ikatutuma
kuwa vibarua
Katika 'lake' shamba?

Wali wakifanya nini?
maskini babangu,
alipojipinda
kwa uzee kushika mipini
kujisulubu
kwa idhilali
na kuumbuka
kwenye shamba
la mwenyewe
riziki azumbue
karo alipe
masomo nipate
Moyo wake ukisema,
"Huyu ndiye mshumaa
unaotoa tumaini
la maisha ya neema
kwa aila hii?"
Kwani hakutokea mmoja
akamjuza baba,
"Shamba hili ni milki yako shaibu?"

Wali wakifanyani?
chuoni nilipokwenda
kwa matumaini makuu
ya kumvua babangu
kwenye bahari ya ufukara?
Wali wakiishi wapi?
chuoni nilipohitimu
kwa bashasha za ujana
misuli imetuna nguvu
kulihudumia taifa?
Kwani hawakunikabidhi kazi
walizoahidi kwenye mabuku?
Kwani hawakunipa nyenzo
za kujiendeshea maisha?
Kwani walitupuuzilia mbali
tulipolilia kuhiniwa?
Nafasi za kazi
zilipotwaliwa
na ndugu zao
Huku tukiambiwa kindanindani,
"Viganja huoshana,
aso mwana aeleke jiwe!"

Wali wakiwa wapi?
nilipopata gange, ya kufutia chozi?
Wali wakiwazani?
Mimi na wenzangu
tulipochanika
Kwa mishahara tumba?

Kwani hawakusikia rai yetu
tulipoomba mishahara kuimarika
Mahitaji kuyakidhi?
Kwani hawakumuliza
Bwamkubwa alosema
mikono kwenye nyongaye,
"Nyinyi ni *unskilled labourers,*
mishahara mlonayo,
ni kufu yenu?"

Wali wakisemani?
Nyoyo tulipotia ari
tukachachawa
tukasema tuna shahada
tukaomba kufikiriwa
kama wanataaluma wengine
nafasi za kupandishwa nyadhifa zilipopatikana?
Hawakututazama
kwenye runinga
tukifurushwa kutoka mabandani
ya kampuni
tulikopata sitara
ya nyani
mkia kukalia?
Ati kazi tumefutwa
kwa kuwazia kugoma
kuifilisi kampuni?

Wali wakifanyani?
nilipokugeukia wewe

mwenzi wangu wa pekee
kuniondolea uchungu
wa kufiwa na baba
kwa njaa?
Kwani hawakutuma
cha msada chakula
kikamwauni baba
kikamzuia
kubugia vijasumu
vya mizizi mwitu
Amekosa la mama
la mbwa akaamwa?

Muulize huyo mungwana
alo pale kwenye roshani
Kwani hata hakuwepo
hospitali ilipokosekana
kijijini mwa baba?
Dawa zilipokosekana
kwenye hospitali ya walalahoi jijini?
Baba asipate matibabu ya dharura
roho yake kuiokoa?

Waache wacheke wanaotucheka
Wanakicheka kilema
cha ufukara wa mali na utu
Ila hawa nakuhakikishia,
sahibu yangu
Hawafi,

Kama hakijawafika
Twende muhibu wangu chupa
Huenda tukampata Bi. Halua
ameambulia kibaba cha unga
kwa kidogo alichojitwalia
siku ya ujira huu wao wa tabu
kabla sijaja kukutafuta
tutumie fungu nililomkataza.

"Leo Shamsi anasikika kama amebadilisha wimbo wake," alisema Ridhaa kwa sauti ya chini, "huu wa leo unahisika kama wa kiumbe mwenye maumivu zaidi, mapigo yake hasa ni ya mbolezi, ni tofauti na yale majigambo yake ya kila siku," akaongezea Ridhaa huku akiyaghani majigambo ya Shamsi kwa sauti ya chini kama anayeyatia maneno ya majigambo yenyewe kwenye mizani.

"Hawa wanifuatao wananicha
kwa ukoo wangu mtukufu
Kwa jadi yenye majagina
wa mioyo na vitendo
Wananicha
kwa kuwa wa kwanza kijijini
kuvishwa taji
Kwa mabuku kubukua
Kwa kuwa jogoo wa kwanza
Kuwika kwenye anga za ilimu
idhini nikakabidhiwa,
ya tafiti kuendeleza

mamlaka nikapawa,
Ya kuwaza kwa niaba ya jamii.

Hawa wanifuatao
wananicha
Kwa kuweza
kuvyaza mikakati
ya kukabiliana
na ulitima walonipagaza
kwa ndoto zangu za ujana kuzima.

Nani asiyejua
Bwana Shamsi ambaye
wapiga mikanja wengine
wakifa na kupofuka
kwa kufaidi dengelua
Ilotiwa vijasumu
kusudi iive haraka,
yeye huinukia kuwa simba
roho anaishikilia kukutu
na kuzidhihaki
nguvu za dengelua?"

Ridhaa anamtazama Shamsi akipita hapa kama afanyavyo kila siku. Mtaa anakoishi Shamsi si mbali na hapa, unaweza kusema Shamsi na Ridhaa ni majirani. Hili la kuwa jirani wa Shamsi limetokea baada ya miezi mingi ya fikira na tafakuri. Kwa kweli huu ni mwezi wa tatu tangu Ridhaa kuhamia kwenye mtaa wa Afueni. Afueni ni mtaa wa raia wenye kima

cha juu kiuchumi. Mtu anapoutazama mtaa huu husalimiwa na majengo ya kifahari ya ghorofa, yale ambayo yanaitwa katika janibu hizi *town houses*. Daraja kubwa limeutenga mtaa huu na mtaa wa Kazikeni ambako ndiko familia ya Shamsi na nyingine za aina yake zinapoishi. La! Haziishi, zinaambulia maisha ya kubahatisha tu. Ni mtaa wenye mabanda akthari yaliyojengwa kwa udongo na mabati.

Baada ya kushuhudia kuzaliwa kwa mjukuu wake wa mwisho, Ridhaa aliona kwamba maisha ya Mwangeka yameanza kutengenea. Ile barafu ya hamaniko aliyokuwa nayo Mwangeka ilikuwa imeanza kuyeyushwa na pendo na ushirika wa mkewe Apondi. Sasa Ridhaa aliwaza kuwa huu ulikuwa wakati wake wa kuanza kuyajenga maisha yake upya kama buibui ajengavyo tandabui.

"Mwangeka," aliita Ridhaa jioni moja, "miaka kadha imepita tangu urudi nyumbani. Nimeshuhudia maisha yako yakijengeka upya, hasa baada ya ndoa yako. Huenda ufa aliokuachia moyoni mkeo wa kwanza hautawahi kuzibika. Ila naona sasa maisha yako yametengenea. Mungu amekufidia si haba. Wewe, mkaza mwanangu na wajukuu wangu mmekuwa wenzi wa kutegemewa. Ila sasa nahisi kwamba muda wangu wa kuanza kuyajenga upya maisha yangu umewadia."

Mwangeka alitabasamu na kusema, "Baba, usiniambie moyo wako umeanza kukubali waridi la kuufariji na kuupumbaza!"

"La! La! La mwanangu! Hayo unayoyawazia siyo, ila naona ni muhimu nihamie ile nyumba yangu ya Afueni. Nimeisha kulipa ilani shirika lililompangia Afisa Mkuu Mtendaji wake

jumba hili. Nadhani ni muhimu nianze kuizoea hali hii yangu ya ujane. Ikitokea kwamba moyo utanituma kupenda tena katika machweo ya maisha yangu, basi nitakuwa radhi kuupa nafasi msukumo huo. Kwa sasa azma yangu kuu ni kumalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya nilichokijenga kwenye lile ganjo letu. Haidhuru kwamba humo ndimo mlimoangamia familia yangu. La muhimu ni kwamba kituo hiki kikikamilika kitawafaa raia wengi ambao hawamudu gharama ya matibabu katika hospitali za kibinafsi na wengine hata hospitali za umma."

"Basi, *Doc*, nakubaliana na rai yako," alisema Mwangeka huku amemshika babake begani na tabasamu kuutawala uso wake.

******

Selume alishusha pumzi baada ya kumhudumia mgonjwa wake wa mwisho. Akrabu ndogo ya saa ya ukutani ilisimama kwenye nambari moja, na ile kubwa kwenye nambari kumi na mbili. Zamu yake ya leo imekamilika na yu tayari kumpisha muuguzi mwenzake. Ingawa hii ni kazi ileile aliyokuwa ameifanya kwenye hospitali ya umma kwa miaka na mikaka, anaona hali katika kituo cha afya cha Mwanzo Mpya ni bora mara mia kuliko ilivyokuwa katika hospitali ya umma. Hata Selume anapowazia maisha haya yake mapya, hajui jinsi alivyoweza kuyastahimili makeke katika hospitali alikokuwa akifanya kazi awali. Ile hali ya kumtazama mama mwanagenzi akitapatapa kwa uchungu wa mwana, moyoni anaomba kitoto kikawie kwenye mji aweze kujinunulia glavu za kumhudumia mama mzazi. Zile 'Msalie Mtume' za mama mwanagenzi,

zingizi la baada ya uzazi limemkaba, naye Selume hana dawa wala kafara ya kumpoza mwili na roho mama huyu. Kule kulazimika kupapasa kwenye giza kutafuta dawa za mgonjwa, umeme umekatika ghafla, usimamizi wa hospitali haujalipia gharama yake, na wale wanaostahili kushughulikia dharura hii wametoweka ... Yote yalimpa hamaniko kuu. Sasa haya ameyapa kisogo. Kwa Selume, kufunguliwa kwa kituo hiki ni kama mana iliyomdondokea kinywani kutoka mbinguni. Alikuwa tayari amewazia kujiuzulu kwa kusinywa na aliyokuwa anayaona.

"Nimechoka," alijisemea siku moja, "nimechoka kuwatazama wagonjwa wakifa kwa kukosa huduma za kimsingi huku shehena za dawa zilizotengewa hospitali hii zikiishia kwenye maduka ya dawa ya wasimamizi wa hospitali. Nimechoka kuongolewa kwa wimbo wa *performance contract*. Ati, 'Kufikia mwisho wa mwaka huu, tutakuwa tumeimarisha kampeni dhidi ya polio na kuwachanja watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano. Tutakuwa tumejenga vituo zaidi vya kutolea huduma za ushauri katika kila eneo la ugatuzi ili kuwasaidia walioathiriwa na ugonjwa wa UKIMWI na saratani kukabiliana na changamoto za maisha.' La kushangaza ni kwamba hata chanjo ya polio yenyewe inauziwa maskini ambao hata hawamudu kujilisha! Kufikia lengo lenyewe la kuangamiza polio kunabakia kwenye ndoto za wanaozindua kampeni zenyewe. Tazama pia dawa za kukabiliana na makali ya UKIMWI na saratani. Wanaoweza kuimudu gharama yazo ndio hao hao wanaozinyakua dawa zilizotengewa raia wasiojiweza."

Mambo ya sudi huenda kwa sudi. Wakati Selume akiwazia kustaafu mapema, naye Ridhaa ndipo anapomalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Nafasi za kazi zilipotangazwa, Selume na Kaizari waliomba kazi, Selume akaajiriwa kama Muuguzi Mkuu, naye Kaizari kama Afisa wa Matibabu. Huu ni mwaka wa tatu tangu kuanza kazi hapa chini ya usimamizi wa Ridhaa ambaye ndiye mkurugenzi.

"Huyu hapa ameletwa na Wasamaria wema leo asubuhi," Selume alimwambia Meko, muuguzi mwenzake, huku akimwashiria mgonjwa mwanamume aliyelala chali kitandani, kichwa kimejaa mabendeji yaliyolemazwa na damu. "Inasemekana alivamiwa na kuumizwa kwenye ule mgogoro wa kupigania ardhi katika eneo la Tamuchungu. Hali yake sasa si mbaya ila anahitaji uangalizi wa makini."

"Sawa," aliitikia Meko huku akiiandika habari fulani kwenye kijitabu kidogo alichokibeba.

Selume na Meko walitembea hadi kwenye kitanda kilichokuwa mkabala na hicho, wakafungua pazia na kuingia ndani. Walimpata mwanamke fulani akipigana na iziraili kuiokoa roho yake. Hata hivyo, inaonekana kwamba walikuwa wamechelewa. Selume alikishika kiwiko cha muwele huyu, akasikiza mpigo wa moyo na kutikisa kichwa.

"Naona tumempoteza huyu pia," alisema huku akimtazama Meko.

"Je, ni yule aliyeletwa usiku wa kuamkia jana?" aliuliza Meko.

"Ndio. Sijui kwa nini watu hawa hawajifunzi kutokana na majanga yanayowakumba wenzao. Nashangaa kinachompa kijana kama huyu, na wengine waliofariki jana, ambao

wanasomea shahada za uzamili, kujihusisha na unywaji wa pombe haramu!"

"Nasikia wanalewa kujipurukusha na hali duni ya maisha vyuoni. Wanasema kuwa gharama ya masomo imekuwa ghali, nayo halmashauri ya elimu inayotoa mikopo ya masomo haimudu kutosheleza mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitaji mikopo na ruzuku. Isitoshe, nasikia kwamba wanaoishia kupewa mikopo au ruzuku hizi ni watoto kutoka familia zinazojiweza kiuchumi huku wana wa maskini wakilazimika kufanya vibarua wakati wa likizo kujilipia karo na kugharamia mahitaji mengine. Wengine huwa mawindo rahisi ya matajiri wanaotafuta roho za kulangulia na kusafirishia dawa za kulevya ughaibuni," Meko akachangia.

"Ni hali ngumu sana Meko," aliongeza Selume, "na usidhani wanaotumia vileo vibaya ni wale tu wanaotaka kujipurukusha na hali duni chuoni. Wapo wanaovitumia ili kujisahaulisha kusambaratika kwa familia zao. Kuna huyo kijana, Kipanga, anayepokea huduma za ushauri-nasaha hapa petu. Yeye alinusurika kifo kutokana na kangara iliyowaua watu sabini mwezi uliopita. Huyu anasema kwamba alianza kuchovya kidogokidogo akiwa kidato cha pili baada ya aliyedhania kuwa baba yake kumkana, na kulazimika kuhama alikoita kwao, yeye, mama yake na mnuna wake ambaye alisemekana ndiye mwana halisi wa baba yake. Kipanga anasema kwamba lililomuuma zaidi ni kwamba alipomtaka mama yake kumwambia ukweli, mama mtu hakumpa jawabu la kuridhisha. Alichosema ni, 'Yapo mambo ambayo mtu hawi na uso wa kumtazamia mwanawe kwayo. Anayekulea ndiye mzazi wako, mradi tu akubali kuwajibikia ulezi.'

"Kipanga sasa ameanza kuuhuisha utu wake. Anasema amemsamehe mama yake, amemsamehe baba mlezi ambaye alimkana katika kipindi ambacho alikuwa akisaka ujitambuaji. Anasema atarudi shuleni akamilishe masomo yake," Selume aliukamilisha usemi wake na kumwelekeza Meko kwenye kitanda cha mgonjwa mwingine wa kike.

"Hujambo Tuama? Unajihisi vipi?" aliuliza Meko kwa tabasamu.

"Sijambo, nimepata afueni," alijibu Tuama kwa sauti hafifu.

"Una bahati sana Tuama, hukufikwa na yale yaliyowafika wasichana wenzako," alisema Selume, "tunamshukuru Mungu kwamba amekuokoa. Hii ni fursa nzuri kwako kuwaelimisha wanafunzi wenzako dhidi ya kufuata mila zilizopitwa na wakati."

Tuama aliinuka kitandani alikokuwa amelala, akaketi na kumtazama Selume kwa jicho la kubisha.

"Kupashwa tohara si mila iliyopitwa na wakati. Bila tohara mwanamke hubakia kuwa mtoto. Nisingepashwa tohara nisingeolewa. Msiba uliowapata wenzangu ni bahati mbaya tu," alisema Tuama.

"Kifo ni janga kubwa Tuama," alisema Meko, "wenzako hao walipukutika wakati ambao jamii yao inawahitaji mno. Walihitaji kukamilisha masomo yao, wapate kazi, waweze kuchangia katika maendeleo ya kitaifa."

"Lakini kupashwa tohara hakumaanishi kuacha shule. Dadangu Hazina alipashwa tohara lakini sasa amehitimu shahada katika chuo kikuu. La muhimu ni mtu *kujifocus*

kwenye malengo yake tu. Mimi najua kwamba japo nimepashwa tohara, baada ya kupona uwele huu, nitaendelea na masomo yangu," alijibu Tuama.

"Ni kweli msichana anaweza kupashwa tohara na kuendelea na masomo. Lakini mara nyingi hali haiwi hivyo. Wasichana wengi huozwa au kuolewa kwa hiari mara tu wanapopashwa hiyo tohara. Si wazazi wengi walio na muono kama baba yako. Kumbuka wewe ulijificha tu ukaenda kupashwa tohara. Baba yako hakuridhia jambo hili. Isitoshe, kuna hatari ya kuambukizwa magonjwa ambayo hayana tiba, au kupoteza damu nyingi kama ulivyofanya wewe," alisisitiza Selume.

"Ni kweli asemavyo mwenzangu," alisema Meko, "Tuama, unaweza kutumia hali iliyokukumba kuwashauri wasichana wa rika lako dhidi ya kushiriki mila ambazo zinakiangamiza kizazi chenu. Kwa vile wewe ni mwenzao, utakuwa na ushawishi mkubwa kuliko hata kikundi cha kupigania haki za kibinadamu kijijini mwenu ambacho kiliasisiwa na babako Mzee Maarifa."

Tuama alishusha pumzi ndefu, akatikisa kichwa na kusema, "Nitajaribu, ila najua kwamba hili litanifanya kutengwa na wenzangu ambao kwa kweli ndio walionishinikiza kupashwa tohara. Sijui kama baba yangu atawahi kunisamehe kwa kumuasi."

"Atakusamehe. Mwana akinyea kiweo hakikatwi," alisema Selume huku akimwashiria mwenzake waondoke wamhudumie mgonjwa mwingine.

"Huyu hapa anaendelea kupata ahueni," alisema Selume huku akimwashiria kwa kidole cha shahada mgonjwa mmoja

aliyekuwa pembeni mwa chumba, karibu na dirisha la wodi ya wanawake.

"Pete, unajihisi vipi?" aliuliza Meko, muuguzi mwenzake Selume.

"Sijambo," alijibu Pete na kukigeuza kipaji chake kuelekea ukutani.

"Maskini, inaonekana umemtonesha kidonda," alisema Selume huku akitikisa kichwa, "inasikitisha sana kumwona mtoto mbichi kama huyu akijaribu kujiangamiza pamoja na kitoto alichokihimili."

"Nadhani la muhimu ni kwamba Pete na kitoto chake wameokolewa. Analohitaji zaidi ni ushauri wa kumwezesha kukabiliana na hatima ya tendo lake hili, hali inayomzunguka, pamoja na unyanyapaa unaoweza kuandamana na kitendo chake," alisema Meko.

"Hali inayomzunguka! Mtu utawezaje kujua hali inayomzunguka mwingine na hali huishi katika hali hiyo," alijiuliza Pete, "ama ni ile hali ya mzigo wa mwenzio na kitanda usichokilalia? Hawa wauguzi kweli hawajui lolote. Hawajui linalompa mama kutaka kujitoa roho huku akijua kwamba anawaacha wanawakiwa wawili. Hawajui, hawajui kabisa. Na watajuaje na lao ni kushika zamu tu, kumlazimisha muwele huyu kumeza vidonge vichungu vya dawa, kufunga bendeji donda hili, kutia kitata mkono huo uliovunjika, kutazama zebaki ya kipima joto ikipanda na kushuka, kukishika kitoto kijoga viguu kidungwe sindano, kuwatazama binadamu wenzao wakiwana na kutoa jasho kupambana na iziraili anapokuja kubwakura nafsi zao, na hatimaye kuwafunika kwa shuka nyeupe waliotokwa na roho zao?"

Pete alizisema kauli hizi mfululizo mawazoni mwake, akajipindua na kuketi katikati mwa kitanda chake cha uwele huku akiwatazama Selume na mwenzake kwa imani. Gharika ya machozi ilivunja kingo za mto wa machozi yake, yakaanza kutiririka kama maji kwenye mlima. Katikati mwa kilio hiki, Pete alifungua pazia la jukwaa la maisha yake, akaanza kuwasimulia kina Selume kisa chake mawazoni kimya kimya, moyoni akisema kwamba huenda wakakielewa kiini chake kutenda alichotenda.

"Nilizaliwa katika kijiji cha Tokosa. Mimi ndiye mtoto wa nne katika familia yenye watoto sita. Nina wazazi wawili, ila hawa ni wazazi tu, hawajadiriki kuwa walezi wangu, wala jina 'mlezi' haliwaafiki. Naona mnaniuliza vipi mtu kuwa mzazi na asiwe mlezi. Ila nataka mjue kuwa haya hutokea mara nyingi. Hamuwezi kujua haya nyinyi, yaonekana mlilelewa kwa *Nun* na *Cerelac*, hamjaonja shubiri ya maisha. Mara tu macho yangu makinda yalipoanza kuutambua ulimwengu, nilijipata kwenye boma la bibi mzaa mama, kisa na maana, kumetokea mtafaruku fulani kati ya baba na mama. Sijui ni mtafaruku wa aina gani, ila katika pitapita zangu kijijini mwa bibi, alitokea domo kaya fulani akaninong'onezea kwamba sikuwa na mshabaha hata chembe na baba. Nilishangaa ikiwa kutoshabihiana kwa mtu na mmoja kati ya wazazi wake ni mizani tosha ya kupimia kukubalika au kutokubalika kwa mtu katika familia yake. Basi huyo huyo aliyeniambia hayo alidhukuru kusema kwamba mama mtu, kwa kuchelea kuingiza kitumbua cha ndoa yake mchanga, alihiari kumpagaza mama yake mzigo wa malezi. Hapa mnionapo, sijadiriki kuonja tamu ya kupendwa na wazazi wangu.

Nimemjua mama kama mhisani wa muda ambaye alikuwa akipita mara mojamoja kwa bibi kumpa pesa za kukidhia mahitaji yangu na ya bibi. Sidhani kama moyo wa mja huyu uliwahi kutaka kujua lolote kuhusu ukuaji wangu. Sikumbuki hata siku moja akiniuliza kuhusu neema na mashaka yangu shuleni. Hata alipoona kwamba bibi anamtaka kununua sare nyingine kila baada ya miezi michache—ya awali imeanza kuukataa mwili wa mwanawe—haikumpa kuwaza kuwa kima cha mwanawe kimeanza kuwanda, nayo maumbile yameanza kufanya kazi yake.

"Sijui kama umepata kuwazia hili, umeingia darasa la sita, ni asubuhi, unataka kuondoka nyumbani mwa bibi yako kuelekea shuleni, kisha unashtukia kwamba unakabiliana ana kwa ana na hedhi yako ya kwanza. Hujawa na mama wala dada wa kukujuza ya kufanya litokeapo la kutokea. Unamwendea ajuza huyu ambaye amegotama kwa uzee, naye, kwa yale mazoea yao ya jadi, anakutafutia tambara la blanketi, ndilo sodo! Sijui hali ikiwa hivi wewe utafanya nini, lakini ninalokumbuka ni kwamba nililitwaa hilo tambara, likawa ndilo fimbo ya karibu. Na usidhani hili lilifaa kitu, kwani baada ya muda si muda, nilihitaji kutafuta njia nyingine ya kujikuna nijipatapo; kikawa kivangaito cha kutafuta kanzu hii na ile kuukuu kujifadhilia. Hata mahangaiko haya yalipokwisha, juma zima lilikuwa limepita, darasa halijakilimbuka hata kivuli changu.

"Maisha yangu yalichukua mkondo mwingine nilipojiunga na darasa la saba. Katika jamii yangu, inaaminiwa kuwa msichana akiisha kupashwa tohara, ameingia utuuzima, hivyo ataipaka familia yake tope ikiwa ataendelea kuozea kwao bila mume. Wajomba zangu hawakuchelea kupokea posa

na baadaye mahari kutoka kwa buda mmoja ambaye alinioa kama mke wa nne. Bibi alijaribu kupinga,

"'Huyu mtoto ni mbichi mno,' alisema, 'hatuwezi kumkabidhi mzee wetu huyu kifaranga kiteketeke hivi, tutakuwa tunampagaza ulezi. Isitoshe, Pete mwenyewe ana hamu kuu ya kufuatilia elimu, tumwache aizime kiu yake. Akiisha kutimiza maazimio yake, atajichagulia kijana mwenzake wafunge nakidi.'

"Maneno ya bibi yaliangukia masikio yaliyotiwa uziwi. Mama na ndugu zake hawa walikuwa wameamua, na tangu hapo, kama alivyosema mama, nyanya hakuwa na mamlaka ya kutoa uamuzi wowote kuhusu maisha yangu.

"Maisha yangu na Fungo yalikuwa kama ya ng'ombe aliyetiwa shemere na kufungwa nira pamoja na punda ambaye anakaidi kusonga. Ule unene wake, lile kutuzi lililotoka kwenye makwapa yake makuza na kufudikiza kote chumbani, ule wivu wa mke mwenzangu wa pili, kule kukemewa na kuchekwa na wana wa mke wa kwanza ... yote yalininyong'onyeza na kuniumbua. Nilichukia jaala iliyonipa mama anayejali masilahi yake tu, nilichukia nguvu ya maumbile iliyoniweka kwenye jinsia ya kike, nilikichukia kitoto nilichohimili kwenye mji wangu ... Hata miezi tisa ilipotimia na kupata salama, niliamua kwamba kwa Mzee Fungo hakuniweki tena.

Na unadhani unakwenda wapi? Utawezaje kujitunza wewe na mtoto wako na hali bibi yako ndiye huyo, hana hanani, na wazazi wako walafi walikuuza kwangu ili wapate pesa za kuwasomeshea ndugu wako watano wa kiume?' aliuliza Fungo.

"'Nitatokomea kokote kule. Afadhali kuishi jehanamu kuliko kwenye husuni hii yako. Hata mitaa ya miji imejaa familia zisizo na asili wala fasili,' nilimwambia Fungo.

"'Basi nenda mwanakwenda,' alisema Fungo, 'kichukue pia kijalaana hiki chako, hata kuwepo kwenu hapa hakuzidishi hakupunguzi. Tayari nina jeshi tosha la watoto kutoka kwa wake wangu watatu.'

Niliifungia kifuani mbeleko iliyokibeba kitoto changu na kuondoka kwa Fungo bila kutazama nyuma, tayari nimepoteza miaka minne ya ujana wangu. Nilijitoma jijini kuzumbua riziki kama wafanyavyo wengine kama mimi. Kazi yenyewe usiniulize ilikuwa ya aina gani kwani wewe mwenyewe unajua wanazopata watu wenye kitembo duni cha elimu. Niliambulia kibarua cha kwanza kwenye kampuni ya kutengenezea sare za shule, na za wafanyakazi wa umma. Kampuni hii ilimilikiwa na Mhindi mmoja. Kazi yangu na wengine kama mimi ilikuwa kushonea vifungo kwenye sare hizi. Ni kazi iliyomhitaji mtu kuamka kabla ya jimbi la kwanza ili kuwahi kibarua cha siku kabla lango la Patel halijafungwa, na kuondoka saa kumi na mbili jioni.

"Ujira wangu ulikuwa shilingi mia mbili kwa siku. Huenda ukataka kujua jinsi mtu anavyoweza kuishi kwa ujira wa aina hii. Hata hivyo fahamu kwamba mara zote binadamu huhitajika kujikuna ajipatapo; nami nilijaribu kadiri ya uwezo wangu kudunduliza pesa hizi ili kukikimu kitoto changu. Ndizo zilizonunua maziwa ya mtoto, ndizo zilizolipa kodi ya ujima kwenye kibanda tulimoishi mimi na wenzangu wanne, ndizo zilizokuwa kiinua mgongo kwa msichana mdogo aliyejisabilia kunitazamia kitoto nikiwa kazini.

"Kadiri siku zilivyosonga, ndivyo nilivyoanza kujua mizungu ya mji. Haikuwa vigumu tena kwangu kukubali 'zawadi' za pesa za kufutia machozi kutoka kwa mibaba iliyodai kukionea imani kitoto changu. Sikuipenda hali hii ya kuwa mtegemezi lakini sidhani maskini huwa na hiari. Hata baada ya mwaka alitokea mwanamume mmoja na kudai kuwa ananipenda, kwamba angependa tujaribishe maisha, kisha tufunge akidi baada ya miezi mitatu.

"Sijui kama umewahi kujawa na hisia za kukataliwa, ukajihisi kama mkoma aliyesiribwa kinyesi usoni?' nilijiuliza huku nikiwatazama akina Selume na mwenzake kana kwamba ninataka kuiona taathira ya maneno haya machoni mwao.

"Basi hisia hii ndiyo iliyonifanya kuyaamini maneno ya Nyangumi; nikahamia kwenye chumba chake kimoja cha mawe. Hiki nilikiona afadhali kuliko kile chetu cha udongo. 'Angaa kitoto changu kitaweza kuishi maisha ya staha,' nikajiambia.

"Zao la muungano huu lilikuwa kuzaliwa kwa mwanangu wa pili. Huyu yumo mtaa wa Sinyaa ambako nilikuwa ninaishi baada ya kupigwa pute na Nyangumi, mkewe wa halali amemrudia. Analelelewa na ndugu yake. Inabidi hali iwe hivi kwani sina pesa za kumlipia kijakazi, na vinywa hivi viwili lazima vilishwe. Na usidhani hata kitoto hiki cha pili sikujaribu kukiangamiza. Kwa kweli ukaidi wa kijusi chake ndio mwokozi wacho. Nilikuwa nimejaribu mara nne kukiavya kwa vidonge, kisikubali. Mwishowe nilimwendea daktari ambaye, badala ya kunisaidia, alikilaani kitendo changu na kuniambia kwamba nisimtie katika majaribu.

"Hiki kilichonilaza hapa nacho kina roho zaidi ya saba. Ni kijalaana ambacho nilikiokota katika shughuli za uuzaji pombe. Nadhani mmoja kati ya walevi waliozoea kuja kwenye baa nilimoajiriwa kuuza pombe aliniwahi nishai zikiwa zimenilemea, yakatokea ya kutokea, akaniachia ujira wangu na kiafriti hiki. Fikira ya kuwa na vitoto vitatu hata kabla ya kufikisha umri wa miaka ishirini na mmoja ndizo zilizoisumbua dhamiri yangu. Na liwe hilo la kuwa mzazi mchanga, lakini, watoto wenyewe kuwa wa baba tofauti! Isitoshe, maisha yenyewe ni ya kupapatisha, sina kazi ya maana wala kisomo!

"Asubuhi hii fikira zilikuwa zimenijaa kifua tele, nikaona kwamba ni heri niyaangamize maisha yangu. Nilimwambia jirani yangu anichungie wanangu, nikaacha kikaratasi chenye anwani ya bibi yangu juu ya kimeza kidogo katikati mwa chumba changu na kuondoka.

"'Ikiwa dawa ya kutibia maradhi ya binadamu ilishindwa kutungua mimba ya pili, hii ya kuulia panya haitashindwa kunifisha mimi pamoja na kilichomo tumboni,' nilisema haya na kumiminia kopo la dawa hii kinywani.

"'Usinitazame kana kwamba unataka nikwambie yaliyotokea baadaye,' nilijisemea kana kwamba ninajibu mtazamo wa Selume, 'nyinyi ndio wa kuniambia kwani nilijipata hapa penu,'" Pete aliongezea na kukatisha ghafla usimulizi uliokuwa mawazoni mwake.

******

"Mawio ya leo yanaelekea kuwa na kiza kisicho cha kawaida," anajisemea kijakazi Sauna huku akijipindua kuusikiliza

mlio wa king'ora unaosikika kwa mbali. Anaenda miayo na kujikokota kutoka kitandani. Maungo yake ambayo daima huwa mepesi yanahisika kuwa mazito kama nanga. Anatamani kurudi kitandani alale lakini inabidi amtayarishie Bi. Kangara kiamshakinywa; ana miadi ya mapema na mzalendo mmoja jijini. Sauna anaingia jikoni na kujifunga kimori, tayari kuanza kuchoma mandazi. Mara moyo unaanza kumwenda mbio na vipapasio vya akili yake kusimama wima. Anajihisi kama anayetarajia kuanza kinyang'anyiro kikali cha upiganaji masumbwi. Kwa mbali anasikia mbisho hafifu langoni mwa jumba hili. Anatoka nje kwenda kuitika mbisho huu. Ghafla, uso wake unakumbana ana kwa ana na polisi! Mara anasikia moyo wake ukimwambia, "Yako ya arubaini imefika," huku akijaribu kuvaa tabasamu na kuwakaribisha maafisa hawa nyumbani.

Hii ni wiki ya pili baada ya Sauna kuwatorosha Dick na Mwaliko. Amefanikiwa kumbadilisha Dick kwa kitita cha pesa.

"Dick sasa ni mali ya Mzee Buda. Yatakayomfika ni yake na malaika wake,"aliwaza Sauna siku hiyo.

Mwaliko naye amepelekwa kwa Bi. Kangara, apate mbavu kidogo, kama asemavyo bibi huyu, kisha atafutiwe cha kufanya. Sauna ameisha kupata ujira wake kwa kazi hii pia, na yu tayari kuondoka asubuhi ya kuamkia Krismasi. Hata Sauna anapowazia matendo yake, hasa ya hivi majuzi, anatamani kujisuta. Anahisi kwamba hafurahii kazi hii yake. Hata hivyo, ndani ya nafsi yake anaukemea moyo wake ambao unataka kuipweza ari yake.

"Mlaani shetani," Sauna aliuambia moyo wake, "unajua kwamba mimi sikuumbiwa ujalaana, walimwengu ndio walionifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari. Fikiria wewe, u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kisha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna hata uso wa kumtazamia yeyote, wala kinywa cha kumwambia mama yako kuhusu feli uliyotendewa. Na utamwambia vipi mja huyu na daima yeye ni mwanamke taa, atakalo baba yeye huliridhia bila swali, na ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde, vitisho na matusi? Hebu yatie haya kwenye mizani; baada ya mwezi mmoja unaanza kushikwa na kisulisuli, kichefuchefu cha asubuhi nacho kinakuandama. Fikira zako za kitoto zinakutuma kuwaza kuwa ni malaria au homa ya matumbo. Unamwambia mama yako ambaye anaonekana kushtuka kiasi. Mama anapokupeleka hospitali anapasuliwa mbarika, nawe limbukeni hujui lolote. Mnapofika nyumbani anakuhoji, nawe hujui kuficha lolote, unamwambia imekuwa mazoea baba yako kukuhujumu kila apatapo nafasi.

"'Hili haliwezi kukubalika! Kujipagaza uzazi na ulezi katika umri huu, tena mzazi mwenzio si mwingine, ila baba yako? Lazima nitatue haya kabla wenye macho hawajaanza kuona,' sauti ya mama yenye uchungu na kuvunjikiwa inasikika.

"Moyo wangu, uchungu na kukata tamaa kulikonikumbatia nilipotoka hospitali hakuwezi kumithilika. Sikuweza kuamini kwamba mama yangu angekuwa amrijeshi wa mauaji. Maskini kitoto changu kilitunguliwa kabla hata hakijaumbika.

Linalonikatakata maini zaidi ni kwamba mama alinionya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama wa baba.

"'Mwanangu,' alisema mama huku kilio kimemvaa, 'usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakukuzaa wewe. Ndiye aliyenivua kutoka kwenye umaskini alionipakaza baba yako mzazi baada ya kujizika kwenye unywaji wa dengelua mitaani na kujisababishia kupigwa kalamu. Msamehe Bwana Maya, hakuna mja aliyekamilika.'

"Maneno haya ya mama mzazi yalinitonesha jeraha zaidi. Nilijua kwamba mama alikuwa mjane wa Bwana Kero, lakini haya ya kuwa Bwana Maya si baba yangu hayaaminiki. Kiumbe huyu alimkimbia baba yangu hata kabla hajafikwa na mauti? Nilimaka sana. Baada ya tendo hili la mama niliamua kwamba nyumbani pa Maya hapaniweki tena. Nilitaka kutokomea popote pale. Sikuwa na cha kujivunia. Sikuwa na utu. Heshima yangu kwa mama na kwa Bwana Maya walikuwa wamekwisha kuisagasaga. Usuli niliokuwa nimejivunia ulikuwa umetokea kuwa bandia. Sikuwa na matumaini wala hamu ya kuendelea na masomo yangu baada ya kuhujumiwa kimapenzi na kihisia.

"Asubuhi moja mbichi ilinipata kwenye baraste kuu; nimeamua kutamba na ulimwengu. Nimefanya kazi katika machimbo ya mawe, nimewahudumia waungwana kwa namna zote katika majumba ya kuuzia pombe, nimeuza maji ya mito na madimbwi yaliyotiwa kwenye chupa zenye vibandiko vya kuvutia, ati ni *mineral water* ... Sijui ni mangapi sijafanya katika sayari hii hadi pale alipotokea mja huyu wa

imani—Bi. Kangara—ambaye alinifunza mbinu mpya za kujinyanyua. Nayakumbuka maneno yake vyema:

"'Wenye hadhi na mali wanahitaji wafanyakazi wa kuwaendelezea biashara zao. Nawe ninavyokuona ni mhitaji, mkulima hasa ambaye hastahili kuchagua jembe. Pana soko kubwa la binadamu katika mitaa ya watu wa kimo wastani kiuchumi. Hawa wana familia changa zinazohitaji ulinzi wa vijakazi. Unajua tena kuwa wanawake siku hizi wamejitia kiguu na njia kuwasaidia waume zao kuzikimu familia zao. Wengine wanajitia kufanya kazi ili washindane na waume zao tu. Njia mufti ya kufanikiwa katika biashara hii ni kujitia unyenyekevu, kufanikiwa kuwaaminisha waajiri wako kuwa unavipenda vitoto vyao, hata vile ambavyo havipendeki. Hili litakupa nafasi ya kuwateka watoto hawa. Soko ni pana, mwanangu; wanunuzi ni wengi kuliko bidhaa zenyewe.'"

Sauna aliianza kazi yake. Ni kazi ambayo ilimpa pato kubwa sana, hata akataka kuyasahau yaliyopita na kuwasamehe walezi wake. Hata hivyo, kadiri alivyopata ndivyo tamaa ilivyozidi kuwanda. Hatimaye ulanguzi wa binadamu uligeuka kuwa ngozi yake. Na sasa yu tayari kushika tariki kutekeleza utumwa mwingine wa Bi. Kangara.

Safari yake ilipata mkondo mwingine baada ya polisi kupata fununu kuhusu njama ambazo yeye na Bi. Kangara walikuwa wakiendesha. Mabibi hawa walikuwa na mtandao ambao kazi yake ilikuwa kuwauza watoto na vijana. Bi. Kangara ndiye aliyekuwa kinara wa mtandao huu. Huyu aliishi katika mji wa Ghushi. Sauna alikuwa mmojawapo wa mawakala wake wa mashinani, *Grassroot Agents,* kama alivyowaita Bi. Kangara. Kupitia kwa juhudi za Sauna na wengine Bi. Kangara alifanikiwa kupata wasichana wa kuuza katika madanguro,

wavulana wa kuwapelekea matajiri ambao walishiriki katika ulanguzi wa dawa za kulevya, na wafanyakazi katika makasri ya matajiri, na katika mashamba ya mikahawa na michai. Wengine walisafirishwa ughaibuni ambako waliahidiwa kazi. La kusikitisha ni kwamba vijana hawa walipofika ughaibuni walipata kwamba kazi zenyewe ni za kujidhalilisha, wakawa kama waacha mbacha kwa mswala ambao kwa kweli uliishia kuwa duni kuliko mbacha yao. Wapo walioteswa na waajiri wao hata wakajiuma vidole na kutamani kusagika kwenye kinamasi cha uhawinde na ukosefu wa nafasi za kazi waliouacha nchini kwao.

Basi hii ilikuwa ya arubaini kwa sauna.

Polisi walipopashwa habari kuhusu maficho ya Bi. Kangara walishika tariki moja kwa moja hadi nyumbani kwake ambako waliwatia mbaroni Bi. Kangara na Sauna. Mabibi hawa walifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la ukiukaji wa haki za watoto, wakarambishwa miaka saba gerezani na kazi ngumu. Mwaliko alichukuliwa na polisi kuhojiwa. Polisi walijaribu kumhimiza Mwaliko kukumbuka kwao lakini hakuweza. Visa alivyokuwa ameshuhudia katika umri wake mbichi vilikuwa vya kusikitisha. Vilimtia utando ubongoni, asiweze kufikiria lolote. Alichoweza kukumbuka ni kwamba alikuwa na ndugu wawili: Umu na Dick. Alikumbuka pia kwamba alikuwa na mama mbaya ambaye hakuwapenda. Baba, kulingana na Mwaliko, alienda kwa Mungu, lakini alikuwa mzuri.

Polisi walimpeleka Mwaliko katika kituo kimoja cha watoto mayatima. Kituo hiki kilisimamiwa na watawa wa kundi la Mtakatifu Teresia. Hapa Mwaliko aliweza kuendelea na masomo, yeye na wenzake.

Sura ya Kumi

"Neema," alisema Mwangemi huku amemwekea mkono begani, "usiwe na mawazo finyu na hasi kuhusu kupanga mtoto. Wanasema wasemao kuwa ukimlea wako na wa mwenzio mlee. Hakuna udhaifu wowote katika kumpanga mtoto. Tumejaribu kupata mtoto, huu ni mwaka wa tano sasa. Si kwamba hatuna uwezo wa kupata kizazi. Umetunga mimba, si mara moja wala mbili, umefanikiwa hata kuilea mimba hadi ikakomaa, tukaweza hata kukipakata kilaika mikononi mwetu, lakini ... Haikuwa baraka yetu, mwanetu Bahati *was a sickle-cell case. She did not survive her first week.* Nilimtazama uhai ukimponyoka bila hata uwezo wa kumwokoa pamoja na kwamba mimi nina shahada ya uzamili katika uuguzi. Hujui simanzi iliyonivamia kukutazama wewe alfajiri hiyo, ukigaragara kitandani, unauguza donda la *CS*, na zaidi jeraha la kumpoteza mwana linaufanya moyo wako kutoja damu. Mke wangu, kubali tumpange mtoto, huenda hata Mungu akatujalia wetu halisi baadaye."

"Teddy," Neema alimwita Mwangemi kwa jina lake la Kiingereza, ndilo alilozoea, ndilo linalomkumbusha pendo lao, uchumba na ndoa, "si kwamba nakataa kumlea mwana wa mwenzangu, la hasha, natamani sana kukipakata kilaika, kiwe changu au cha mwingine. Hata hivyo, ninavyowazia

kumpanga mtoto, dhamiri yangu hunisumbua sana, hukumbuka nafasi ambayo Mungu alinipa ya kumpanga mtoto, lakini nikaitema kama masuo."

Maneno haya yalifungua pazia la jukwaa la mawazo ya Neema, akaanza kumsimulia mumewe, la, kuisimulia hadithi aliyoitunga yeye mwenyewe kwa matendo yake miaka kumi iliyopita.

"Siku hizo nilikuwa nikifanya kazi kama Hasibu Mwandamizi katika Hazina ya Kitaifa," alianza Neema, "asubuhi moja ya umande ilinipata nimeshuka kutoka kwenye daladala, nashika tariki kuelekea afisini. Mzizimo wa Julai uliidhulumu ngozi yangu laini, nikalaani msongamano wa magari jijini, ukosefu wa mahali pa kuegesha, na ada kubwa iliyotozwa walioazimia kuendesha magari yao hadi kitovu cha jiji. Laiti vinara wa jiji wangeboresha hali, ningeweza kulitumia gari langu. Ujia ulioelekea afisini mwangu ulikuwa katikati ya safu mbili za majengo ya zamani. Viambaza vya majengo haya vilihimili kila aina ya taka. Si maandishi yenye matusi, si michoro ya picha za wanawake mashuhuri na wanaume mashuhuri ambao wachoraji wake husema kuwa ndio waliowakweza vitini, si laini za michirizi ya mikojo ... vyote vilishindana kuyatia nakshi mahali hapa. Mtu alilazimika kupitia hapo akienda mchakamchaka huku ameiziba pua, huku akijihadhari asije akatia wayo kwenye dongo lisilokanyagika!

"Nilichapuka, nikapapita mahali hapa, nikawa ninakabiliana ana kwa ana na lima la taka lililojikita hatua mia moja kutoka afisi za Hazina ya Fedha. Biwi hili ambalo liliselelea hapa kwa miaka na mikaka lilikuwa mkabala mwa

dirisha la afisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Nilikuwa nyuma ya kundi kubwa la wapitanjia ambao walilipita jalala hili wakitazama kando kana kwamba wanahofia kitu fulani. Nilipolikaribia biwi hili, nilisikia sauti fulani, dhaifu mawazoni mwangu, 'Ng'aa! Ng'aa!' Niliipuuza sauti hii, nikidhani kuwa huu ni mwangwi wa sauti ya kitoto cha jirani yangu ambacho kilikuwa na mazoea ya kulia usiku kucha. Mara sauti hiyo ilisikika tena, ikanituma kutazama kando. Hapohapo katikati mwa kilima hiki cha taka, niliona karatasi ya sandarusi ikifurukuta katikati ya fondogoo la kila aina. Kufurukuta huku kuliandamana na kilio kile hafifu. Moyo uliniambia nijipitie kama walivyofanya wenzangu, hata baada ya kuniona nikichunguza kilichosetiriwa na mchafukoge huu wa vitu.

"'Usijitie kubeba mzigo ambao si wako,' sauti ya mpitanjia mwenzangu ikaniambia, 'je, umepata vijusi vingapi hapahapa vimetupwa vikajifia? Je, iwapo huu ni mtego wa kukupagaza wizi wa binadamu, utakuwa mgeni wa nani?'

"Hata hivyo, nguvu imara za kimaumbile zilinisukuma, nikainama kwenye mchafukoge huo wa taka. Nilitwaa ile karatasi ya sandarusi, nikaifunua na kupata kilaika cha kike. Nilipokigusa tu, kilitia vikono kinywani na kulala. Sasa safari yangu ilichukua mkondo mpya. Nilifululiza moja kwa moja hadi kituo cha polisi na kuwaelezea kadhia yangu. Askari alikisikiliza kisa hiki huku akiandika kwenye *OB*.

"'Wanawake ni viumbe wa kushangaza sana,' alisema afisa huyu huku akitikisa kichwa, 'ya nini kuilea mimba kisha kuja kutupa matokeo yake? Lipi linalogharimu zaidi, kutungua mimba au kujikopoa mtoto na kutupa? Mbinu bora za kuavya

mimba zipo, hata za kudhibiti uzazi zipo, nao wanazikaidi na kuambulia ujauzito huku wakijua hawawezi malezi. Viumbe hivi!' afisa yule alisema haya kisha akaendelea, 'asante sana bimdogo, natumai utakuwa radhi kuandamana nasi hadi kituo cha Watoto cha Benefactor. Huko mtoto huyu anaweza kufadhiliwa. Mara mojamoja hutokea wahisani wakawapanga, wakaishi katika familia halisi.'

"Mtawa Cizarina alitukaribisha afisini mwake kwa bashasha. 'Karibuni,' alisema, 'naona mmetuletea kilaika. Siku hizi imekuwa ibada kuvipokea. Juzi mmoja aliachwa hapahapa langoni mwetu, kafunikwa kiblanketi kikuukuu. Inatisha jinsi binadamu amezika hadhi na utakatifu wa maisha ya mja katika kaburi la sahau.'

"'Huyu hapa ameokotwa na binti huyu kwenye jaa la taka,' alisema askari, 'huenda akataka kukueleza kadhia yenyewe,' akaongeza.

"Nilimsimulia Cizarina kisa changu. Alikisikiliza bila kuonyesha hisia yoyote ya kushtuka, ila uso wake ulitwaa vituta vilivyoficha huzuni na kuudhika.

"'Asante sana, Neema, kwa utu wako,' akasema mtawa huyu, 'kitoto hiki kimepata kwao. Hapa, tutakiita Nasibu, Nasibu Immaculata. Najua itatokea familia hitaji kuja kutaka kumpanga kama mwanao. Siku hizi hata walio na watoto wao halisi hujitolea kuwachukua na kuwahalalisha wana wa wengine kuwa wao. Hata vijana kama wewe hutokea mara mojamoja wakawahalalisha watoto kama hawa kuwa wao hata kabla ya kufunga nakidi,' akaongeza Cizarina.

"'*Sista*, unawezaje kumrithisha mwanagenzi mtoto? Mtu utawezaje kulea ikiwa hata hujaulimbuka uzazi?' nikamuuliza.

"'Haya yametokea. Kumbuka hata mtu anapopata mtoto wa kwanza huwa mwanagenzi wa uzazi na ulezi. Isitoshe, kutoa ni moyo; wanaojisabilia kuwachukua wana hawa huwa na mioyo kuza. Na usidhani tunawakabidhi wana hawa kiholela. Tunawahoji, na tukiridhika kwamba ni watu thabiti kiroho, kihisia na kimawazo, tunawarithisha wana hawa kisheria,' Cizarina alinifafanulia.

"Hadi sasa najutia kutouzingatia ushauri wa Cizarina kwamba hata mimi naweza kuhojiwa, na nikifaulu ninaweza kuhalalishiwa Immaculata. Mungu alikuwa amenikabidhi mtoto, nami nikamkataa kwa kujiona kuwa aliyetingwa na kazi nyingi, hivyo kitoto hicho kingekuwa mzigo. Fikiria wewe, Teddy, hata niliwahi kuwaza kuwa siwezi kumpanga mtoto huyu, kwani sijui ukoo wake. Je, ikatokea kuwa nasaba yao ni ya watu wenye kifafa au hata wendawazimu? Nani atashinda hospitali akikiuguza? Laiti ningalijua," alisema Neema na kukata usimulizi wake ghafla huku akifuta machozi na kumalizia kilio kilichomjaa kifua tele.

"Neema, mke wangu," alisema Mwangemi, "usijisulubu kwa 'kosa' ambalo ulilitenda kwa kutokuwa na ufahamu bora wa malimwengu. Hayo yamepita. Immaculata hakupangiwa kuwa mwanao. Inaridhisha kwamba wewe ndiwe uliyemwokoa. Labda angekuwa kitoweo cha mataya ya majibwa koko, labda hata angeambulia kichomi, kikampoka roho yake changa. Hayo sasa yamepita, si ndwele hasa. Ninalokuomba ni kwamba uridhie rai yangu ya kumpanga mtoto. Ukitaka tunaweza kwenda hapohapo kwenye kituo cha watoto cha Benefactor. Haiyumkiniki kuwa tutampata

Immaculata, lakini sina shaka kwamba tutapata mtoto. Sisi wenyewe ndio tutakaomuumba mwana huyu kihulka kutokana na malezi yetu."

Neema alikubali rai ya Mwangemi na leo hii wamo afisini mwa mtawa anayekisimamia kituo cha watoto cha Benefactor. Neema anasikitika kwamba hakumpata Cizarina ambaye alikuwa ameondoka na kurudi kwao Ughaibuni. Aliyeshika usukani ni Mtawa Annastacia Mwale.

"Karibuni," alisema Mtawa Annastacia, "tulipata ombi lenu kuhusiana na suala la kumpanga mojawapo wa watoto wetu. Tuna kijana mmoja wa kiume. Ikiwa mtafaulu katika mahojiano nitakayowapitisha, kituo hiki kinaweza kuwatayarishia na kuwakabidhi stakabadhi rasmi za kumpangia mtoto huyu. Baadaye nitazungumza na mtoto mwenyewe kabla yanyi kuja kumchukua. Ni kijana mchangamfu. Kila mara huniambia kuwa ana ndugu wawili ambao hajui walikopelekwa na *Auntie*. Yaelekea kuwa ni yatima, kwani yeye husema kuwa baba yake alienda kwa Mungu. Husema pia kwamba mama yake hampendi. Hili huenda likamfanya kutomwamini sana Neema. Ni jukumu lako Neema kumsadikisha mwana huyu kwamba unaweza kuaminika."

Mahojiano yalikamilika, nao Mwangemi na Neema wakaondoka wakitarajia kurudi kumchukua mwanao.

******

Utulivu na fahari ya uzazi na ulezi ulimvaa Neema adhuhuri hii ya mwezi wa Disemba. Yeye na Mwangemi walikuwa

wameketi afisini mwa Annastacia wakingojea kumchukua mwanao. Tayari wamekutana naye japo kwa muda mfupi tu alipojuzwa kwao na mtawa huyu. Hata wanapomsubiri mwana huyu aletwe, Mwangemi anahisi kwamba familia yake imekamilika.

"Kumbe hata mja akafanikiwa vipi kielimu na kitaaluma, maisha yake huwa ombwe bila mwana?" alijisemea kimoyomoyo.

Sasa Mwangemi anamshukuru Muumba kwa neema hii. Anajua kuwa maisha yake yamepata changamoto mpya, ana kiumbe ambacho kama udongo, kinahitaji kufinyangwa. Anajua kwamba umahiri wake na mkewe katika ufinyanzi huu ndio utakaoamua watamkuza kiumbe wa aina gani.

"Nitataka mwana huyu awe muuguzi kama mimi. Wahasibu wana adha zao, wanapima viwango vya matumizi ya kila kitu, hata hewa yenyewe wanataka waifanyie makadirio ya matumizi!" Mwangemi alimnong'onezea Neema mawazoni huku akitabasamu.

Mwangemi alizinduliwa kutoka mawazoni na mlio wa kitasa cha mlango, kisha sauti tulivu ya Mtawa Annastacia,

"Karibu kijana, keti."

Mwangemi alimtulizia macho kijana huyu, mrefu na mwembamba, mwenye sura jamali. Macho yao yalipokutana, kijana alitabasamu na kudhihirisha meno meupe pepepe ambayo yalimkumbusha binamu na rafiki yake Mwangeka. Hapohapo nyoyo za waja hawa wawili ziliungana, kila mmoja akawa anajisemea kimyakimya, "Haikosi huyu atakuwa rafiki wa dhati."

"Mwaliko," alisema Mtawa Annastacia, "huyu hapa ni Bwana Mwangemi na huyu hapa ni Bi. Neema. Kama nilivyokujuza hapo awali, wamekuja kukuchukua kwenda kuishi nao kama mwana wao. Nimeisha kukwambia kuwa hawana watoto wengine. Wewe ndiye utakayekuwa kifunguamimba na pengine kitinda mimba wao. Wao wenyewe wameisha kukubali kukutunza kama wazazi, na hivyo utaweza kuendelea na masomo. Utapata marafiki wengine huko. Nitakuja kukutazama mara kwa mara."

Mwaliko alimtazama Bi. Neema kwa hofu iliyojaa mapenzi. Neema alirudisha mtazamo huu kwa tabasamu ambalo liliupeperusha woga na shaka ambayo Mwaliko alikuwa nayo. Aliondoka pale alipokuwa amesimama, akamkumbatia Neema na kusema, "Nitakwenda nawe mama."

Neema, huku chozi la furaha likimdondoka, alimkumbatia Mwaliko kwa mapenzi ya mama mzazi. Alihisi kama aliyezaliwa upya. Sasa amepata kizazi. Cheko ambalo walimwengu wamekuwa wakimchekea—ati anashindwa hata kulea mimba, ati anazaa watoto wenye upungufu kwa sababu aliavya mimba nyingi akiwa shuleni—litakatika. Kitoto hiki kitakuwa mwenzi wake, kitampa mshawasha zaidi wa kufanya kazi ili kukikimu. Si hoja kuwa si chake halisi, heri nusu shari kuliko shari kamili.

******

Mwaliko alilelewa na Mwangemi na Neema kwa tunu, tamasha na nidhamu. Aliinukia kuwa ghulamu mwenye nidhamu ya hali ya juu, akiwaheshimu wazazi na majirani na akiwatii walimu wake. Hata alipohitimu masomo yake ya kidato cha

nne na kujiunga na chuo kikuu kusomea shahada ya Isimu na Lugha, Mwangemi na Neema walijua kuwa juhudi zao za malezi hazikuambulia patupu. Walikuwa wamechangia katika kumpa tegemeo mwana wa mwenzao.

******

Miaka mitatu imepita baada ya Mwaliko kukamilisha masomo yake ya chuo kikuu. Amejisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu. Ameajiriwa na kampuni ya magazeti ya *Tabora* kama mhariri katika kitengo cha biashara. Mwaliko anaifanya kazi yake kwa bidii ya mchwa. Haishi kuwashukuru wazazi wake ambao walijisabilia kumwelimisha licha ya kuwa hakuwa mwanao halisi. Daima huhisi ya kwamba ana deni kubwa la kulipa kwa Neema ambaye alimlea kwa upendo na uthabiti mkubwa. Kila mara Mwaliko hujiuliza moyoni kwa nini jaala ilimnyima Neema mwana.

"Huyu ana imani," Mwaliko alijiambia, "si kama mamangu mzazi ambaye aliithamini furaha yake kuliko watoto wake. Dada Umu aliniambia kuwa mama yangu aliniacha nikiwa na umri wa miaka mitano. Sikumbuki kumwona siku alipoenda lakini nakumbuka kwamba alipenda kujishika nyonga wakati akizungumza na baba. Alipenda pia kumfanya baba yangu kujiinamia na kukataa kula. Siku nilipoacha kumwona nyumbani mwetu baba alishinda kutwa kashika tama japo yeye baba alitukataza kushika tama, akisema kuwa kushika tama hukaribisha umaskini na ukiwa. Nadhani siku hiyo baba alikumbatiwa na ukiwa na umaskini wa kumpoteza mke wake," Mwaliko alijisemea.

Mwaliko alitamani kuona siku ambayo angekutana na ndugu zake. Ingawa hakuwahi kukutana nao tangu siku waliyotenganishwa na Sauna, moyoni alihisi kuwa walikuwa hai. Mama Neema alishinda akimkumbusha kuwa siku moja atawaona ndugu zake. Siku moja Mwaliko na baba yake, Mwangemi, waliamua kwenda kuuvinjari mji. Ilikuwa siku ya kuzaliwa kwa Mwangemi, naye mwanawe aliamua kumnunulia baba yake chakula cha mchana. Hii ilikuwa 'siku ya wavulana' kama walivyozoea kusema siku ambazo hawakutaka kuandamana na Neema. Kwa hivyo Neema alibaki nyumbani pamoja na mpwa wake Cynthia ambaye Neema alikuwa amemchukua kumtunza baada ya wazazi wake kufariki kutokana na maradhi fulani.

"*Mum*, yapo mambo ambayo baba na mwanawe wa kiume huhitaji kuzungumza faraghani," Mwaliko alimwambia Neema alipong'ang'ania kuandamana nao.

"Mambo gani hayo?" aliuliza Neema. "Zamani ulituambia matumaini na mashaka yako sote wawili. Ama unataka kutuletea mkaza mwana na unachelea kuwa mama atamchambua asimbakize?" Mwaliko alicheka kwa haya, akamshika mama yake begani kama kawaida yake na kumuaga kwaheri ya kuonana.

Mwaliko ndiye aliyeendesha gari siku hiyo; *Birthday Boy* akaambiwa apumzike. Walifika katika hoteli ya Majaliwa saa sita unusu adhuhuri, wakaketi mahali ambapo walikuwa wamezoea kuketi kila mara ambapo hawakutaka kughasiwa na pitapita za watu. Mhudumu alikuja akawapa menyu kutazama. Baadaye waliagiza chakula na kuanza kula kimyakimya.

"Baba," alianza Mwaliko, "unadhani ndugu zangu wako hai? Miaka mingi imepita bila ya hata kupata fununu yoyote kuwahusu. Sijui kama walibahatika kunasuliwa kutoka vitimbi vya dunia. Labda hata wamekufa. Labda mama alibadilika, akaenda kuwatafuta."

Mwangemi alimtazama mwanawe kwa imani. Laiti angalijua waliko wana hawa angalikwenda kuwatafuta, akawalea pamoja na mwanawe Mwaliko. Lakini hakujua angewapata wapi. Alikuwa ametembea katika vituo mbalimbali vya watoto mayatima lakini hakuwapata.

"Mwanangu," alisema Mwangemi, "ndugu zako wako hai na bila shaka mtakutana."

"Tutakutana vipi na hali ni kama polisi walizizika juhudi za kuwatafuta katika kaburi la sahau? Yumkini hata wanajua waliko. Pengine hata wamepangwa na walionacho, nao polisi wanahofia kusema wasije wakavikata vyanda vinavyowalisha," alisema Mwaliko huku akishusha pumzi kama aliyelemewa na jambo zito. Hatimaye alijipurukusha kwa, "Hii haikuwa siku ya kukumbuka mawi niliyopata. Nastahili kuwazia tu neema niliyoipata baada ya kuwapata wazazi wengine. Kweli hata mimi sina fadhila. Ni wangapi katika umri wangu waliowahi kuwa na wazazi wanne? Karibu baba, *happy birthday*; furahia siku hii yako."

******

"*Happy birthday*, Umulkheri," Mwangeka alimwambia Umulkheri huku kainua bilauri ya sharubati kuigongesha kwenye bilauri ya Umulkheri.

"Happy birthday, Engineer Umulkheri Lunga–Mwangeka," alisema Apondi huku akimtazama Mwangeka kwa nia ya kumkosoa.

"Thank you, Mummy, for reminding Daddy that there is another engineer in the family," Umu alisema kwa bashasha, "baba, ningependa kukujuza rasmi kwa Mhandisi Umulkheri Lunga–Mwangeka."

Mwangeka na familia yake walikuwa wametengewa chumba maalum katika hoteli ya Majaliwa kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Umulkheri. Sophie ndiye aliyepachagua pahali hapa. Alipaona kuwa panapofaa kusherehekea kuzaliwa kwa dada yake ambaye kuzaliwa kwake katika familia hii kulikuwa majaliwa kwa Sophie.

Umu aliwatazama wazazi wake kana kwamba ndio anawaona kwa mara ya kwanza. Mawazo yake yalirudi shuleni, siku ile walipokuja kumchukua. Anakumbuka maneno ya Mwalimu Dhahabu kwake.

"Umu, hawa ni marafiki wangu wa chanda na pete. Ni watu wakarimu na wenye imani. Hutajuta kulelewa nao. Watakukidhia mahitaji yako yote ya kihali, kihisia na kimali. Usichelee kuwafunulia moyo wako uonapo mashaka. Zaidi, watii jinsi ulivyowatii wazazi wako halisi."

Na kwa kweli Umu hajawahi kujuta tangu alipoingia nyumbani mwa Mwangeka na Apondi. Anakumbuka imani ya Apondi na Mwangeka. Anakumbuka kujitolea kwao kumwelimisha. Anakumbuka nasaha yao ya kila mara. Anakumbuka urafiki wao wa dhati ... Hata anapowaelekezea macho sasa hivi hawaoni. Anachoona ni malaika wa heri

waliotumwa kutoka mbinguni kumwokoa yeye na ndugu yake Dick. Umu alipomfikiria Dick hakuweza kujizuia. Machozi yalifurika machoni, yakatiririka, akalia kama mtoto mdogo. Wazazi wake ambao walijua kilichokuwa kikimliza walimwacha kuupunguza mwemeo wa hisia zilizokuwa moyoni mwake.

"Mama na baba, nawashukuru sana kwa hisani yenu. Nimetembea kwingi katika umri wangu mdogo huu lakini sijapata kuwaona waja wenye utu kama nyinyi, labda Babu Ridhaa ndiye anayewakaribia. Usiku nilipotoka Mlima wa Simba nilijua kuwa maisha yangu yameingia katika mkondo wa maangamizi. Nilidhani kuwa huo ndio uliokuwa mwisho wa masomo yangu. Sikuotea kukamilisha hata kidato cha pili. Lakini nitazameni hapa nilipo. Nina familia. Nina shahada ambayo nyinyi wenyewe ndio mlioidhamini. Ndugu yangu huyu, Dick, ameweza kujiendeleza kimasomo kwa msaada wenu. Sasa anajitegemea. Sina cha kuwapa nyinyi. Nawaombea thawabu za Mungu, hapa duniani na ahera," Umu alisema haya huku akifuta machozi kwa kitambaa alichopewa na Sophie.

Mwangeka alimshika begani bintiye na kumshukuru kwa imani yake kwao. Apondi naye alimwambia Umu, *"Come on girl,* usizungumze kana kwamba wewe tu ndiye uliyefaidika kuwa mwana wetu. Nani aliyejua kuwa ningepata kuwa na binti mwingine? Ni mara ngapi ambapo mimi na baba yako husafiri na kukupakaza ulezi wa ndugu zako hawa? Mimi ndiye wa kukushukuru. Umeweza kumwelekeza Sophie katika kipindi hiki ambacho anatafuta ujitambuaji. Wewe

pekee ndiwe dawa ya hasira ya Sophie ya kivolkano. Bila wewe malezi ya hawa wadogo wako yangekuwa magumu mno."

"Umu, unakumbuka siku uliponiambia kuwa utatulea mimi na Mwaliko kwa viganja vyako?" alisema Dick, "siku hiyo nilitazama vikono vyako nikashangaa jinsi unavyoweza kutulea. Hata hivyo, nimekuja kuamini kwamba ulijua kuwa unaweza. Kutokata tamaa kwako kunashangaza. Siku niliyokutana nawe katika uwanja wa ndege, tukasafiri pamoja, ndiyo iliyokuwa siku ya heri zaidi kwangu. Nasaha uliyonipa ilinifunza thamani ya maisha. Ndio, nilikuwa nimeamua kubadilisha maisha yangu, na nilikuwa nimeanza hata kupona kutokana na donda lililosababishwa na usafirishaji wa bidhaa haramu. Hata hivyo bila kuwa na mwelekezi ningerudia uwele wangu, yakawa yale ya mwenye kovu sidhani kapoa. Nakushukuru kwa kunielekeza kwa wazazi wetu hawa. Wamenilea kama mwanao. Baba Mwangeka hapa amenifunza uwajibikaji. Kila ninapomjia kwa ushauri, hata wa kikazi, hasiti kuniauni. Nawashukuru sana, *Mum* Apondi, Baba Mwangeka, Sophie na Don Ridhaa (hili ni jina ambalo Dick alimrejelea kitinda mimba wa Mwangeka kwalo). Changamoto ambazo mmekuwa mkinipa mara kwa mara zimeniwezesha kuinua kiwango changu cha maisha. Mlinipokea kwenu japo hatukuhusiana kwa damu wala usaha. Tulipokutana nilikuwa na kiduka kimoja tu cha kuuzia vifaa vya simu. Hivi sasa nahesabiwa katika safu ya wanajamii mashuhuri katika kuendeleza TEKNOHAMA. Nimekuwa kielelezo kwa vijana wengi ambao awali waliamini kwamba mhalifu hawezi kubadilika na kuudhibiti mustakabali wa maisha yake. Biashara yangu hii ya vifaa vya mawasiliano

ya kisasa imebuni nafasi nyingi za kazi kwa wanyonge ambao wangekuwa mawindo rahisi ya wahalifu. Yote haya yamewezekana kutokana na mwongozo mlionipa nyinyi. Zaidi, utulivu nilioupata nilipoambulia familia hii ulinipa msukumo kila mara nilipokabiliwa na ndaro. Sina cha kuwapa, nawaombea mpate neema na utulivu katika utu uzima wenu; sisi wana wenu tuweze kuwauguza ndwele za utu uzima," Dick alimaliza usemi wake huku kila mmoja katika familia hii akijifuta machozi.

Taathira ya hotuba ya Dick ilikuwa bado inaigonga hadhira yake Mwangeka aliposhtukia mtu kamshika begani na kumwita, "*Vuuuk!* Engineer *Vuuuk!*" Mwangeka alimtambua aliyekuwa amemshika hata kabla ya kumtazama. Kuna mtu mmoja tu katika ulimwengu huu ambaye humwita kwa jina hili. Huyu ni binamu yake Mwangemi, almaarufu, Tesi. Historia yao ni ndefu, tangu zile siku za Babu Msubili ...

"Tesi! Sadfa gani hii? Unafanya nini hapa? Ulikuja lini jijini humu? Yu wapi wifi Neema? Nilisikia mtoto wenu amehitimu chuoni! Ajabu hatujapata kukutana naye," Mwangeka aliyauliza maswali haya moja baada ya lingine bila kumpa mwenzake muda wa kujibu hata la kwanza. Wengine walimtazama wakishangaa kwa nini hata hamwachi mgeni akawasalimu.

"Baba, mwache *uncle* atusalimu kwanza," Ridhaa alisema. "*Hi uncle*," Sophie na Umu walisema kwa pamoja. Mwangemi alijipapatua mikononi mwa Mwangeka na kwenda kuwasalimia shemeji Apondi na watoto.

"Hii ni sadfa kubwa sana. Mimi huwa siji hapa sana lakini mwanangu Mwaliko aling'ang'ania kunileta hapa kwa chakula

cha mchana. Bila shaka *Vuuk* unakumbuka kuwa hii ni siku ya kuzaliwa kwangu!"

"Nakumbuka sana. Na kweli hii ni sadfa kwa sababu pia ni siku ya kuzaliwa kwa binti yangu Umulkheri."

"Ukweli? Basi *happy birthday, Umu,*" alisema Mwangemi.

Umu hakusikia alichoambiwa na Mwangemi. Yeye na Dick walishtuka sana kusikia Mwangemi akitaja jina la Mwaliko. Walishangaa ikiwa hii pia ni sadfa nyingine, kuwa Mwangemi ana mtoto mwenye jina kama la ndugu yao mchanga! Ama ndiye huyo ndugu yao? Mwangeka aliyaona mabadiliko yaliyodhihirika kwenye vipaji vya Umu na Dick, akawa anajiuliza kuhusu kichocheo cha hali hii. Kwa mbali alikumbuka Umu akimtajia jina la ndugu yao mdogo—Mwaliko—ingawa hakutaka kuamsha fadhaa zaidi kwa kuuliza kuhusu mwana huyu wa Mwangemi ambaye tangu hapo akijua ni wa kupanga. Alingojea mambo yajitanzue yenyewe. Alikuwa amesikia kuwa binamu yake ana mtoto wa kupanga, lakini hakutaka kumdadisi hapo awali kuhusu habari hizi asije akafufua vidonda ambavyo vilikuwa vimepona.

"Hey," Mwangemi alisema huku akimpungia mkono barobaro mmoja mrefu kiasi, mwenye sura jamali, "njoo nikujuze kwa yule binamu *Vuuk* ambaye hukwambia habari yake kila mara."

Mwaliko aligeuka na kuelekea alikokuwa baba yake, tabasamu lake likidhihirisha meno meupe pepepe yenye mwanya wa kupendeza. Umu alimtazama ghulamu huyu kwa tuo. Kutembea kwake, uso wake wa mviringo, ukunjufu wake, nywele zake za koto ...

"Mungu wangu! Huyu si ndugu yangu Mwaliko?" alisema Umu kimyakimya. Dick naye alikuwa kaghumiwa, hajui la kusema. Anamtazama mnuna wake kana kwamba ni *Mr Super Man* katika sinema za kijasiri. Wote wawili walitazamana, kila mmoja akiapa moyoni kuwa amewahi kumwona kiumbe huyu mahali, lakini hakuna aliyethubutu kunena.

"Mwaliko, huyu ni binamu Mwangeka, yaani *Vuuk*. Unakumbuka kile kisa ambacho hukusimulia kila mara kuhusu mimi, *Vuuk* na babu?"

Mwangeka alitoa kicheko kikubwa, na katika kipindi kidogo hicho akayaleta maisha yake ya kisogoni mbele ya kipaji chake. Mawazo yalimvuta nyuma, siku zake za ushujaa. Siku ambazo ndizo zilizozaa cheche za mapenzi yake kwa taaluma ya uhandisi. Hata anapokumbuka siku hii anajiambia kimoyoyo, 'Kweli mimi nilikuwa sikio la mbuzi ambalo nyanya alizoea kusema husikia chunguni. Tesi, binamu Tesi ...'

Mwangeka na Mwangemi walikuwa mabinamu wawili waliopendana kama chanda na pete. Urafiki wao ulishinda wa maumbu, ulikuwa zaidi ya wa ndugu wa toka nitoke. Ulikuwa ule usuhuba wa mmoja akijikwaa mwingine anauhisi uchungu wenyewe! Babake Mwangeka alikuwa mdogo wa babake Mwangemi, ikawa Mwangemi anamwita baba Mwangeka Bamdogo, na Mwangeka anamwita baba Mwangemi Bamkubwa badala ya ami. Siku hizo Dkt. Ridhaa alikuwa akifanya kazi katika hospitali ya wilaya karibu na kijiji chao. Hivyo mkewe na watoto waliishi katika nyumba aliyokuwa amejenga katika boma la babake.

Urafiki wa vijana hawa ulianza kimzaha, ukachochewa zaidi na tabia zao za mizaha, mizaha ambayo ikivuka mipaka wakati mwingine na kutibuka usaha. Siku hiyo Mwangeka alikuwa amekamilisha uundaji wa gari la kienyeji maarufu kijijini kwa jina *Ngookoo*. Ni kama hivi vigari vya kifahari wanavyoendesha watoto wa wakwasi huko katika maeneo ya burudani. Mwangemi alipita pale na kumwona mwenzake amekenua meno kwa furaha; akiwa kama mhandisi wa humu mwetu baada ya kuvumbua lile gari maarufu kwa jina *Pioneer*. Pongezi *Engineer Vuuk*. Naona hili litatusaidia kumhepa *Kũmũkũ*. Wote waliangua cheko ambalo lilimfanya *Kũmũkũ* mwenyewe kuchungulia kutoka dirisha dogo la kibanda chake. *Kũmũkũ* ilikuwa lakabu ambayo vijana hawa walikuwa wamembandika babu yao; lakabu ambayo ilikuwa msiba wa kujitakia—kutokana na ukali wake na tabia yake ya kukohoakohoa kama mgonjwa wa kifua kikuu, kama walivyodai vijana hawa.

Uvumbuzi wa Mwangeka uliuunga zaidi urafiki wao. Licha ya kuwa na adui mmoja—babu yao—walikuwa na mazoea sawa. Mwangeka na Mwangemi walipenda michezo, usidhani eti michezo ya kawaida ya kitoto kama vile mwajificho, mchezo wa baba na mama ... La, hasha! Michezo yao ilihusu uvumbuzi na vituko vya kishujaa. Miongoni mwa mambo mengi ambayo walipenda Mwangeka na Mwangemi ni sinema pendwa, zile za kijasusi, kipelelezi na vita. Baadhi ya sinema walizibuni wenyewe. Katika maigizo haya yao ya kubuni, kila mmoja alipenda kujitambulisha na majagina wa kihistoria katika jamii mbalimbali za ulimwengu. Mmoja wa miungu wao alikuwa *James Bond*. Huyu alipendwa kwa sababu ya ujasusi wake. Wengine walikuwa majagina wa vita,

hasa majagina ambao walipigana vita kueneza himaya zao katika mataifa jirani. Sikuacha kushangaa jinsi vitoto hivi ambavyo vilikuwa ndio vinaingia katika darasa la sita viliweza kujua mighani na tendi kama vile Utendi wa Shaka Zulu ambaye enzi zake alilihangaisha eneo zima la Kusini mwa Afrika! Lakini, kama ungejaribu kuviuliza, ungejibiwa,

"Historia, dada, historia tumeisoma na si kuisoma tu, tunaiishi hasa! Fahamu kuwa historia haikubuniwa na Wazungu! Tuliibuni wenyewe; akina Mwangeka, Lwanda Magere, Kisoi Munyao, Kinjeketile ..." Mwangemi angejibu kabla ya kukatwa usemi.

"Nasikia hata Mekatilili pia alijaribu," angeongeza Mwangeka kwa sauti ya chini yenye muonjo wa bezo.

Katika kupalilia vipawa vyao vya uigizaji, Mwangeka na Mwangemi walipenda kupiganisha majogoo, huku wao wakiwa mashabiki. Kila mmoja aliwakilishwa na jogoo mmojawapo. Nakumbuka siku moja nilipobahatika kuitazama sinema hii. Ilikuwa siku ya Jumamosi. Mama na mkaza ami walikuwa wameenda sokoni. Siku hizo waliopanda mboga walikuwa wachache. Sehemu hii ilikuwa kame na maji ya mabomba yalikuwa kaburi la Baniani. Ilibidi kuamka mapema ili kuziwahi mboga nzuri, ule msemo wa 'atanguliaye kisimani hunywa maji maenge'.

Basi baada ya kiamsha kinywa nilimsikia Mwangeka akimwambia Mwangemi,

"Leo unaonaje tukiwajaribu mababe wetu? Ni vizuri kuanza mapema kabla ya jua kufika utosini. Unajua tena nyanya alisema kuwa majeruhi huvuja damu zaidi jua likiwa kali."

Mwangemi alikubaliana na wazo hili. Utashangaa jinsi ambavyo vijana hawa walidiriki kusababisha mgogoro kati ya majogoo. Hilo hata mimi sikuwahi kuliwazia hadi Jumamosi hii. Ilikuwa rahisi kuwajaza majogoo wote wawili tamaa na hamasa za kupigania windo. Siku hizo hakukuwa na ile misala ya mashambani ya mashimo ambamo mtu huhitajika kuchutama ili kukamilisha haja zake. Vichaka vilitosha kwa wengi! Usiniulize jinsi watu hawa walivyoweza kukinga dhidi ya uchafuzi wa mazingira pamoja na magonjwa yanayoandamana na uchafu huo! Hata wale waliokuwa na misala kama familia ya akina Mwangeka hawakuwa na nidhamu ya kuitumia, au tuseme walihiari kufanya kama wenzao vijijini. Unajua wewe jinsi vijana, kama bendera, hupenda kufuata upepo. Isitoshe, Mwangeka na Mwangemi walihofia kwamba wangetengwa na vijana wenzao kwa kujitia 'Uzungu'.

Mwangemi na Mwangeka walijua kuwa hekima ya jadi inasema kuwa kuku habagui cha kula. Walijua kuwaelekeza majogoo wao kwenye nyanja zilizokuwa nyuma ya nyumba ambako walijua kuwa watoto wenzao wamekamilishia haja zao. Kisha wangewaelekeza mashujaa wao kupigania windo, kila mmoja akimshajiisha shujaa wake. Vijana hawa waliamini kuwa, ikiwa wafalme walipigana kufa na kupona ili kueneza tawala zao na kuwadhulumu watawaliwa, basi majimbi hawa watapigana kwa jino na ukucha, si kwa ajili ya kujaza matumbo yao tu, bali pia kwa lengo la kupata fahari; fahari ambayo pia ingewaendea Mwangemi na Mwangeka.

Vita vingeanza, huku, "Twende Kiko, Kavyu chini, Kiko huyooo ..." hadi pale ambapo wangemwona mmoja

wa majogoo anatoja damu na kukimbia. Huku nyuma mwenye jogoo aliyeshinda angeinuliwa juu na mwenzake na kupewa *ride* ya *ngookoo*. Mara nyingi jogoo wa Mwangeka ndiye aliyeshinda huku Mwangemi akipagazwa jukumu la kumzungusha Mwangeka kijiji kizima. Wakati huu wote Mwangeka akiwapungia mikono wapita njia jinsi rais hufanya katika ziara zake vijijini.

Wakati kama huu Mwangeka angejitanua kifua na kusema, "Mimi ni mwana wa mhunzi, na bila shaka wa mhunzi asiposana huvuvia. Babangu hakuna linalomshinda katika uwanja wa upasuaji. Ni kama yule mbabe wa kivita aliyepigana na *Akavi* kuwaokoa mifugo wa ukoo wetu kutokana na kutekwa na jamaa hawa ambao siku hizo wakiamini ndio waliotunukiwa na Manani jukumu la kuwamiliki ng'ombe wote. Baba huniambia kuwa mara nyingi huwafufua maiti katika chumba cha wagonjwa mahututi, akawatoa kwenye mashine na kuwarejeshea uhai, jamaa zao wakitazama hivi hivi! Hilo usilione dogo, Tet! Baba si tofauti na huyo Fumo Liyongo tuliokuwa tukihadithiwa na nyanya! Ati bwana huyu angeweza kuinua tani, ngapi vile za chuma?"

"Mia moja!" Mwangemi angemkumbusha mwenzake kila mara.

Jumamosi hii kinyang'anyiro kilikuwa kati ya majimbi wawili—wa Mwangeka akiitwa *Kyenza Kinyenyo* (Anayenyoa kabisa) na wa Mwangemi akiitwa *Mumina* (Kamaliza). Ndugu hawa hawakupenda walichokiita 'wingi' (watu wengine) katika michezo yao. Basi ilinibidi kukaa mbali na kuyaonjesha macho yangu mara mojamoja. Mwangemi ndiye aliyetafuta 'windo' la kupiganiwa. Kitali kilianza. Kyenza Kinyenyo

ndiye aliyeshambulia kwanza. Shungi lake kichwani lilikuwa kama kilemba! Mumina alilijibu shambulizi hilo kwa hamasa kubwa, macho yake mekundu mithili ya damu kayatunga kwa hasimu wake. Mashabiki wakaanza kushangilia na kuhongera. *"Come on, Kyenza Kinyenyo, give him another one, just like the other one!"* Mwangeka akahimiza, *"Go,* Kamaliza! *Go Mumina*! Ukoo wetu ni wa *go-getters."* Huu ulikuwa kama uwanja wa miereka usio na marefa. Fukuto lilizidi huku nikijawa na matarajio kama mtazamaji wa sinema ya upelelezi. Hatimaye Mumina alianza kuonyesha hisia za kunyong'onyea huku macho ya Mwangeka yakitwaa mng'aro, mng'aro uliobashiri ushindi, mng'aro uliomhakikishia mandari katika kijiji kizima akisukumwa na Mwangemi kwa *ngookoo*.

Hata hivyo, ghafla upepo ulibadilika! Mumina akapata nguvu mpya, usiniulize alizitoa wapi. Aliruka kama simba aliyejeruhiwa na kumpata Kyenza Kinyenyo kwenye jicho la kulia. Mumina juu, Kyenza Kinyenyo chini! Ule msemo maarufu wa babu yangu, 'Usiisifu njaa ya mbwa kabla usiku haujaingia ukahakikisha kuwa mbwa amelala njaa', ukatimia. Msemo huu ni sawa na methali ya Kiswahili, 'Mungu hamsahau mja wake', au hata bora zaidi, 'Kuregarega si kufa, kufa ni kuoza utumbo'. Ulikuwa wakati wa Kyenza Kinyenyo kufedheheka, na Mumima kutafahari. Kama kawaida yao Mwangemi na Mwangeka walipigana pambaja. Mwangeka alimpongeza Mwangemi kwa ushindi wake ambao alisema kimzaha kuwa hakuulalia wala kuuamkia. Waliwachukua askari wao na kuwapa punje za mahindi pamoja kana kwamba wanawafunza kusahau tofauti zao za hivi punde na kuwakumbusha kuwa asiyekubali kushindwa si mshindani!

Hii ilikuwa desturi ya vijana hawa kila baada ya vita vya majogoo.

Wakati uigizaji huu unapomalizika jua la utosini linanyemelea. Tunawatarajia walioenda sokoni kurudi. Kisadfa wakati huohuo Babu Mwimo Msubili akawa ndio anatoka kwenye shughuli zake za *'usili'* (ujaji). Babu alikuwa hakimu wa kienyeji aliyejulikana kote katika tarafa ya Heri. Kesi nyingi ambazo zilikuwa zimewashinda wazee na mabaraza ya kijadi aliziamua yeye. Haikuwa ibra kwake kutoonekana nyumbani kwa mwezi mzima! Hizo zingekuwa siku za maji mafu kwa Mwangeka na Mwangemi kwani wangecheza michezo yao bila 'jicho la kipanga', kama walivyoiita tabia ya babu ya kuchunguza shughuli zao. Babu alipokaribia ilibidi nijifiche kwani hakupenda kukutana na wanawake asubuhi. Kwa babu asubuhi huanzia jua la matlai mpaka saa saba. Mama alitukumbusha haya kila mara. Ndugu wetu wa kiume ndio waliotumwa kumpelekea babu uji, mimi na dadangu tukawa hatujongelei kijumba cha babu hadi pale tulipoona kuwa ku salama.

"*Nau* (Baba) husema kumwona mwanamke asubuhi ni nuksi kwa kuwa mtu hafanikiwi kwa atakalo," mama alizoea kusema. Kile ambacho sikuelewa, na ambacho nilichelea kukiuliza ni: "Je, hiyo nuksi haiwezi kusababishwa na mwanamke kumpikia huo uji asubuhi?"

Mwangeka na Mwangemi sasa wameshajipangusa majasho yaliyosababishwa na jitihada zao za kuwatakia ushindi mafahali wao. Wanahitaji kupumua kabla ya kuanza ziara yao ya baada ya vita. Mara nilisikia vicheko vya kitundu, kisha, mwigo wao wa kila siku: *kũmũkũmũkũmũkũũũ* kisha

kikikiki ... (kicheko). Hatimaye nilisikia babu akisafisha koo kwa utulivu huku akiwauliza:

"Mama zenu wameenda wapi?"

"Walienda sokoni," wawili hawa wakajibu sawia. Babu aliondoka, kisha nikasikia tena ule mwigo, *'Kũmũkũ, kũmũkũmũ, kũmũũũ* ... mama zenu wameenda wapi?', uliofuatwa na kicheko cha ushindi. Nilitoka mafichoni na kuwaonya dhidi ya utovu huu wa nidhamu. Vijana walinijibu kwa mzaha wao wa kawaida,

"Wewe nawe hujui kuwa kuna malumbano ya utani kati ya wajukuu na babu zao? Husikii hata nyanya akituita *husband*?" Sikujibu mzaha huu. Nilijua kwamba vijana hawa walikuwa wakichezea tope na bila shaka wangerukiwa.

Usiku huo kijiji kizima kilijua kuwa jogoo wake, *Ngumii ya Wathi* (mbwekea ngoma ya kienyeji), kama alivyojulikana babu na wanakijiji, amewika. Ulikuwa usiku wenye baridi kali, baridi ya mwezi wa Julai yenye kusababisha mzizimo kwa kondoo, hata wale wenye manyoya tumbi tele. Mwangeka alikuwa kajilaza jikoni, karibu na mafiga ili apate uvuguvugu. Haya yalikuwa mazoea yake kila jioni. Mzee Msubili alitambulisha kufika kwake kwa mkaza mwanawe kwa kusafisha koo.

"Mbaulanga—hili ndilo jina alilomrejelea Mama Mwangeka kwalo —je, Mwangeka yupo? Ningependa kumpa ujumbe ampashe Mutangili kesho asubuhi," babu akasema.

Mwangeka, ambaye mavune ya siku nzima ndio yalikuwa yanataka kuupisha usingizi, alisikia kwa mbali na kuchupa.

"Ndio babu, nipo hapa," akasema.

"Sawa mjukuu wangu. Midume haitakiwi kulala mapema. Njoo ndugu yangu nikutume," akasema babu.

Mwangeka aliamka na kuelekea mlangoni. Kabla hajakivuka kizingiti malaika yalimsimama, akajawa na kitetemeshi cha ajabu kilichotikisa nafsi yake nzima, akajiona kana kwamba anakabiliana na mojawapo ya madubwana ambayo nyanya alikuwa amewahadithia kuwahusu jioni iliyotangulia. Hata hivyo, alijipa kujipurukusha na hisia hizo na kukabiliana ana kwa ana na babu. Kabla hata hajahesabu moja alihisi mwanguko wa mshipi juu ya ngozi yake laini. Kabla hajadiriki kujitetea kwa lolote alitazama nyuma na kumwona sahibu wake Mwangemi, amevuvuwaa na kujikunyata kama kuku aliyemwagiwa maji. Mshipi ulifanya kazi kwa dakika mbili huku Mwangeka, ambaye kwa kawaida huwa mwoga kama kunguru anakabiliwa na adhabu ya babu akikitumbuiza kijiji kizima kwa siahi iliyotishia kuporomosha paa la jiko la mamake. Aliyatazama macho ya Mwangemi yaliyosharabu wekundu na kujua kwamba babu alikuwa ameutimiza usemi wa mwalimu wa kila mara kuwa *'Spare the rod, spoil the child'*, usemi ambao ndio uliokuwa mwongozo kwa walezi wengi kwani siku hizo iliaminika kuwa njia ya pekee ya kumshinikiza mtoto kutii ilikuwa kutumia mchapo.

Mamake Mwangeka na mamake Mwangemi walikilaani kitendo cha vijana hawa. Mwangeka na Mwangemi walilazimika kulala njaa kama adhabu kutoka kwa wazazi wao kwa kumwiga babu na kuwafanya kuonekana kama wametelekeza wajibu wao wa kuwaadilisha wanao. Hii ilikuwa adhabu ya kawaida siku hizo, hasa kwa wale waliozembea kazi. Mwangeka alijikunjia kitandani mwake, chanda

mdomoni. Moyo ulimsuta kwa kitendo chake cha utukutu, kitendo ambacho japo kilikuwa ibada kwake na Mwangemi, siku yao ya arubaini ilikuwa imefika. Kwa mbali aliisikia sauti ya ndege akiimba, sauti ambayo ilikuwa inayakariri maneno ya mwalimu wake wa dini:

Watoto sharti muwe watiifu kwa wazazi na watu waliowapiku umri. Hii ndiyo amri ya pekee yenye ahadi. Mkiwadharau wazazi eti kwa sababu mnaziona sera wanazoandama kuwa zimepitwa na wakati, mtakuja kukosa radhi, radhi ilo bora kuliko mali.

Mwangeka aliwaza ikiwa kweli uigizaji wao ungewekwa kwenye safu ya vitendo vya kikaidi, hasa pale uigizaji wenyewe haukunuiwa kutazamwa na kinachoigwa! Alikumbuka nyakati zote ambazo walimwiga babu jinsi fanani katika ngano aigavyo vitendo vya mmojawapo wa wahusika ili kukashifu vitendo hasi.

"Kumwiga babu hakukuwa ishara ya kukosa heshima. La hasha! Tuliiga tu ili kujiburudisha," alijiwazia.

Hata hivyo moyoni alijua kuwa uigizaji wao ulikuwa na jukumu lingine fiche, kumkumbusha babu kuwa alihitaji kuwa mtani wao, kama walivyo mababu wengine, badala ya kujitenga nao kama ardhi na mbingu. Hata njaa iliposalimu amri na usingizi kulegeza parafujo za mwili wake dhaifu, Mwangeka alishangaa ikiwa kweli Mwangemi alihisi uchungu ambao ulikuwa unamtafuna yeye.

******

"Basi *engineer* mwenyewe ndiye huyu," alisema Mwangemi. "Usicheze! Yeye ndiye aliyevumbua gari la kwanza la Kiafrika!"

Kauli hii ilimzindua Mwangeka, ikamtoa kuleee ... kwenye kisa chake na babu. Mwangemi alipomwangalia Mwangeka aliviona vipira vya machozi vikitunga machoni, akajua mwenzake ametoneshwa kidonda na kumbukumbu zake, akatabasamu.

"Lakini hayo yote yamepita, hiyo ilikuwa hatua ya ukuaji. Ilibidi tuipitie," Mwangemi alijisemea, kisha akamgeukia Mwangeka na kusema, "*Vuuk*, huyu ndiye mwanangu Mwaliko. Si mwana tu bali ni rafiki yangu wa dhati. Maisha yangu na ya Neema yangekuwa kaka tupu bila yeye," Mwangemi akamwambia Mwangeka huku akimshika Mwaliko begani.

Wakati wote huu Mwaliko hasemi lolote. Yu mbele ya aila ya Mwangeka kana kwamba ni igizo ambalo wanatazama. Mwangeka na Apondi wameona mshabaha uliopo kati ya Umu, Dick na Mwaliko. Yote yamewabainikia. Wanangoja kuhakikishiwa na Umu kuwa huyu ndiye ndugu ambaye wamekuwa wakimtafuta msitu na nyika. Mwaliko moyo wa udugu umemwambia kuwa hawa ni ndugu zake. Anapowatazama anaona mshabaha mkubwa kati yao na wale watoto walio kwenye picha ambayo baba yao Lunga alipigwa nao kabla ya mauko yake. Picha hii Mwaliko ameihifadhi katika buku lake la picha kama kumbukumbu ya familia yake. *Auntie* Sauna alizoea kumwambia kuwa hao ni Umulkheri na Dick.

"Kweli milima tu ndiyo haikutani. Huyu ni dada Umu na yule pale ni kaka Di," akasema Mwaliko kimoyomoyo huku akizidi kuwakazia macho.

Taratibu Mwaliko aliinua macho yake na kusema, "Dada Umu, Di, ni mimi. Ni mimi ndugu yenu. Ni hai. *Auntie* Sauna alishikwa na polisi. Baba Mwangemi alinichukua akanilea. Hata nina mama, Neema. Naona hata nyinyi mlibahatika kupata wazazi wazuri kama mimi."

Umu na Dick hawakungojea Mwaliko amalize. Walikimbia, wote wakamkumbatia ndugu yao, wakaanza kulia huku wakiliwazana. Sophie na Ridhaa nao walijiunga nao, wote wakakumbatiana na kulizana, baadaye wakashikana mikono, wakafanya mduara kama ule ufanywao na watoto wakicheza, ikawa kana kwamba wanaunga udugu upya. Wazazi walibaki wanatazamana bila kusema lolote. Umu aliwaomba wote waketi chini. Yeye aliketi baina ya wazazi wake wawili, kama alivyopenda kufanya kila mara.

"Nahisi kama nasimulia kisa kirefu chenye mwisho mwema," alianza Umu, "najihisi kama Kurwa katika novela ya *Kurwa na Doto* baada ya kumpata mchumba wake Faki ambaye alikuwa amenyang'anywa na pacha wake Doto. Kifo kilitupokonya mimi na ndugu zangu hawa baba ambaye ndiye aliyekuwa mlezi wetu wa pekee baada ya mama kutuacha. Kwa miaka mingi nimeishi nikidhani kwamba Mwaliko amekufa. Kumbe analelewa na binamu ya baba yangu? Tulipitia machungu makali katika utoto wetu lakini haya yote yalikuja kufidiwa tulipowapata nyinyi wazazi wetu. Asante sana *uncle* kwa kumlea Mwaliko, akawa mwana wa kutegemewa."

Wote walikaa kimya kumsikiliza Umu. Dick hakuacha kumshukuru Umu kwa tumaini alilompa kuwa siku moja atamwona ndugu yao. Mwaliko alimtazama Umu. Hakumbuki vyema jinsi sura yake ilivyokuwa siku zile katika Mlima wa

Simba, lakini jambo ambalo hawezi kulisahau kumhusu dadake ni ukarimu wake. Umu angempa Mwaliko chakula chake chote wakati Mwaliko aliposema kuwa chakula chake hakitoshi. Hata anapomtazama kwa macho yaliyofunikwa na vidimbwi vya machozi, anajua kuwa familia yao imerudiana, japo katika mazingira tofauti. Anamshukuru Mungu kimoyomyo. Anamshika baba yake mkono na kumwambia,

"Baba, unaona kuja kwetu hapa kumetuletea heri! Familia yetu imepanuka. Nimekutana na mabinamu ambao huwasikia tu ukiwataja. Tena imekuwa heri kuwa *Uncle* Mwangeka ndiye mzazi na mlezi wa ndugu zangu. Kweli nimesadiki maneno ya Mama Neema kila mara kuwa Mungu ni Mungu wa mayatima na wajane."

Mwangemi alimtazama mwanawe kwa imani na furaha kubwa, akasema, "Kweli kuja kwetu hapa kumetokea kuwa majaliwa kwetu sote. Huu ndio mwisho wa kutengana na ndugu zako. Sasa mnaweza kuanza kuujenga upya uhusiano wenu. Tunaweza hata kumtafuta mama yenu, huenda tukampata. Itakuwa bora akijua kuwa nyote m salama, mkamjuza pia kwa wazazi wenu wapya. Natumai kuwa nyote mmemsamehe."

"Hilo ni wazo zuri Tesi," Mwangeka alisema, "nimekuwa nikimwambia Dick ayawazie hayo, naye kila mara huniambia anangojea Umu ahitimu masomo yake na kurejea nchini. Maadamu Umu yu hapa, na isitoshe hata Mwaliko amepatikana, sioni kinachotuzuia kuanza kumtafuta Bi. Naomi. Ana haki ya kujua walipo wanawe."

******

Kile ambacho Mwangeka hakujua ni kwamba Bi. Naomi, baada ya kurudi kwao, hakuishi na wazazi wake. Uso una

haya ati! Alijiambia kwamba atatumia stashahada yake ya uhazili kutafuta kazi adunduize pesa kidogokidogo. Hali yake ya kiuchumi ikiimarika huenda akarudi Mlima wa Simba kumsaidia mumewe kwa malezi. Hata hivyo, azma ya Naomi ilikuwa dhaifu. Alihamia mjini na kuwa shangingi kwelikweli. Haukupita muda kabla ya kukumbana na Bwana Kimbaumbau, shaibu mmoja tajiri ambaye, baada ya kumweka Naomi kimada kwa muda, alimpitisha makuruhu yasiyomithilika; kusimangwa, kupigwa, na kuadhibiwa. Karaha hii ilimtia Naomi majuto makuu.

"Kipi kilichonipa kumkimbia Lunga wangu wakati ambapo alinihitaji zaidi?" alisema Naomi usiku mmoja ambao bahari ya dhiki ilikuwa imejaa isidiriki kupwa, "maskini Lunga, nimekusababishia mauko. Wanangu Umu, Dick, Mwaliko, sina uso wa kuwatazamia."

Naomi alijipangusa machozi, kisha akaanza kuzungumza kana kwamba anawahadithia wanawe yale yaliyotokea, kana kwamba anaungama makosa yake, wakitaka wamhukumu au wamsamehe.

"Siku nilipopigwa pute na Kimbaumbau, uchungu wa uzazi ulinituma kuwatafuta. Niliabiri chombo hadi Mlima wa Simba. Nilifululiza moja kwa moja hadi nyumbani, ambapo nilipata hapakuwa nyumbani tena bali mahame yenye kaburi ambalo lilijikita kunikebehi kwa unyama niliowatendea nyinyi. Nilikifyeka kichaka cha magugu kilicholibana kaburi la maskini mume wangu, nikanadhifisha kiambo, kisha nikaweka koja la maua juu ya kaburi.

"Wanangu, si kwamba sijawatafuta, hakika hamna kituo cha polisi ambacho sijabisha hodi. Ila naelekea kukata tamaa,

hasa baada ya majirani huko Mlima wa Simba kunijuvya kwamba Di na Mwaliko waliibwa na Sauna, nawe Umu uliondoka tu. Sijui walimwengu waliwatumbukiza kwenye handaki lipi la ufuska na ujangili. Najilaumu kwa yote yanayowafika sasa.

"Wanangu, sina lolote la kujivunia, ila nataka mjue kwamba nimeanza kuyajenga maisha yangu upya. Nimejifunza umuhimu wa kufanya kazi, japo ya pato duni, ili kujitegemea. Nimefungua kiafisi kidogo karibu na Chuo Kikuu cha Mbalamwezi. Huko ndiko ninakowapigia wasomi kazi zao chapa na kuisarifu miswada yao.

"Maskini wanangu, huenda tusikutane nikiwa hai, ila nawausia kwa kauli moja tu, msiache ubinafsi na tamaa kuupweza ubinadamu wenu."

******

"Ni kweli, mama ana haki ya kusamehewa, kwani hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika. Tutashirikiana kumtoa kwenye lindi ambalo ulimwengu huenda ulimsongomezea," Dick akasema.

Mwaliko aliitikia maneno ya Mwangeka na Mwangemi kwa kichwa, akamshika babake mkononi na kumwambia,

"Tutayawazia hayo baadaye. Muda wa kufanya hayo upo. La muhimu ni kwamba ndugu zangu wako hai. *Now it's time to get home. Young Neema is waiting for us.* Nina hamu kuu ya kumwambia majaliwa yetu ya leo."

2323 081

** Mwisho **

Fasihi Tambuzi ya Kiafrika (FATAKI)

Chozi la Heri

"Mungu wangu! Huyu si ndugu yangu Mwaliko?" alisema Umu kimyakimya. Dick naye alikuwa kaghumiwa, hajui la kusema. Anamtazama mnuna wake kana kwamba ni *Mr Super Man* katika sinema za kijasiri. Wote wawili walitazamana, kila mmoja akiapa moyoni kuwa amewahi kumwona kiumbe huyu mahali, lakini hakuna aliyethubutu kunena …

Tamaa ya kumiliki nyenzo za kujiinua kiuchumi na kisiasa, kama inavyodhihirika katika riwaya hii, inasambaratisha asasi za kijamii, pamoja na miundomsingi ya mshikamano wa kijamii. Maazimio yasiyofikiwa yanazua hali ya kuvunjikiwa—kihoro hasa. Lakini baada ya kiza kizito huja mawio ya uzawa wa jamii mpya yenye matumaini.

Assumpta K. Matei ni mtafiti na mwalimu mwenye tajiriba pana katika ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili katika shule za upili na vyuo vikuu. Kati ya taasisi alizowahi kufundisha ni Kenya High School na Catholic University of Eastern Africa. Ameshiriki katika majopo mbalimbali ya ukuzaji, utekelezaji na tathmini ya mitaala. Hivi sasa ni afisa katika Wizara ya Elimu, kitengo kinachoshughulikia tathmini ya mitaala.

ISBN 978-9966-068-18-7
Chozi la Heri
2010143000788
370.00 TBC
9 789966 068187

OnePLANET